# DHULUMA DHIDI YA VIJANA WA KIKE KATIKA RIWAYA ZA ROSA MISTIKA NA TUMAINI

ELIJAH MORARA OBURE

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI

C50/61761/2011

OKTOBA 2012

University of NAIROBI Library
0389223 9

# UNGAMO

Kazi hii ni matokeo ya juhudi zangu za utafiti pamoja na wasimamizi wangu na si kazi ya mtu mwingine haijawahi kuwasilishwa kwa mahitaji ya shahada ya uzamili katika chuo kikuu chochote kingine.

**MTAHINIWA**

**Sahihi:** ______________________ **Tarehe** 5/11/2012

**Elijah M. Obure**

Tasnifu hii inatolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na chuo Kikuu cha Nairobi.

______________________ 5/11/2012

**Dkt. Ayubu Mukhwana** **Tarehe**

______________________ 5/11/2012

**BI. Mary Ndung'u** **Tarehe**

# TABARUKU

Kazi hii naitabarukia wazazi wangu Peris Kwamboka na Marehemu babangu Stephen Obure kwa maazimio mema ya kunihimiza kutia juhudi katika masomo lakini Mola akamchukua babangu kutokana na kifo kichungu, kabla ya kushuhudia tamati ya mashauri yake mema katika masomo yangu.

## SHUKRANI

Utafiti huu umekamilika kutokana na usaidizi, uongozi na mchango wa watu wengi ambao ni vigumu kuwataja wote. Ningependa kutoa shukurani za dhati kwa Dkt. Ayubu Mukhwana kwa mawaidha na ushauri wake wa busara, mwongozo na masahihisho aliyonipa wakati nilipokuwa na vuguvugu la kutofahamu njia ambayo ningeifuata katika bahari hii ya usomi na utafiti. Kama msimamizi wangu hakuchoka kusoma kazi yangu kila nilipompelekea na kunishauri ipasavyo. Nampa hongera kwa namna alivyozipitia sehemu mbalimbali za kazi yangu kwa haraka na kwa umakini na kuniwezesha kuukamilisha utafiti wangu kwa muda mfupi. Mawaidha yake mema yalinitia ari na mshawasha wa kuwaza, kutafakari zaidi na kuandika kazi hii. Mola azidi kumpa hekima na neema.

Shukurani pia nazitoa kwa Bi Mary Ndung'u ambaye hakuchoka kuusoma utafiti wangu mara kwa mara. Uhakiki wake pamoja na maoni yake ndiyo yaliyoupatia utafiti huu sura iliyo nayo. Kwa mawasiliano na mawaidha yake namshukuru.

Wahadhiri wengine katika idara ya isimu na lugha katika Chuo Kikuu cha Nairobi, nawapa shukrani kwa kazi bora ya mwongozo mlionipa katika harakati yangu ya kusomea shahada ya uzamili katika chuo kikuu cha Nairobi. Mliniongoza na kunielekeza hatua kwa hatua katika safari hii ya usomi ambayo haikuwa rahisi. Hawa ni Dkt. Iribe Mwangi, Prof. John Habwe, Dkt. Mwenda Mbatiah, Dkt. Evans Mbuthia, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Omoga Zaja, Prof. Kinene wa Mutiso, Dkt Amir Swaleh na Bw. Basilio Mungania.

Sitasahau wakufunzi wenzangu ambao tulishirikiana katika safari hii ya usomi wa shahada ya uzamili ambao ni Jones, Omar, Grace, Leah, Racheal, Joyce, Chisia, Maina, Bore, Dickson, Benard, Kabibi, Janet, Ndege, Sabastian, Ruth,Dorine,Monicah,Gataka,Otwere na Jenifer. Shukrani za dhati ni kwa Bw. Jones Manoti kwa ushirikiano wake mwema katika kupitia kazi yangu na kunipa maoni yake katika harakati za kuandika utafiti huu. Nawatakia kila la heri maishani mwao.

Heko na shukrani nawatunukia mke wangu Christine Kerubo, mtoto wetu Stephen Obure bila kumsahau dadangu Asenath Bitengo kwa mchango wake wa kifedha katika shughuli za kufanikisha utafiti huu. Ndugu zangu Henry, Samuel, Eucabeth, Joyce, Simon na Bathsheba wote kwa jumla nawaombea heri na fanaka kwa mchango wenu katika kufanikisha dua langu katika masomo. Namshehenezea shukrani za dhati Bw. John Muigai Mwalimu Mkuu wa shule

ya Nyondia kwa usaidizi wake na kunihimiza kwake wakati wote nilipokuwa katika usomi. Walimu wote was shule ya Nyondia pia nawapa shukurani kwa mchango wenu katika kufanikisha hatua yangu katika kipindi cha usomi.Wanafunzi wangu na wasomi wa Kiswahili nawashauri kuwa tukienzi na kukitukuza Kiswahili.

Mwisho nawatolea shukurani Mama Tony na Bi Sally kwa kazi yenu ya kupiga chapa tasnifu hii.

## YALIYOMO:

**uk**

Mada ............................................................ i

Ungamo ............................................................ ii

Tabaruku ............................................................ iii

Shukrani ............................................................ iv

Yaliyomo ............................................................ vi

Ikisiri ............................................................ x

Orodha ya Vifupisho ............................................................ x

**SURA YA KWANZA**

**PENDEKEZO LA UTAFITI.**

1.0 Utangulizi ............................................................ 1

1.1 Tatizo la Utafiti ............................................................ 3

1.2 Madhumuni ya Utafiti ............................................................ 4

1.3 Nadharia Tete ............................................................ 4

1.4 Sababu ya Kuchagua Mada ............................................................ 5

1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti ............................................................ 6

1.6 Msingi wa Nadharia ............................................................ 6

1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ............................................................ 8

1.8 Njia za Utafiti ............................................................ 8

## SURA YA PILI

## DHULUMA DHIDI YA VIJANA WA KIKE NA ATHARI ZAKE KATIKA RIWAYA YA ROSA MISTIKA.


2.0 Utangulizi........................................................................................13

2.1 Kudharauliwa.....................................................................................14

2.2 Kupigwa............................................................................................15

2.3 Kuozwa kwa Lazima...........................................................................17

2.4 Kubakwa na Kupachikwa Mimba...........................................................18

2.5 Vitisho...............................................................................................20

2.6 Matusi...............................................................................................21

2.7 Kubaguliwa na Kunyimwa Uhuru............................................................23

2.8 Kuchuuzwa.........................................................................................28

2.9 Kukandamizwa Kimapenzi.....................................................................29

2.10 Kukanwa na Jamii...............................................................................32

2.11 Hitimisho...........................................................................................33

## SURA YA TATU

## DHULUMA DHIDI YA VIJANA WA KIKE NA ATHARI ZAKE KATIKA RIWAYA YA TUMAINI.


3.0 Utangulizi....................................................................................37

3.1 Kudharauliwa..............................................................................37

3.2 Kupigwa......................................................................................38

3.3 Tohara.........................................................................................39

3.4 Kuozwa kwa Lazima....................................................................44

3.5 Kubakwa na Kupachikwa Mimba.................................................48

3.6 Vitisho.........................................................................................49

3.7 Matusi .........................................................................................50

3.8 Kubaguliwa na Kunyimwa Uhuru ................................................51

3.9 Kukandamizwa Kimapenzi...........................................................54

3.10 Hitimisho....................................................................................56


## SURA YA NNE

## MITAZAMO YA WAANDISHI KUHUSU DHULUMA DHIDI YA VIJANA WA KIKE.


4.0 Utangulizi....................................................................................59

4.1 Mwandishi wa Kiume ...................................................................59

4.2 Mwandishi wa Kike .....................................................................61

4.3. Ulinganishi na Ulinganuzi wa Mitazamo ya Waandishi kati ya Rosa Mistika na Tumaini....64

4.3.1 Taswira Hasi....66

4.3.2 Taswira Chanya....67

4.4 Hitimisho....69

**SURA YA TANO**

**MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

5.0 Utangulizi....71

5.1 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti....72

5.2 Mapendekezo ya Utafiti....76

5.3 Tafiti za Baadaye....78

MAREJELEO....79

# IKISIRI

Utafiti huu unashughulikia swala la dhuluma dhidi ya vijana wa kike katika riwaya za E.Kezilahabi, *Rosa Mistika* (1971) na C. Momanyi, *Tumaini* (2006) .

Uchanganuzi huu umegawanywa katika sura tano. Sura ya kwanza inahusu utangulizi wa utafiti. Katika sura ya pili tunachunguza na kuchanganua aina za dhuluma dhidi ya vijana wa kike na athari zake katika riwaya ya *Rosa Mistika* (1971). Katika sura ya tatu tunachanganua dhuluma dhidi ya vijana wa kike na athari zake katika riwaya ya C. Momanyi, *Tumaini* (2006).

Sura ya nne inashughulikia vipengele vya mitazamo ya waandishi hawa wawili wa kiume na wa kike. Sura ya tano ni muhtasari na mapendekezo ya utafiti.

# ORODHA YA VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| Dkt. | - | Daktari |
| Bi. | - | Bibi |
| Ub. | - | Ubeti |
| Uk. | - | Ukurasa |
| K.v. | - | Kama vile |
| K.m. | - | Kwa mfano |
| M.w | - | Msisitizo wetu |
| TUKI | - | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |
| Prof. | - | Profesa |

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi

Katika utafiti huu tunadhamiria kuangazia swala la dhuluma dhidi ya vijana wa kike. Kulingana na maelezo ya UN kwenye nakala ya *Gender and Child Development* katika tovuti kijana wa kike ni mtu wa jinsia ya kike aliye kati ya miaka 0-18. Nayo Kamusi ya Kiswahili Sanifu ineleza kuwa kijana wa kike ni kijana mwanamke aliyebaleghe lakini bado hajaolewa au kuzaa.

Dhuluma katika utafiti huu ni dhana ambayo tumeitumia kuangazia tendo lisilo la haki, onevu, la kutesa ama la ukatili dhidi ya mtu. Kulingana na *Gender and Child Development* kwenye tovuti, inabainika kuwa, kwa sababu ya vile jamii zote zina dhuluma zenye misingi ya jinsia inayoanza katika viwango vya mwanzo katika maisha, usawa wa kijana wa kike ni muhimu katika kufikia maazimio pamoja na kumpa nafasi sawa ili awe mshirika katika hatua za kimaendeleo.

Dhuluma dhidi ya vijana wa kike imedhihirika kutoka enzi za kale. Kulingana na maandiko ya Biblia, kijana wa kike amedhulumiwa katika kipindi cha Ibrahimu. Katika Biblia, Kitabu cha Mwanzo 16:1-4, Hagar, msichana kijakazi na mtumwa amekumbana na dhuluma kandamizi na kufanya kazi kama mtumwa. Mwajiri wake Sarah anamrai Abrahamu azae naye. Katika kitabu cha Mwanzo 3: 1-3 Biblia inamsawiri Zilpha kama msichana mtumwa na kijakazi aliyetumikia Laban naye Bithem akamtumikia bintiye Racheal. Dhuluma kwa kijana wa kike inajidhirihirisha wakati Dinah mtoto wa Yakobo ananajisiwa na Schem mwana wa Chifu Hamor, katika katika kitabu cha Mwanzo 34:1-4. Hizi ni baadhi tu ya dhuluma chache kati ya dhuluma nyingi zilizoko katika Biblia. Zaidi ya hayo dhuluma dhidi ya vijana wa kike hujitokeza katika tenzi za kale, kama vile *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa*, Allen (1971)

Ub. *37 Mwanangu kujile watu*
*Waungwana wenye vitu*
*Kusudi wajile kwetu*
*Ili kutaka kukuoa*

*38 Mayasa akadhukuri*
*Mimi sitaki tajiri*
*Wala salubu amri*
*Siwatake wote pia*

Mfalme anamwona bintiye Mayasa kama kitegauchumi katika miliki yake, wakati ambapo ameamua kumnadi kwa yule atakayetoa mahari mengi na kuahidi kuwa ndiye angemuoa Mayasa.

Utanzu wa tamthilia pia umechangia katika kutoa maoni kuhusu dhuluma zinazowakumba vijana wa kike. Katika T. Ngugi, (2006:14-15), *Kesho Wakati kama Huu*, tunamwona Mumbi akilazimishwa kuozwa kwa Charles ambaye hamjui na wala hawajawahi kuonana naye, tukio ambalo linasababisha ajitie kitanzi kabla hata ya kuozwa. Katika tamthilia hiyo kwenye uk. 36, Njango anamkataza bintiye, Wanjiru kuolewa na Asinjo akidai kuwa ni mtu kutoka kabila jingine na kumnyima bintiye haki ya kujifanyia uamuzi wake.

Mila, itikadi na tamaduni zilizopitwa na wakati za Mwafrika zinachangia pakubwa katika kumdhalilisha na kumkandamiza kijana wa kike. Kwa kiasi zimempa picha ya kumdunisha katika jamii anamokulia. Mila na itikadi zimempa nafasi mwanamume na hata kijana mdogo wa kiume, kumkandamiza na kumdharau kijana wa kike. Momanyi, katika riwaya ya *Tumaini* (2006:46) ametuonyesha Shabani akimkariria Tumaini shairi lifuatalo;

*Nashikilia ukale ambapo hapana budi*

*na huacha vile vile iwapo haunifaidi*

*nitabadili milele siwezi kuwa abidi*

*wa kutenda yale yale.*

Katika riwaya za *Rosa Mistika* (1971), *Utengano* (1980), *Nguvu ya Sala* (1999) na *Tumaini* (2006) miongoni mwa riwaya zingine, waandishi wa tungo hizi za kifasihi wamechangia katika kuweka wazi swala hili la dhuluma dhidi ya vijana wa kike katika jamii tunamoishi.

Kuna mifumo na misingi ya ubabedume ambayo imetumika kuangazia jinsia ya kike kama viumbe dhaifu ambavyo haviwezi kujifanyia maamuzi kuhusu mahitaji yao muhimu. Hili ni tukio ambalo limechangia katika kuidhulumu na kuikandamiza jinsia ya kike kwa jumla.

Wafuasi wa Ufeministi katika vipindi hivi vya kisasa wametumia tungo za uandishi katika kutetea na kushambulia asasi kandamizi katika jamii. Asasi hizi zimekuza dhuluma au udhalilishaji wa jinsia ya kike. Wafuasi hawa wanatumia mbinu za uandishi wa riwaya, tamthilia, mashairi, novela na hadithi fupi katika kutetea haki za jinsia ya kike. Utafiti wetu

unajikita katika riwaya mbili ambazo ni *Rosa Mistika* (1971) na *Tumaini* (2006) za Kezilahabi na Momanyi mtawalia.

## 1.1 Tatizo la Utafiti

Kila uchao waandishi wa riwaya, tamthilia na tanzu zingine za fasihi wameangazia swala la dhuluma kwa vijana wa kike kwenye tungo zao. Kwa mfano, mwandishi Mohamed S.A katika riwaya za *Nyota ya Rehema* ( 1976), *Utengano* ( 1980), na *Tata za Asumini* (1990) ameangazia dhuluma dhidi ya vijana wa kike. Mwandishi Wamitila K.W katika riwaya ya *Nguvu ya Sala* (1999), ameangazia swala la dhuluma dhidi ya vijana wa kike. Vyombo vya habari navyo hutoa habari kuhusu jinsi kijana wa kike anavyoendelea kudhulumiwa kwa matendo kama vile, kuachishwa elimu, kupachikwa mimba, kuozwa mapema, kupashwa tohara miongoni mwa dhuluma zingine. Nakala ya *Daily Nation* 2/10/2012, imeangazia Bwana Clyde Asiema Mmbaha aliyehukumiwa kwa kumteka nyara kijana wa kike, mwanafunzi wake, Stacy Agatha Akinyi mnamo tarehe 8/7/2012.Tukio hili na kutekwa kwa kijana huyu wa kike ni dhihirisho kuwa vijana wa kike bado wangali wanadhulumiwa katikakipindi hiki cha miaka ya 2012. Kwa mujibu *Women, Health and Development* kwenye tovuti imesemekana kuwa kiwango cha kijana wa kike kuelimishwa ni cha chini zaid. Vijana wengi wa kike hawayafikii masomo ya viwango vya juu kwa sababu ya vikwazo vya jamii zao,wengi wao hukamilishia masomo yao hasa kwenye shule ya msingi. Imedhihirika kuwa mara nyingi wao hubaki nyumbani kutekeleza majukumu ya nyumbani, kulima pamoja na kazi zingine za ziada. Hili ni dhihirisho kuwa kijana wa kike bado hajakombolewa kutokana na dhuluma kandamizi.

Kutokana na hii hali kandamizi dhidi ya kijana wa kike, utafiti wetu umelenga kushughulikia swala la dhuluma dhidi ya wahusika vijana wa kike katika riwaya za *Rosa Mistika* (1971) na *Tumaini* (2006). Katika utafiti huu tumeangazia dhuluma katika misingi ya maonevu ya kimwili, kijinsia, kihisia na matumizi ya lugha ya kumdhalilisha kijana wa kike.

Watafiti wengi wamejikita katika kuangalia maswala ya dhuluma dhidi ya jinsia ya kike kwa ujumla lakini sisi tumejishughulisha na dhuluma zinazowakumba vijana wa kike katika muktadha halisi pamoja na vipengele vya dhuluma mahsusi. Tumetumia wahusika wawili wakuu ambao ni Rosa katika *Rosa Mistika*, (1971) na Tumaini katika *Tumaini*, (2006) miongoni mwa vijana wa kike wengine katika riwaya hizi mbili.

## 1.2 Madhumuni ya Utafiti

Utafiti wetu una malengo yafuatayo:

i) Kuchunguza na kubainisha namna dhuluma dhidi ya vijana wa kike inavyojitokeza katika riwaya mbili za Kiswahili; Euphrase Kezilahabi, katika *Rosa Mistika* (1971) na Clara Momanyi, katika *Tumaini* (2006).

ii) Kubainisha athari zinazojitokeza kutokana na dhuluma dhidi ya wahusika vijana wa kike katika jamii.

iii) Kulinganisha na kulinganua mitazamo ya waandishi wa kike na kiume kuhusu jinsi wanavyomsawiri kijana wa kike katika riwaya zao, *Rosa Mistika* (1971) na *Tumaini* (2006).

iv) Kupambanua taswira za waandishi wa kike na kiume kuhusu kijana wa kike katika riwaya za *Rosa Mistika* (1971) na *Tumaini* (2006).

v) Kuchunguza juhudi zinazofanywa na vijana wa kike katika kujikomboa dhidi ya dhuluma zinazowakumba katika jamii zao.

## 1.3 Nadharia Tete

Uhakiki wetu utaongozwa na nadharia tete zifuatazo:

i) Dhuluma zinazomkumba kijana wa kike zina chanzo chake kwenye misingi ya ubabedume inayoongozwa na mifumo ya itikadi na mila.

ii) Dhuluma dhidi ya kijana wa kike zinasababisha athari hasi katika maisha ya kijana wa kike katika jamii.

iii) Waandishi wa kiume na wa kike hutofautiana na kukubaliana katika jinsi wanavyoshughulikia swala la dhuluma dhidi ya vijana wa kike katika tungo zao.

(iv) Utetezi wa imani na msimamo wa kijana wa kike umefaulu licha ya vitisho katika juhudi za kujikomboa kutokana na dhuluma zinazomkumba.

## 1.4 Sababu ya Kuchagua Mada

Swala la dhuluma dhidi ya vijana wa kike limekumbwa na changamoto nyingi kutokana na mabadiliko mengi ya kihistoria na ya kijamii. Mabadiliko haya yanapaswa kuangaliwa mara

kwa mara kulingana na vile mitazamo ya uhakiki inavyotofautiana kuhusu jinsi wanavyolihakiki swala lenyewe.

Mukobwa, M.J. (1985) katika utafiti wake kuhusu maendeleo ya kimaudhui katika tamthilia tano za Ebrahim Hussein, anamnukuu Hough (1986) kwa kusema;

*" Hakuna kazi yoyote ya uhakiki wa fasihi iliyokamilika. Uhakiki haushughulikiwi wakati mmoja na kuisha kabisa kwani hutegemea historia na mazingira ya kijamii katika kila kipindi kipya cha historia. Fasihi ya wakati uliopita yafaa kufasiriwa upya, jinsi tunavyofasiri maandishi mapya ndivyo hali zetu za yale ya zamani zinavyobadilika."*

Udhalimu dhidi ya vijana wa kike katika riwaya hizi za *Rosa Mistuka* (1971) na *Tumaini* (2006). Hii ni mada tumeteua ili tuweze kuchunguza dhuluma inayowakumba vijana wa kike na taswira waandishi wanayowapa vijana wa kike ili kuwapa ujasiri na sauti ya nguvu ya kupambana na mfumo wa ubabedume. Riwaya hizi za Kiswahili ni za Euphrase Kezilahabi, katika *Rosa Mistika* (1971) na Clara Momanyi, katika *Tumaini* (2006).

Watafiti wa awali wameshughulikia masuala ya wanawake kwa kijumla katika tenzi, tamthilia na hata riwaya ilhali sisi tunataka kujikita katika kipengele mahususi cha vijana wa kike katika riwaya mahususi tulizoziteua za *Rosa Mistika* na *Tumaini*. Kwa kutumia riwaya hizi tumedhamiria kuwafikia vijana wa kike katika ulimwengu huu wa tatu ili kuwahamasisha katika kuleta mabadiliko yanayowahusu.

Sababu nyingine ya kuteua mada hii ni kudhihirisha ari tuliyonayo katika kutoa mchango wetu kama wahakiki ili kuongezea mchango wa uchambuzi wa wasomi na wahakiki wa awali waliotangulia katika kuleta mtazamo mpya katika jamii kuhusu vijana wa kike. Kama wahakiki na watafiti pia tuliteua mada hii ili iweze kuwa mojawapo ya mbinu za kutoa maoni na mchango wetu katika kuifikishia jamii ujumbe kuhusu swala la dhuluma dhidi ya wahusika vijana wa kike. Lengo letu ni kuelimisha na kisha kuleta mabadilikiko katika jamii kwenye harakati za kumkomboa kijana wa kike kutokana na dhuluma kandamizi.

## 1.5 Upeo na Mipaka

Utafiti huu unajishughulisha na uchunguzi wa swala la kimsingi linalohusu dhuluma dhidi ya vijana wa kike katika jamii. Tuchunguza riwaya mbili teule za *Rosa Mistika* (1971) na *Tumaini* (2006), katika kuchanganua mada hii utafiti wenyewe una malengo makuu katika kueleza na kuchanganua dhuluma zinazowakumba vijana wa kike katika hali yao ya kimwili, kihisia, lugha mbovu wanayokumbana nayo na inayosheheni matusi na kejeli.

Katika uchunguzi wetu tumeshughulikia riwaya mbili tu ambazo ni; *Rosa Mistika* ( 1971) na *Tumaini* ( 2006). Tumeangazia dhuluma na maonevu yanayomkumba kijana wa kike kwa mtazamo wa kumnyima haki zake, kumpasha tohara ya lazima, kumuoza kwa lazima pamoja na kumkatizia ari yake masomoni. mtendea u Riwaya hizi zilizotungwa katika vipindi tofauti yaani kati ya miaka 1971 na 2006, zinatuongoza katika utafiti ili kuangazia swala la dhuluma dhidi ya vijana wa kike katika vipindi hivi tofauti.

## 1.6 Msingi wa Kinadharia

Utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Ufeministi. Katika uchunguzi wa dhuluma dhidi ya kijana wa kike katika riwaya za *Rosa Mistika* na *Tumaini*. Nadharia hii inaafikiana na yale tunayoyashughulikia katika mada yetu.

Dhana ya Nadharia ya Ufeminsti imewahi kutolewa fafanuzi nyingi na wataalamu wengi kama vile W.K Wamitila, Njogu na Chimera,Wafula na Njogu. Kila mtaalamu katika ufafanuzi wake ana mtazamo wake. Licha ya tofauti zao za kimtazamo, kuna baadhi ya maelewano na maafikiano kati yao.

Nadharia ya Ufeministi ina historia ndefu. Katika karne ya kumi na nane, Ufeministi ulitumiwa kumaanisha sifa za kike. Mnamo mwaka wa 1892, kongamano la wanawake lilifanyika mjini Paris. Neno la kifaransa *Feministe* lilitumika kuelezea mtazamo na itikadi za kupigania haki za wanawake kwa imani kwamba jinsia zote ni sawa. Harakati hizi zilipata mashiko zaidi Marekani na Ulaya mnamo karne ya kumi na tisa na ishirini.

Nadharia hii ina misingi yake katika kazi ya Mary Wollstonecraft (1792) iitwayo A *Vindication of the Rights of Women*, ambapo anapendekeza kuundwa kwa jamii mpya yenye usawa kati ya mwanamke na mwanamume. Wollstonecraft alikuwa mmoja wa waandishi wa awali waliochangia katika tetezi kali dhidi ya haki za jinsia ya kike. Katika kazi zake nyingi za tetezi.

Kazi hizi za awali ziliongozwa na Nadharia hii katika uandishi wao, nazo ni kama vile *A Room of One's Own* (1929) ya Virginia woolf na *The Second Sex* (1949) ya Simon de Beavoire.

Kulingana na Wollstonecraft elimu ni kitu cha kimsingi katika harakati za ukombozi wa wanawake. Ni kwa misingi hii tunadhamiria kuitumia Nadharia ya Ufeministi ili kuhakiki dhuluma zinazomkumba mhusika wa kike katika elimu yake. Wolf (1949) anatilia mkazo kwa kuongezea kwamba ni muhimu kwa mwanamke kuwa huru kiuchumi. Kulingana na Wolf, mwanamke akipata elimu na pesa atajitegemea na kufanikiwa katika taaluma ya uandishi.

Nadharia ya Ufeministi inahusu asasi zote katika jamii ambazo zinachangia kumdhulumu mwanamke. Wafuasi wa Nadharia hii wanapendekeza usawa uwepo baina ya mwanamke na mwanamume bila kutilia maanani tofauti zao za kimaumbile.

Nadharia ya Ufeministi iliasisiwa kutokana na kuzuka kwa tapo la Ufeministi huko Ulaya. Wafuasi wa Nadharia hii kama anavyosema Mbatiah (2001), wanachukua mwelekeo wa kiharakati na kushambulia baadhi ya asasi zinazochangia katika kumdhulumu na kumdhalilisha mwanamke.

Njogu na Chimera (1999:19) wanasema kuwa Nadharia ya Ufeministi imeweka msingi na msukumo mkubwa pamoja na nia ya kupigania ukombozi wa mwanamke. Asasi mbalimbali za kijamii kama vile dini, siasa na uchumi zimemkandamiza mwanamke kwa muda mrefu.

Kulingana na kamusi ya TUKI (1986), Ufeministi ni Nadharia ya usawa wa wanawake. Nadharia hii inadhamiria kupigania ukombozi, haki na usawa kati ya wanawake na wanaume.Nadharia ya Ufeministi inapinga mifumo ya kiume inayowapendelea wanaume kwa kuwatwaza huku ikiwatweza wanawake. Hivyo basi, Nadharia hii tumeitumia katika kuhakiki jinsi kijana wa kike anavyodhulumiwa na mikakati yake katika kujikomboa kutokana na dhuluma kandamizi.

Wamitila K.W (2003:253) anaelezea dhana ya Ufeministi kama istilahi inayotumiwa kuelezea mojawapo ya misingi na misukumo mikubwa pamoja na nia ya kupigania ukombozi wa mwanamke kutokana na pingu za kitamaduni, kidini, kijamii, siasa, kiuchumi na kiusawiri. Nadharia hii inaelezea Ufeministi kama istilahi inayorejelea harakati za ukombozi wa mwanamke.

Wengine waliochangia katika uvumbuzi wa Nadharia hii wanadai kwamba tamaduni nyingi katika jamii humpendelea mwanamume na kumdhulumu mwanamke kama kiumbe duni.

Ndiposa wanapendekeza wanawake wajitoe muhari katika kutetea na kupigania uhuru na ukombozi wao.

Wafula na Njogu (2007 :90) wanasema kuwa Ufeministi ni dhana inayojumuisha mikabala tofauti yenye misukumo ya kupigania ukombozi wa mwanamke kutokana na pingu za kiutamaduni, kidini, kijamii, kisiasa na kiuchumi. Pingu hizi zimejengeka kwenye misimamo na itikadi ya kiume. Birke (1986) na Lovenduski na Randall (1993) wakinukuliwa na Wafula na Njogu, wanasema kuwa, Ufeministi ni dhana inayoelezea hali na tendo la wanawake wanaodai kujielezea katika jamii mbalimbali na wanaume wanaounga mkono jitihada za wanawake hao. Ni dhana inayopinga mfumo wa kiubabedume.

Tawi la Nadharia ya Ufeministi linaloongoza utafiti wetu ni lile linalofahamika kama Ufeministi huru. Miongoni mwa matawi mengine, tawi hili linafahamika zaidi katika utetezi wa kuwakomboa wanawake na kuwaweka huru. Ufeministi huru hujishughulisaha na kupigania haki na mabadiliko ya kijumla katika jamii na kupigania kumalizika kwa ubaguzi na kandamizi dhidi ya jinsia ya kike. Tawi hili linabainisha kuwa wanadamu wameumbwa kuwa viumbe sawa, waume kwa wake. Wote wanapaswa kuwa huru kutekeleza majukumu sawa bila kuwepo na mipaka.

Kati ya mwanamke na mwanamume, waumini na wafuasi wa tawi hili wanapendekeza kutekelezwa kwa mabadiliko kupitia kwa mikakati kama vile ushawishi, mwamko wa kitabaka na kujumuisha maswala yanayohusu wanawake na maisha yao.

Tawi la Ufeministi huru linakubali kuwa mwanamke na mwanamume lazima washirikiane katika nyanja mbalimbali maishani. Kinachohitajika ni kubadilishwa kwa mtazamo wa jamii ili wanawake waweze kutambuliwa kama binadamu sawa na wanaume ili wasidhulumiwe kamwe. Ni kwa misingi hii ambapo tunahisi kuwa Nadharia hii ni faafu zaidi kutumika katika kuchanganulia mada yetu ya utafiti.

## 1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Sehemu hii inashughulikia baadhi ya kazi zilizoandikwa hapo awali na ambazo zina uhusiano na mada ya utafiti . Tumeweza kubaini jinsi kazi hizo zinavyotofautiana na utafiti wetu huku tukionyesha pia michango yake kwa malengo ya kujenga na kukuza utafiti huu. Uhakiki wa kazi

za awali zimetufaidi kutoa mwongozo wa kuchanganua na kubainisha swala letu la utafiti ili kufikia azima yetu ya utafiti.

Waandishi wa kazi za awali walikuwa na mitazamo ya kijumla katika kuangazia swala la dhuluma kwa mtazamo mpana. Wameshughulikia wanawake kwa jumla bila kuweka mipaka kati ya mwanamke mchanga na mwanamke mtu mzima. Tafiti hizi zinatufaa kutokana na misingi yake ya kidhuluma.

Ndungo (1995) katika tasnifu yake ya MA alishughulikia swala la nafasi ya mwanamke katika jamii. Alishughulikia swala hili kwa kujumuisha usawiri wa mwanamke katika mazingira ya kihistoria, kijamii, kielimu, kiuchumi, kisiasa na kitamaduni katika ndoa. Asasi hizi kuu alizoangazia zitakuwa nguzo katika kuchunguza mada ya utafiti wetu.

Momanyi (1998) alishughulikia swala la usawiri wa mwanamke katika jamii ya Waswahili kama inavyobainika katika ushairi wa Kiswahili. Mtafiti huyu aliangazia jamii, elimu, siasa na tamaduni. Alitumia msimamo huu kumtambua mwanamke na baadaye akautumia ufanisi huo wa nafasi ya mwanamke kama msingi kudai nafasi katika harakati za kijamii na asasi zilizotawala jamii ya Kiislamu. Kazi hii ya Momanyi ni muhimu katika utafiti wetu kwani hutufafanulia masaibu yanayowakumba wanawake katika jamii, tukio ambalo ni la kimsingi katika utafiti wetu kuhusu dhuluma ya kijana wa kike.

Kruger (1998) alitafiti kuhusu usawiri wa wanawake kulingana na waandishi wa Kiafrika walioandika riwaya na hadithi fupi. Alisema kwamba waandishi hawa hawatumii wahusika wanawake kama wahusika wakuu bali huwatumia kama wahusika wajenzi. Kazi hii imetusaidia kuelewa upungufu uliopo katika usawiri wa vijana wa kike kama wahusika wakuu.

Lugano (1989) alitafitia swala la usawiri wa mwanamke kisiasa, kiuchumi na kijamii katika riwaya za Kezilahabi. Alionyesha jinsi mwanamke alivyosawiriwa kama mtegemezi wa mwanamume, chombo cha mwanamume na chanzo cha maovu yote katika jamii. Kazi hii ilijitokeza na itikadi ya Kezilahabi kuhusu mwanamke katika ujumla wake.Utafiti wetu ni wa kiulinganifu tofauti na utafiti wa Lugano .Hata hivyo, utafiti huu utatufaidi katika kuangazia taswira anayopewa mwanamke katika riwaya. Aidha, Nadharia aliyoitumia inahusiana na yetu, hivyo, itatuwezesha kuelewa maswala ya nadharia hiyo zaidi.

Katola (2006) ametafiti kuhusu udhalimu wa wahusika wanawake katika tamthilia za Kiswahili. Alishughulikia tamthilia za Ali Katini Mwachofi, *Mama ee* (1987), Penina Muhando, *Hatia* (1972), A. S Yahya na David Mulwa, *Buriani* (1983) na Said Ahmed Mohamed, *Kitumbua Kimeingia Mchanga* (2000). Alishughulikia swala la udhalimu wa wanawake kwa jumla huku akirejelea katika waandishi wa kiume na wale wa kike kwenye tungo za tamthilia.Utafiti wetu umejibana katika riwaya na kuangazia dhuluma dhidi ya vijana wa kike.Hivyo basi, utafiti huu umetufaa kwa kutupa mwangaza kuhusu yale tunayoyatafitia.

Mutua (2007) alitafiti mitazamo ya vijana na wazee kuhusu ukombozi wa wanawake katika tamthilia tatu za Kiswahili. Kwenye utafiti wake anabainisha kuwa vijana na wazee kwa jumla wanaunga mkono na vilevile kupinga ukombozi wa wanawake. Kazi yake ni muhimu katika kuangazia swala la ukombozi wa vijana wa kike.

Nyaosi (2008) ameshughulikia taswira ya dhuluma zilizoko katika asasi ya ndoa katika riwaya za *Kiu* na *Msimu wa Vipepeo*. Katika utafiti wake ameshughulikia namna ndoa inavyotumiwa kumdhulumu na kumkandamiza mwanamke. Ndoa ni asasi moja tu ya kijamii. Utafiti wetu umeziangazia asasi zingine zaidi, ndoa ikiwa mojawapo ya asasi zinazotumika kumdhulumu kijana wa kike.

Masibo, B. (2009) katika *Gendered Perceptives in the Novels of Ngugi Wa Thiongo and Alice Walker,* analinganisha fasihi iliyoandikwa na Mwafrika wa kiume Ngugi Wa Thiongo na Mmarekani mweusi wa kike kuhusu taswira ya mwanamke na mwanamume. Kazi ya Masibo inachanganua na kulinganisha taswira chanya na hasi zilizopewa mwanamke. Kazi hii imetufaa katika utafiti wetu kwani tumeangazia waandishi wawili, wa kiume na wa kike. Waidha, kazi yetu imenufaika na utafiti wake kwa sababu tumeangazia maswala ya Afrika ambayo yalishughulikiwa katika utafiti wake kwa kiasi fulani.

Mirikau (2011) katika tasnifu yake ya ameangazia swala la *Taswira ya Mwanamke katika Tamthilia tatu za Kiswahili: Wingu la Kupita (1999), Pango (2003) na Seserumbe (2009)* za K.W Wamitila. Amezungumzia usawiri chanya na hasi wa mwanamke. Usawiri huu wa mwanamke umetuwezesha kuangazia changamoto na dhuluma zinazomkabili kijana wa kike katika jamii na mikakati yake katika kujikomboa kutokana na dhuluma anazokumbana nazo. Mirikau ametumia Tamthilia tatu lakini sisi tumeangazia riwaya mbili tu.

Ukinzano mwingine baina ya kazi za awali na yetu ni kuwa watafiti wengi wamelitafitia swala la dhuluma dhidi ya wanawake kwa jumla kama vile (Katola (2006), Nyaosi (2008), Lugano (1999), Mutua (2008) na wengine. Kazi yetu imekuwa tofauti na hizi za awali kwa sababu imelenga swala la dhuluma dhidi ya vijana kike. Katika kazi tangulizi watafiti wameangalia wahusika wanawake kwa ujumla katika tafiti zao ilhali sisi tumejikita katika wahusika wakuu ambao ni vijana wa kike pekee.

Watafiti wote wameangazia ukombozi wa mwanamke kwa kijumla. Kwa hivyo ingawa lengo ni moja kuna njia nyingi ambazo hazikuambatana na mada yetu kulingana na mtazamo wetu wa kuangazia kijana wa kike ambapo si kuangazia wanawake kijumla. Matatizo yanayomsibu kijana wa kike katika asasi ya elimu ni tofauti na yale yanayomkumba mwanamke kwenye ndoa . Hata hivyo, kazi hizi tangulizi zimetufaa katika mitazamo yao katika kuangazia suala letu la jinsia ya kike.

Isitoshe utafiti wetu ni wa kiulinganishi kwenye kipengele cha wakati na vile vile waandishi kwa kuzingatia jinsia zao. Pia swala la Nadharia zilizotumika katika kuzihakiki kazi za awali zimetupatia nafasi ya kutafiti mada hii. Hata hivyo ifahamike kuwa kazi yetu imefaidika kutokana na kazi za awali kwenye mahusiko ya njia za uhakiki, njia za utafiti na hata mapendekezo kuhusu yafaayo kufanywa zaidi kuhusiana na mada kuu ya nafasi ya mwanamke dhidi ya ile ya mwanamume katika jamii.

Utafiti huu unatofautiana na maswala ya mada zilizotafitiwa awali na hata Nadharia za Ufeministi zilizotumika.Muingiliano unajitokeza katika maswala ya dhuluma na kwa upande mwingine kuna kuhitilafiana katika kazi yetu na zile tangulizi. Kwa mfano, utafiti wetu unatumia nadharia ya Ufeministi huru na utafiti kama ule wa Katola (2006) ulitumia Ufeministi wa Kiafrika.

## 1.8 Njia za Utafiti

Katika utafiti huu, kimsngi tumetumia njia za kusoma na kuhakiki vitabu mbalimbali. Tumesoma na kuzihakiki riwaya mbili za Kiswahili ambazo ni Rosa Mistika na Tumaini.

Pia tumerejelea vitabu mbalimbali kwa mnajili ya kufafanua hoja zetu, vilevile tumetumia kamusi mbalimbali na makala tofautitofauti yalisoshughulikia maswala ya dhumuna. Aidha

tumekuwa na mazungumzo ya ana kwa ana na waadhiri hasa wasimamizi wa utafiti huu. Tumetumia muda wetu pia katika kusoma kwenya mtandao wa hasa pale tulipohitaji ufafanuzi wa mwelekeo wa karibuni, kuhusu maswala ya dhulama dhidi ya vijana wa kike.

Kwenye mtandao tumesoma maswala yanayohusu eneo la Nadharia ya Ufeministi kwa hivyo utafiti wetu mwingi umekuwa wa maktabani. Vilevle tuliziangazia kwa makini baadhi ya kazi za awali zilizohusu Nadharia hii ya Ufeministi huru katika kuhakiki swala la dhuuma. Tulisoma makala na maandishi ya wasomi yanayohusu Nadharia tuliyoitumia.

Katika kazi hii tuliwashirikisha kimawazo wahadhiri na baadhi ya wanafunzi wenye ujuzi katika taaluma hii kwa kuwahoji. Baada ya kukusanya data za kutosha tulizigawa kulingana na madhumuni ya utafiti wetu. Data hizi tumezichanganua kulingana na msingi wa nadharia na kutoa taswira ya dhuluma kwa wahusika wa kike.

Tumesoma riwaya ya Euphrase Kezilehabi, *Rosa Mistika* (1971) na Clara Momanyi, *Tumaini* (2006). Riwaya hizi zimetufaa zaidi katika kujenga na kukuza suala la utafiti kwani mada ya utafiti huu imejikita katika tungo zilizoko katika riwaya hizi mbili.

# SURA YA PILI

# DHULUMA DHIDI YA VIJANA WA KIKE NA ATHARI ZAKE KATIKA RIWAYA YA ROSA MISTIKA

## 2.0 Utangulizi

Fasihi ina majukumu muhimu ya kujenga, kuelimisha na kufasiri matendo katika jamii. Msanii huangazia na kufasiri asasi kuu za jamii kama vile desturi, utamaduini, mila, dini, siasa na uchumi. Msanii huwa ni mwanajamii na ndiyo sababu katika utunzi wake yeye huangazia maswala yake katika jamii. Fasihi hukiuka jukumu la kioo cha jamii kwa kumulika na kuonyesha sura ya jamii na kutoa taswira ya jamii ambayo si tuli bali inayoshughulika katika kutekeleza majukumu tofauti tofauti. Matukio yanayoshughulikiwa na fasihi ni yale tunayoyasoma katika fasihi na tunayalinganisha na hali halisi katika jamii. Baadhi ya matukio yanayoibuka na kushughulikiwa katika taaluma ya fasihi ya Kiswahili ni dhuluma dhidi ya vijana wa kike, tukio ambalo tumelitafiti katika jamii ya Rosa Mistika katika riwaya ya *Rosa Mistika* (1971).

Suala hili la dhuluma dhidi ya kijana wa kike na wahusika wa kike kwa jumla lina kina kirefu kihistoria. Tukio hili limezua mwamko mpya na mtazamo mpya hasa katika karne hii ya ishirini na moja. Kutokana na kuibuliwa kwa Nadharia ya Ufeministi, uhakiki wa kifasihi kuhusu jinsia ya kike umepata wafuasi wengi wanaotaka kutoa michango yao ili kushambulia asasi kandamizi kama vile ndoa, tamaduni, elimu, na dini ambazo zimechangia kumdhulumu kijana wa kike.

Imebainika kwamba utamaduni anamokulia na kuishi kijana wa kike umechangia zaidi katika kumdhalilisha na kumkandamiza ilhali yule mwenzake wa kiume akitukuzwa na kuenziwa. Katika sura hii tutaangazia dhuluma zinazomkabili kijana wa kike na athari zake katika riwaya ya *Rosa Mistika.* Dhuluma hizi ni pamoja na; kupigwa, kejeli, matusi, ndoa za mapema, kudharauliwa, kunyimwa haki na kukataliwa na jamii, kunajisiwa, kunyanyaswa masomoni, kupachikwa mimba na kunyanyaswa kimapenzi miongoni mwa dhuluma nyingine. Tumezijadili aina hizi za dhuluma na athari zake kwa kijana wa kike tukirejelea riwaya tuliyoiteua ya *Rosa Mistika* (1971).

## 2.1 Kudharauliwa

Katika utafiti wetu dhana ya 'kudharauliwa' imetumika kulenga hali ya kumdunisha na kumtweza kijana wa kike. Hali hii ya kumdunisha kijana wa kike inajitokeza katika hali ya kumwaibisha, kumvunjia staha na kutomthamini kijana wa kike. Hali ya kudharauliwa inajidhihirisha wakati kijana wa kike anapovunjiwa heshima na kukosa thamani mbele ya mhusika mwenziwe kijana wa kiume. Dharau kwa kijana wa kike imechangia kujiona kuwa duni kutokana na maonevu ya vitendo na lugha inayotumika dhidi yake. Wakati mwingi kijana wa kike huchukuliwa kama kiumbe dhaifu kimawazo, asiyefaa kutoa uamuzi na hata ushauri katika jamii inayotawaliwa na ubabedume.

Katika matukio ya udhalimu yanayomkabili kijana wa kike, Rosa katika riwaya ya *Rosa Mistika* iliyoandikwa na Euphrase kezilahabi, (1971) dharau huonenekana mwandishi anaposema kuwa;

> *Regina, alikuwa na watoto watano wasichana, wote wazuri kama yeye lakini bwanake Zakaria hakuwaona kama watoto bali alikuwa akihitaji mkewe amzalie kijana wa kiume.*

Hali hii ya kuhitaji kijana wa kiume inadhihirisha jinsi vijana wa kike wanavyodharauliwa katika jamii ya Rosa.

Lugha waliyotumia vijana wa kiume waliozuru makao ya mzee Zakaria ilikuwa ya kumdunisha kijana wa kike.Vijana hao wa kiume wanapoulizwa walichokuwa wanataka, walijibu "Mzee sisi tunataka mayai ya kununua". Hali ya kulinganisha kijana wa kike na 'mayai' ni ya kudharau. Naye Zakaria baada ya kuwacharaza vijana hao alimgeukia bibiye na kumtolea matusi na kusema;

> "*Mshenzi unanizalia <u>wasichana tu!</u>*
> *Unaniletea taabu nyumbani bure tu!*"(Uk 23) (msisitizo wetu)

Maneno haya yanadhihirisha kuwadharau wasichana kwa kuonyesha kuwa hawana thamani kabisa wanapozaliwa. Mzee Zakaria anatilia ınkazo kauli hii tena anaposema "kuzaa wasichana taabu sana! (uk 38). Zakaria anawaona wanawe wa kike kama chanzo cha matatizo katika nyumba yake.

Katika *Rosa Mistika* swala la dharau kwa vijana wa kike linasawirika pale ambapo vijana wa kiume wanapotumia lugha ya kudunisha na kudharau mji wa Zakaria kwa kuwa na vijana wa kike watano ambao vijana hawa wa kiume waliwaona kuwa wengi mno na kuupa mji wa

Zakaria jina 'zoo'. Tukio hili linadhihirisha kuwa wasichana hawakuwa na thamani katika jamii ya *Rosa Mistika.*

Katika *Rosa Mistika* (1971; 29), vijana wawili katika kituo cha basi wanamkejeli Rosa alipoyasikiliza mazungumzo yao. Mazungumzo yao yanadhihirisha dharau kwa kijana wa kike pale anapokataa matakwa ya kijana mwenzake wa kiume. Rosa anaonewa, kudharauliwa na kukejeliwa kwa jambo ambalo halifai. Haya yanajitokeza pale vijana wanaposema;

> *"Nasikia kwamba msichana huyo hapendi kuzumgumza na wavulana!"*
> *"Sijui anajifikiria yeye ni nani?"*
> *"John alikuwa anasema kwamba msichana huyo ni kilema?"*
> *"Kweli bwana inawezekana. Hakuna uzuri usio na dosari"*
> *"Kweli bwana inawezekana. Wewe unafikiri msichana anaweza kufika darasa la kumi na moja bila..."(uk 29).*

Kijana wa kike anakosa kuthaminiwa na hata anadharauliwa na kijana mwenzake wa kiume. Tukio hili linazua matatizo na changamoto katika maisha ya kijana wa kike.

> *"Rosa alichukiwa sana. Alipojaribu kukaa na kuongea na wenziwe walimkimbia na kumwacha peke yake. Rosa alikonda. Alimaliza darasa la tisa kwa shida sana ingawa aliweza kuwa wa nne katika mtihani wa kumaliza mwaka*" (uk 29).

Jambo linalowakilishwa hapa ni kwamba vijana wa kike wanakumbana na dhuluma kutoka kwa jinsia yao pia.

Mzee mmoja katika *Rosa Mistika* (1971:20) anaonekana akimdhalilisha bintiye. Yeye ni kama jamii nyingi za Kiafrika ambazo hazimchukulii kijana wa kike kama kiumbe sawa na wa kiume. Dhuluma za kudharauliwa zinasababishwa na mfumo wa kuumeni au ubabedume. Mfumo huu wa kijamii unamtweza kijana wa kike na kumtwaza mwenzake wa kiume. Haya yanajidhihirisha pale Zakaria anaposema;

''*...atakayemnunulia madebe mawili ya pombe atampatia binti yake aoe.'' (uk* 20)

## 2.2 Kupigwa

Kupigwa ni kitendo cha kucharaza kwa mfululizo kwa kutumia kifaa fulani. Tamaduni nyingi za Kiafrika zilithamini kutia nidhamu watoto na wanawake. Kulikuwa na adhabu maalum kwa makosa maalum. Aliyetenda kinyume na matakwa fulani au aliyekosa kuwa na mwenendo uliostahili katika jamii husika, aliadhibiwa.

Katika *Rosa Mistika,* (1971:6), tunampata Rosa akipigwa na babake, Bwana Zakaria baada ya kuarifiwa na Stella kuwa alipokea barua na pesa kutoka kwa Charles. Babake anamcharaza mbele ya dada zake na mamaye. Licha ya Regina mamake Rosa na dada zake kulia, Zakaria hakukoma kumpiga. Mwandishi anaelezea kuwa; 'kab*la hajasema lolote alipigwa na kuanguka chini. Rosa alipigwa tena na tena, makofi yalikwenda mfululizo hata damu ikamtoka puani na mdomoni'. (uk 6).*

Kutokana na vitisho na dhuluma kandamizi ya kupigwa, kijana wa kike huathirika na kuingiwa na woga katika maisha na shughuli zao katika jamii. Tukio hili humuogofya kijana wa kike na kutishia ujasiri wake wa kukabiliana na baba zao, kaka zao na hata vijana wenzao wa kiume. Katika riwaya ya *Rosa Mistika* (1971) vijana wa kike wa Mzee Zakaria wanajikuta kila mara wakikimbilia vitandani mwao na hata kushauriwa na mama yao kutorokea mahali pa malazi pindi tu sauti ya Mzee Zakaria inaposikika. Wakati mwingine walilazimika hata kulala mapema kabla ya wakati kuwadia. Vitisho vyake Zakaria vinadhihirika wakati Regina anaposema kuwa; aliposikia sauti, "Hoi! Hoi! Hoi!" alifahamu huyo mtu alikuwa nani na alikuwa katika hali gani: Mara moja aliwahimiza wasichana wake wale upesi wakalale. (uk 40)

> *"Sauti sasa ilifika karibu na mlango wa nyumba. Watoto walijikunja kitandani, kimya! (uk 4)*

Hali hii ya vijana wa kike kujikunja na kukaa kimya punde tu wanaposikia sauti inadhihirisha hali ya woga waliotiwa na baba yao kutokana na kupigwa mara kwa mara.

Katika riwaya ya *Rosa Mistika*, Rosa anadhihirisha kuteswa kwake kupitia kipigo alichokipata kutoka kwa babake Zakaria. Katika ukurasa wa 6, anapigwa na hata baada ya kuchuruzikwa na damu, Zakaria hakomi kumpiga. Haya yanatokea kuwa;

> *"Rosa alipigwa tena na tena, makofi yalikwenda mfululizo hata damu ikatoka puani na mdomoni. Alilia, "Baba nihurumie, sitarudia tena, nimekoma." Rosa alinyang'anywa shuka. Chupi ilimwokoa lakini matiti yalikuwa nje" .(uk 6)*

Kipigo hiki kilimwathiri na kumuumiza Rosa kiasi cha kuchemshiwa maji ya kukandia usoni na mengine kuyanywa ili kuondoa damu mdomoni na puani. Fauka ya Zakaria kumcharaza Rosa, alizidi kumkaba kooni mpaka macho ya Rosa yakawa mekundu na hata ulimi kumtoka kulingana na ukurasa wa 7. Hali hii inasababisha mateso kwa vijana wa kike.

Hatuoni Jamii ikimlaumu mwanamume kwa sababu ya taasubi ya kiume inayojitokeza kutokana na mfumo wa ubabedume wa kumkandamiza kijana wa kike na hata kumnyima uhuru wa kunena. Rosa na dadake wanapotiwa kwenye gunia la upupu na kupigwa, mama yao huishia kutazama tu na kusimama mbali. Hata inasemeka kuwa hakuwa anadhubutu kusema lolote, ukurasa wa 28. Hali hii inadhihirisha mateso na hali ya kumwathiri kijana wa kike kimwili.

Asili ya Rosa kumvunjia Mzee Zakaria heshima katika *Rosa Mistika* (1971) inatokana na ukatili wa babake na dhuluma zake dhidi yake. Kwa mujibu wa Rosa inadhihirika wazi kwamba chanzo chake kumvunjia babake heshima ni mateso aliyoyapata kutoka kwa baba yake. Inadhihirika kuwa;

> *Rosa alikuwa amekwishakata shauri juu ya jambo hili. Alingoja kuchokozwa. Kweli Zakaria alichokoza mzinga wa nyuki. Rosa alitoka nje ghafla. Alikwenda mpaka karibu na baba yake. Alitapika maneno. Maneno haya alikuwa ameyatunza moyoni mwake kwa muda mrefu. "Kila wakati unatuchunga, unafikiri utatuoa wewe!" Rosa mwishowe aliyasema maneno aliyopaswa kusema siku ile aliyopigwa angali msichana (uk 58).*

Kutokana na hali ya Zakaria ya kumpiga Rosa, hali hii ilizua athari ya kumvunjia Zakaria heshima. Mwandishi anasema kuwa, Rosa aliyapata maneno na yakamchoma moyoni na kumfanya kusimama bila kusema lolote. Kwa upande mwingine Rosa inadhihirika kuwa alitembea kwa maringo hali ameinua mabega juu na kuonekana ameshinda. Baadaye hali ya Zakaria kuvunjiwa heshima na mwanawe, anaisimulia kwa rafikiye Ndalo.

## 2.3 Kulazimishwa Kuozwa

Kulingana na desturi nyingi za Kiafrika, hatima ya maisha ya vijana wa kike ni kuolewa. Haya yanatokana na baadhi ya tamaduni za Kiafrika, itikadi , dini na mtindo wa kijamii ambao unatokeza kuwa jukumu la mwanamke limo katika ndoa na hatima yake ni kuolewa. Jamii nyingi za Kiafrika mwanamke hana ruhusa ya kuchagua wala kujitafutia mchumba bali hutafutiwa haya yanatokana na taasubi inayotawala jamii. Wanawake hufahamika kama vitega uchumi vya kuletea wanaume mali kutokana na mahari yanayotolewa kabla ya kuozwa.

Ndoa zilizokuwa na msingi ya kitamaduni za enzi za jadi ziliongozwa na kupangwa na wazazi hasa wa kiume wa wachumba wanaohusika. Wazazi hawa walitekeleza mipango ya ndoa kwa siri, wakati mwingi bila kuwahusisha vijana wao na hata posa kupelekwa. Lilikuwa jambo la nadra kuwajulisha wasichana mipango hii na hata hivyo hawakuwa na budi kukubali

walilopangiwa. Hali hii inadhihirika katika utafiti wa Mirikau (2011), kuhusu, '*Taswira ya mwanamke katika jamii'* na ule wa Katola (2006), '*Udhalimu wa mwanawake'*.

Asasi ya ndoa imechorwa katika jamii ya *Rosa Mistika* kama inayomnyima kijana wa kike uhuru wa kujifanyia uamuzi. Katika *Rosa Mistika* (1971:38) Zakari anadhihirisha jinsi ndoa inavyomnyanyasa kijana wa kike,

> *"Zakaria alikuwa mkali sana katika mambo ya malezi ya binti zake lakini alipenda sana binti zake waolewe upesi iwezekanavyo".*

Nukuu hii inadhihirisha kuwa asasi ya ndoa inampa mwanamume mamlaka ya kuwaoza binti zake haraka hata bila kuangalia umri wao. Matakwa yao ni kuwa vijana wa kike waolewe upesi iwezekanavyo.

## 2.4 Kubakwa na Kupachikwa Mimba

Kubakwa ni tendo la kushikwa kwa nguvu na kutendewa dhuluma kingono bila hiari. Tendo la kupachikwa mimba nalo linahusu tendo la kutia mwanamke au msichana uja uzito. Vitendo hivi huathiri hisia na hali ya kiafya ya vijana wa kike hasa inavyodhihirika katika jamii ya Rosa. Vijana wa kike wanaathirika na kudhalilishwa na vijana wa kiume na hata wazee wanaotambulika kuwa hirimu ya rika la baba zao.

Katika *Rosa Misitika* (1971:85-86), Charles alijiuliza anapozungumza na nafsiye. Hali ya tendo la kubakwa linajidhihirisha na kubainika wazi kupitia maelezeo ya Charles ambapo dhamira inamsumbua kuhusu tendo lake ambalo si la hiari kwa mwenziwe Rosa.

> *"Dhamira yake ilimsumbua, 'Charles unafanya vibaya."*
> *Unatenda dhaubi? Mambo yote yangekwenda vizuri kama*
> *Charles asingeingiliwa na shetani. Alipata tamaa mbaya".*

*Kit*endo ambacho Charles alimtendea Rosa baada ya kumnajisi cha kumlaza chini sakafuni na kumwosha Rosa akiwa mlevi, ili asije akatambua njama ya kubakwakilimdhalilisha Rosa. Matendo haya yote yanadhirisha kwamba Charles alimtendea kijana mwenzake matendo ya kumdhalilisha tukio linalomtia katika hangaiko kwenye dhamira yake.

Dhuluma inayomkumba kijana wa kike inazua athari za kuwa na mimba isiyothaminiwa na mwanamume. Kuna ukosefu wa lengo la kuwa na mimba ikiwa wote wawili wa kiume na kike walioshiriki katika kuizua wana malengo tofauti yanayohitilafiana. Athari ya kuavya mimba inatokana na hali ya kiume inayodhihirika kuongozwa na taasubi ya ubabedume ambayo inakusudia kuwakandamiza vijana wa kike kimapenzi. Baadhi ya wanaume wanaongozwa na

uchu katika mapenzi pindi wanapofanikiwa katika malengo yao, wao hugeuka na kuwa hayawani dhidi ya wapenzi wao ambao hasa ni vigoli.

Katika *Rosa Mistika* (1971:45), Rosa anakumbana na maisha ya uhuru ambayo alikuwa akinyimwa kwa kuchungwa kama ng'ombe na kukatazwa kutangamana na wavulana. Anapopata nafasi ya kutangamana na wavulana na kuwa huru kutoka na mitego ya kuchungwachungwa na Zakaria, anajikuta amejulikana kwa kila mvulana. Mara alipata mimba mara mbili mtawaliwa. Mimba hizo zote zinadhihirika kutokea kwa sababu ya dhuluma kandamizi za kiubabedume. Inasemekana, Zakaria aliwanyima mabinti zake uhuru kwa kuwapiga na kuwakataza kuzungumza na mvulana yeyote na walipopata nafasi hii waliitumia kupita kiasi. Naye Flora, dadake Rosa katika *Rosa Mistika* inasemekana kuwa alitoa mimba akiwa shule ya Mwanza pale anapothibitisha kuwa;

*"Mimba tu haiwezi kunifanya nikajiharibia maisha yangu kwa kuacha shule." (uk 46)*

Hali hii ya kupata mimba kwa wingi kwa vijana wa kike wa Zakaria ina misingi ya mfumo kandamizi wa baba yao unaoongozwa na mila na desturi kandanamizi kwa vijana wa kike. Deogratias ni mmoja wa wanaume walioongozwa na uchu katika kuwakandamiza vijana wa kike. Anapowapachika mimba anaamua kukwepa majukumu, hali inayodhihirisha kuwanyanyasa vijana wa kike kimapenzi. Badala ya kujitokeza kama kielelezo bora kwa watoto wa shule anawakandamiza na kuwashawishi kwa kuwapa shilingi wasiseme siri ya mimba alizowapachika. Majadiliano ya Charles na Flora katika ukurasa wa 83 yanadhihirisha kuwa malezi ya kuwachunga wasichana yanazua athari kwa kijana wa kike. Wanaume wenye vyeo katika uongozi kama vile Deogratias, mkuu wa Wilaya, Thomas mkuu wa chuo cha Morogoro, ndio chanzo cha mimba wapatazo wasichana. Inabainika wazi kuwa wenye uwezo katika jamii ndio wanaowadhulumu vijana wa kike.

Hali ya vijana wa kiume na wanaume kupachika mimba vijana wa kike inadhihirisha dhuluma dhidi ya vijana wa kike kwani wale wanaotendewa uovu huo ni hasa wanafunzi wa shule. Tukio hili linawapotezea matumaini ya kuendelea na masomo yao au kusababisha matokeo mabaya masomoni. Katika Rosa Mistika (1971:40) Deogratias kwa jina la utani 'Bwana Maendeleo' anawadhulumu watoto wa shule akijisingizia kuwa kijana wa shule ilhali yeye ni mtu wa makamo. Haya yanajitokeza katika mazungumzo aliyoyasikia Rosa kati ya wanawake wawili kuwa;

*"Mbona yeye mzee wa miaka arobaini?*

*"Si ameoa, ana wanawake wawili, wote wasichana"*

*"Nasikia alikuwa amekwisha wapa mimba watoto wawili wa shule?(msisitizo wetu).*

Dhuluma zaidi inajitokeza kwa vijana waliopachikwa mimba na kushawishiwa kwa shilingi wasifumbue siri waliyotendewa badala wawajibikiwe na aliyewapachika mimba ipasavyo.

Rosa naye amelazwa hospitali kwa muda wa majuma mawili kutokana na hali ya kutoa mimba ya miezi miwili. Hali hii inatokea akiwa mwanafunzi wa chuo cha Morogoro katika mwaka wa kwanza na wa pili mtawalia.

## 2.5 Vitisho

Vitisho ni vitendo vya kuogofya au vya kutia hofu vinavyotendwa kwa madhumuni ya kumzima na kumtia woga anayelengwa ili asije akawa na ari ya kutaka kulifahamu jambo au kutolifuatilia. Vitisho vinavyoangaziwa katika utafiti huu ni vile vinavyojitokeza katika kazi tunazoshugulikia. Vitisho vinatumika kama njia ya kumkandamiza na kumtia woga kijana wa kike ili aweze kukubaliana na maoni ya dhuluma anayotendewa. Katika kazi tunayoshugulikia vijana wa kike wanakumbana na matusi na vitisho vinavyodhalilisha hali zao na kuwanyima haki zinazowahusu kama vijana wa kike.

Katika *Rosa Mistika* (1971:96) baada ya njama ya kurithi kila kitu kilichokuwa cha familia ya Mzee Zakaria, binti zake walitishwa walipojaribu kugusa kitu pale nyumbani. Walitishwa na kuambiwa kuwa si chao. Walielezewa kuwa pesa zao zilikuwa kwenye benki hivyo basi kudhihirisha kuwa hawakuwa na urithi katika mali ya wazazi wao.

Katika *Rosa Mistika* (1971:59) baada ya Rosa kugombana na babake. Zakaria yeye alinoa upanga na kumtishia kumkataka Rosa vipande vipande kama angedhubutu kurudi nyumbani. Hata baada ya Rosa kurudi nyumbani kutokana na vitisho vyake, mamake, Rosa anamshauri aondoke upesi kabla ya babake kurudi. Ilimbidi Rosa aondoke kwao na kuhamia kwa mama yake wa ubatizo kwa sababu ya vitisho vya babake.

Hali hii ya vitisho inaendelezwa na wanaume wanaopatikana kwenye riwaya tunayoshughulikia. Vitendo vyao dhidi ya vijana wa kike na lugha wanayoitumia inawadhalilisha vijana wa kike wanapoingiliana nao. Wanaume wanatumia vitisho hivyo kuwanyanyasa na kuwanyamazisha vijana wa kike huku wakiwanyima haki za kutangamana na vijana wenzao wa kiume.

Vijana wengi wa kike wanachungwa kama ng'ombe. Hali hii inawaogofya na kuwafanya kuishi kwa woga katika hali ya kutangamana na wenzi wao walio wavulana. Kutokana na hali hii wanapopata nafasi kwa sababu ya woga ule waliotiwa, huishia katika matendo yanayowasababishia madhara ya kupachikwa mimba. Flora anasema haya katika mazungumzo baina yake na Charles anaposema kuwa;

*"Labda wewe unaweza kuniambia: Kwa nini wasichana wengi wa shule yenu wanapata mimba zaidi kuliko shule zingine?"*

*"Sababu yenyewe nafikiri ni kwamba hatuna uhuru wa kutosha. Tunachungwa sana." (uk 82)*

## 2.6 Matusi

Katika utafiti huu matusi yanatumika kwa maana ya maonevu yanayotendewa kijana wa kike na yanahusu matumizi ya maneno yasiyo ya staha na yenye malengo ya kumuudhi kijana wa kike. Matusi yanatumika katika utafiti huu kama njia ya kumdhalilisha na kumkandamiza kijana wa kike yakiwa na lengo la kumnyamazisha. Katika kazi tunayoishughulikia matusi yametumika kumdhulumu na kumdunisha kijana wa kike kwa kumfedhehesha na kumpa hadhi ya chini dhidi ya kijana mwenzake wa kiume. Vijana wa kike wanahisi kuonewa kwani baadhi ya matusi wanayoitwa yanakwepa kutumiwa kwa vijana wa kiume. Kijana wa kike kuitwa 'malaya' na mshirika mwenzake wa kiume katika tendo linalomfanya aitwe 'malaya' haitwi 'malaya' ni mojawapo ya njia za kumtusi kijana wa kike. Tendo hili linamvunja moyo kijana wa kike na kujiona kuonewa na jinsia ya kiume.

Katika *Rosa Mistika* (1971:36), nguzo ya ubabedume ya kuwadhulumu bintize kwa kuwaonea aidha hata wao wakiwa bila makosa au kutumia kosa lililotendwa na mtoto wake tofauti kumwadhibu mtoto mwingine. Inadhihirika kuwa matusi yake Zakaria yanasikika pale yanapojitokeza kuwa;

*"Flora alikuwa sasa shule ya wasichana ya Mwanza. Alikuwa darasa la kumi. Alipokuwa anakuja likizo alikaripiwa kwa maneno ya kuogopesha na matusi."*

Vijana wa kiume wana taasubi ya kuwaonea na kuwadhalilisha vijana wenzao wa kike.Wanatumia maneno ya kuwaonea na kuwashushia hadhi wenzao wa kike. Vijana wa kiume katika majadiliano yao katika Chuo cha ualimu cha Morogoro wamembandika Rosa jina la "laboratory" yaani chumba cha kufanyia majaribio. Rosa mwenyewe anayasikiliza

mazungumuzo ya wavulana hao kutoka mwanzo hadi mwisho alipowafumania wakati walipokuwa wakiangalia gazeti. Jina "Lab" aliloitwa kwa kifupi ni la kumvunjia heshima na kumdhalilisha hasa inapobainika kuwa ni wavulana wanaolitumia dhidi yake.

Zakaria angali anaongozwa na taasubi ya ubabedume kwa kutumia maneno ya kuwavunjia binti zake heshima. Wakati mmoja baada ya Rosa kuwasili nyumbani, Regina anajaribu kumfahamisha Mzee Zakaria kuhusu kufika kwa bintiye Rosa aliyekuwa pale ndani. Zakaria aliguna tu na kusema "*Rosa ndiye nani?" Malaya hajawahi kuwa mgeni wangu wala mtoto wangu."_ (uk 57* )

Matendo ya kuathiri saikolojia yanahusisha athari inayovuruga hali ya nafsi au akili ya binadamu. Baadhi ya dhuluma dhidi ya kijana wa kike zinazua changamoto na kuchangia kuzua athari ya kihisia na kiakili. Kijana wa kike anakumbana na kandamizi zinazozua athari ya kuathiri saikolojia yake kutokana na kunyimwa uhuru wa kutangamana na vijana wenzao wa kiume. Pindi wanapotangamana nao wanakumbana na dhuluma ya kupigwa inayowafanya wawe na mtazamo mbaya kuhusu vijana wa kiume. Haya yanatokea Rosa anapodhihirisha kuwa Masumbuko, babake Rosa, hakujua kuwa;

> *"Mabinti wanahitaji uhuru fulani kutoka kwa baba zao, hakufahamu kwamba kwa kumpiga bintiye alikuwa akiingilia utawala usio wake, na kwamba kuhusu maoni ya ndoa yeye alifaa kidogo sana. Aidha, hakufahamu kwamba Rosa alihitaji kuwafahamu wavulana. Kwa hivyo, kutokana na malezi ya namna hii Rosa alianza kuwaangalia wavulana kama watu asiopaswa kutangamana nao katika jamii.Alidhaniwa kwamba alitakiwa kujitosheleza. Alizidi kuwa mnyamavu.* Uk 9 (msisitizo wetu.)

Hali hii ya kuwaonea na kuwa na mtazamo kuwa kijana wa kike hafai kuandamana na kuzungumza nao iliathiri hali ya nafsi ya Rosa. Kwa upande mwingine inadhihirika kuwa hali ya Rosa kuwa mnyamavu iliathiri hali ya kiakili kwa kijana Rosa na kusababisha kuona wavulana kwa mtazamo mbaya. Hali hii inachangia Rosa kuwa na mtazamo mbaya kwa vijana wa kiume inaposemwa kuwa;

> *Kweli Rosa, kwa wakati huu, alikuwa bado hataki kuzungumza na mvulana yeyote. Wavulana walipokuwa wakimsemesha aliwajibu kwa maneno makali ya kukatisha tamaa." (uk 22*).

Athari hii inatokana na dhuluma kandamizi za ubabedume zilizochochewa na mtazamo mbaya wa babake. Hali ya woga aliyotiwa na babake, ilimwathiri kimawazo kiasi cha kufanya usingizi kumpaa na kutoweka kwa muda anapoingia kulala. (uk 32.)

Changamoto ya athari ya kisaikolojia kwa vijana wa kike inachochewa na hali dhalimu ya kukanwa na wazazi wa kiume na matusi anayoelekezewa kijana wa kike. Hali ya kukanwa na kutusiwa inazua vurugu la kimawazo katika maisha ya Rosa. Katika ukurasa wa 57, Rosa anatiwa katika mashaka anapoitwa malaya na kukanwa na Zakaria. Alijiona kama mtoto mpotevu, alilia na hata kusita kama kweli Zakaria alikuwa babake wa kweli. Alifikiria kwamba hakuwa mtoto wake halali. Hata moyoni, alikuwa amevurugika kama mtu aliyetaka kutapika na hata hakuna yeyote aliyefahamu mawazo yake.

## 2.7 Kubaguliwa na kunyimwa uhuru

Kubaguliwa ni mbinu au hali ya kuweka au kutenga mtu katika kutoshiriki au kukosa kupata manufaa yafaayo ilhali mtu mwingine akifaidika kutokana nayo. Katika riwaya ya *Rosa Mistika* (1971) kijana wa kike ametengwa na kubaguliwa na asasi mbalimbali na zinamkuza kijana mwenzake wa kiume.

Katika asasi ya elimu kijana wa kike ametengwa na kubaguliwa kutokana na juhudi zake za kuweza kuitafuta elimu. Vijana wa kike hawana uhuru wa kujiendeleza kimasomo. Kijanawa kike anakumbana na changamoto nyingi katika hali yake ya kutafuta masomo. Wazazi wa kiume licha ya kuwa na uwezo wa kugharamia elimu ya vijana wao wa kike wanatumia fedha zao nyingi katika ulevi huku wakitoa visingizio kuwa hawana fedha ya kuwapeleka shuleni. Hili ni tukio linalomlazimu kijana wa kike kutafuta mbinu za kuendeleza masomo yao kwa kutafuta ajira. Kina mama walihusika kuwasaidia vijana wao wa kike kutafuta karo ya kugharamia elimu yao.

Katika *Rosa Mistika* inabidi mamake Rosa kuuza ngo'mbe mmoja kwa sababu alikuwa na nia ya kuendeleza binti zake katika masomo. Rosa alipopata barua iliyomjulisha kuhusu kuchaguliwa kwake ili ajiunge na shule ya upili ya Rosary, mamake Rosa anamshughulikia kutafuta karo ili Rosa aweze kujiunga na shule ya upili. Zakaria, babake Rosa, alisikika akisema kwamba hakuwa na pesa za kumpeleka Rosa katika shule ya upili ilhali siku hiyo alienda kunywa pombe. Hali hii inatokea katika ukurasa wa 9, kuwa;

*"Zakaria alikuwa amekwenda kusali kwenye pombe.*

*Aliponunua pombe alizoea kuinua bakuli juu na*

*kuwapatia watu akisema "kunyweni hii ndiyo damu yangu."*

Inadhihirika kwamba pombe aliyokuwa amenunulia watu alikuwa anatumia pesa zilizokuwa zimetengewa karo ya Rosa. Hali ya kuwanunulia wanaume pombe kwa kutumia fedha za karo inabainisha kuwa hakujali masomo ya bintiye lakini muhimu ni kuwanywesha pombe wanaume wenzake. Baada ya Zakaria kuvunja pesa za karo ilibidi Regina atengeneze pombe auze ili aweze kutafuta karo ya Rosa. Rosa na Flora wanahusishwa katika kuuza pombe hii ya kutafuta karo.

Vijana wa kike walibaguliwa katika jamii ya *Rosa Mistika*. Haya yanadhihirika wazi kutokana na ujenzi wa shule tano za upili za wavulana zilizopakana na shule moja tu ya wasichana ya Rosary. Shule tano zaidi zilikuwa zimejengwa za wavulana lakini shule moja ya wasichana ilitosha kufanya pale mahali pazuri pa kusomea (uk 21).Hali hii ya kuwa na shule nyingi za wavulana na moja tu ya wasichana inadhihirisha kuwa vijana wa kike wanabaguliwa katika hali ya kielimu. Katika jamii ya Rosa, Zakaria aliwakandamiza binti zake kwa kuwanyima uhuru wa kutangamana na wenzao wa kiume. Tendo hili la kuwanyima uhuru linamfanya asikike akijigamba na kujidai kuwa yeye alifahamu jinsi ya kuwalea binti zake. Hali hii inadhihirika katika ukurasa wa 9 kuwa;

> *"Hakufahamu kwamba mabinti wanahitaji uhuru fulani kutoka kwa baba zao; na kwamba kuhusu maoni ya ndoa yeye alifaa kidogo sana; na hakufahamu kwamba Rosa alihitaji kuwafahamu wavulana."*

Katika *Rosa Mistika* Mzee Zakaria anawabagua binti zake na kuwanyima uhuru wa kuendelea na masomo anapodai kuwa hana pesa huku akizitumia kwenye ulevi. Lakini wakati mtoto wa kiume Emmanuli anapozaliwa, Zakaria aliyekuwa akidai kutokuwa na pesa anafurahi mpaka akageuza mazungumzo na kumuuliza bibiye kama huko mjini nyama wanauzaje na anahitaji nini zaidi. Anapopewa orodha ya mahitaji, kesho yake alikwenda posta. Mkewe alishangaa wakati mumewe aliporudi jioni na vitu vyote alivyokuwa amevitaja. Ukurasa 24 unathibitisha kuwa alianza kupata sauti na furaha kiasi cha watu wa kijiji kustaajabu.

Taasubi hii ya ubabedume ya kuwanyima wasichana uhuru ilizidi kudumishwa na Zakaria pale inaposemwa kwenye ukurasa 25 kuwa; aliendelea pia kuwachunga binti zake kama ng'ombe,

dhuluma ya kuwalinganisha na wanyama wanaochungwa yaani ng'ombe. Inadhihirika kuwa pindi tu walipotoka shuleni walichungwa zaidi. Kwenye ukurasa wa 36 inabainika kuwa Honorata sasa alichungwa vikali na alizuiwa kuzungumza na mvulana yeyote. Emmanuel alibembelezwa na kutunzwa vizuri sana. Hali hii inamnyima kijana wa kike uhuru na yule wa kiume anapewa uhuru tulio ambalo ni dhihirisho la kumbagua kijana wa kike.

Hali hii ya kumbagua kijana wa kike Kuzua mtazamo kuwa hafai kutangamana na kuzungumza na vijana wa kiume, ni tukio lililoathiri hali ya nafsia ya Rosa. Kwa upande mwingine inadhihirika kuwa hali ya kuwa mnyamavu iliathiri hali ya kiakili ya kijana Rosa na kusababisha kuona wavulana kwa mtazamo hasi. Mtazamo huu mbaya wa Rosa kwa vijana wa kiume unadhihirika pale inaposemwa kuwa;

> *Kweli Rosa, kwa wakati huu, alikuwa bado hataki kuzungumza na mvulana yeyote. Wavulana walipokuwa wakimsemesha aliwajibu kwa maneno makali ya kukatisha tamaa." (uk 22*).

Kandamizi na dhuluma zinapowakumba vijana wa kike huishia kufanya maamuzi potovu dhidi ya hali inayowakumba katika maisha wanayoyaishi yenye matatizo mengi.

Baada ya kudhulumiwa kwa kubaguliwa na kunyimwa haki zake, kijana wa kike anajikuta akifanya maamuzi mabaya. Hali hii imechangiwa na changamoto kandamizi zinazowasonga na kuwadhulumu kijinsia. Katika riwaya ya *Rosa Mistika*, inadhihirika kuwa Rosa alifanya maamuzi mabaya. Anapokandamizwa na Zakaria, anasema;

> *Kama nikifanya urafiki na wavulana baba yangu atafahamu? Yeye yuko Ukerewe mimi niko Usukuma. Baba anakaa akinichunga, anafikiri yeye atanioa? Uk 32.*

Uamuzi wa Rosa wa kutaka kufanya urafiki unazidi kudhihirika katika ndoto yake katika ukurasa wa 32, ambapo Rosa anamwona kijana wa kiume na kuamua kumkimbilia na kumkumbatia akisema *"Lazima unioe! Ukinikataa wewe, maisha yangu yanakwisha sina tumaini tena!"* Hali hii ya fikira na ndoto zilidhihirika wakati ambapo aliamua kuingilia hali ya anasa na mapenzi kwa pupa (uk 33). Maamuzi haya yalizua athari ya kufukuzwa shuleni (uk 35), na kuendesha wavulana kama mtu aendeshaye punda (uk 33). Kulingana na maamuzi ya kutokuwa na matumaini, inadhihirika mwishoni mwake anapokataliwa na mpenzi wake Charles

na akafanya uamuzi wa kujiua. Kutokana na hali ya dhuluma ya kubaguliwa kijana wa kike anakumbana na athari ya kifo.

Kudunishwa kwa vijana wa kike na hali ya Zakaria kuwanyima uhuru wa kutangamana na vijana wa kiume, Rosa alikosa busara ya kufanya maamuzi anapochungwa kama ngo'mbe na babake. Inakuwa vigumu kufanya uamuzi wa busara anapoangukia mikononi mwa mwanamume Deogratias mwenye rika la babake, pale inaposemekana;

> *Ilikuwa siku ya kwanza Rosa kushikwa mikononi mwa mwanamume yeyote. 'Malezi mema' yalimfanya apende yule mwanamume wa kwanza kuonana naye (uk 41).*

Maamuzi haya ya kuona mwanamume wa kwanza kama mwenye malezi mema ndiyo yanayozua balaa. Baadaye, kijana Rosa alijikuta akipenda wapenzi wengi waliompachika mimba zilizozua madhara katika harakati ya kuziavya (uk 45-47). Dhuluma zinapowakumba vijana wa kike huishia kufanya maamuzi potovu dhidi ya hali inayowakumba katika maisha wanayoyaishi yenye matatizo mengi.

Dhuluma dhidi ya vijana wa kike inizua athari ya kukata tamaa. Hali hii inadhihirika wakati kijana wa kike anapokabiliwa na matatizo asiyoweza kuyatatua. Kijana wa kike anaonekana kama chanzo cha ukosefu wa raha kwa wazazi wa kiume katika jamii ya Rosa . Kijana huyu wa kike anaonekana akilaumiwa kuwa yeye ndiye kikwazo cha mzazi wake kuheshimika na jamii ya wanaume wenzao. Hali hii inachangia katika kuwadhulumu vijana wa kike kiasi kwamba wanaamua kukata tamaa katika maisha wanayoyaishi.

Rosa katika *Rosa Mistika* (1971) amekata tamaa anapofanya uamuzi kuwa kijana yeyote atakayetokea na kumchumbia, ataukubali uchumba wake. Baada ya kuwapoteza wachumba wake wote waliokuwa tegemeo la kumuoa kama Deogratias, Mkuu wa wilaya na Thomas mwalimu mkuu wa chuo cha ualimu. Inadhihirika kuwa hawa wote walikuwa wanashibisha na kukinai uchu wao katika mapenzi yao na Rosa. Inasemekana kuwa;

> *Na Rosa, hata kama angalimruhusu vile vile angalipoteza bahati yake. Rosa alikuwa akilenga Shabaha. Alimlenga mnyama wake. Mwindaji akibakia na mshale mmoja hutafuta mti mkubwa ili mradi akimkosa apande upesi kabla mnyama hajamla. Hivyo ndivyo Rosa alivyofanya (uk 80).*

Matamshi haya kumhusu Rosa yanadhihirisha hali ya kukata tamaa kutokana na maisha kandamizi na dhuluma ya kimapenzi aliyokumbana nayo kutoka kwa wanaume kandamizi. Anajiwa na bahati ya mwisho alinapoandikiwa barua na Charles na hali yake ya kukata tamaa inadhihirika wazi inaposemekana kuwa;

*Rosa aliona afadhali ajaribu bahati yake mara ya mwisho. Alipoombwa kidole cha pete na Charles, alihisi kuwa ni jambo kubwa ambalo halitokei mara nyingi. Hali hii ilimtia katika fikira na kuishia kusema kuwa;*

*"Kijana huyu lazima anioe; nikimkataa huyu basi maisha yangu yamekwisha ; sina tumaini tena."Rosa alikata shauri kupiga mshale wake wa mwisho, mshale huu ukienda pembeni, basi jitu-maisha-litaniua," Rosa aliwaza moyoni. (uk 76) (Msisitizo wetu)*

Kutokana na maelezo kuwa 'akimkataa kijana huyo maisha yake yamekwisha' ni dhihirisho bayana kuwa Rosa alikuwa amekwisha kata tamaa maishani mwake.

Inabainika kuwa Zakaria aliwakandamiza na kuwanyima binti zake uhuru. Uhuru huu unalinganishwa na kuwanyimwa mwanga wakati ule walipokuwa wakiuhitaji sana. Wakati anapowapiga na kuwakataza kuzungumza na mvulana yeyote, binti zake wanazama na kukolea katika maovu.Wanamithilishwa na mti unaonyimwa mwanga na miti mingine na unavyojaribu kujirefusha ili upate mwanga. Vivyo hivyo ndivyo Rosa alivyong'ang'ania mapenzi yaliyokuwa na tamati ya kuavya mimba mara tatu au nne, inavyojitokeza kwenye ukurasa 47. Hali hii hii ilisababisha atumiwe padri mmoja na anaposhauriwa na padri alidhihirisha hali ya kukata tamaa pale padri anapomwelezea baada ya kumsomea Biblia kuwa;

*"Usikate tamaa Rosa, usikate tamaa. Kukata tamaa ni dhambi isiyoweza kuondolewa hapa duniani. Yesu bado yu nawe. Katika mfano huu utamwona akimwondolea dhambi mwanamke msherati. Wokovu uko bado machoni mwako." (uk 47).*

Hali ya Rosa katika kujibu shauri la padri ina wingi wa kudhihirisha kukata tamaa kwake anapomjibu padri;

*Rosa alianza kutapika maneno, na matapishi hayamezwi tena. "Wokovu maana yake nini? Wokovu! Wokovu gani! Kama kuna moto basi nitakwenda!" (uk 49) (msisitizo wetu)*

Maneno "kama kuna moto basi nitakwenda" ni dhihirisho kuwa Rosa alikuwa amekata tamaa.

## 2.8 Kuchuuzwa

Hii ni hali ya kuuza vitu rejareja kwa kuvitembeza au kutangaza bei kwa minajili ya kuviuza na kupata manufaa ya kibiashara.

Suala la kuchuuza wanawake limeshughulikiwa katika *The Female Eunuch na Whole Woman* ambapo Greer (1981) anapendekeza kuwa wanawake wanapaswa kuhusishwa katika asasi ya ndoa inayowakandamiza. Anaona kuwa, kwa kuolewa mwanamke anageuzwa na kuwa kitu cha kumilikiwa na kuwapo kwake hufutwa. Kimani (2003) anasema kuwa vijana wa kike huchukuliwa kama vitega uchumi kwani wanapovunja ungo, huozwa kwa wanaume wanaochaguliwa na wazazi wao wa kiume. Kigezo cha kumwoza kijana wa kike ni utajiri unaotokana na mahari itakayotolewa na wala sio mapenzi. Kijana wa kike huishia kuwa kama mali ya anayelipa mahari.

Wanaume wengi inadhihirika kuwa wanawachukulia vijana wa kike kama bidhaa za kuwaletea mali. Mwanamume anapoongozwa na haja ya utajiri hutafuta mnunuzi anayeweza kutoa pato na huuza bidhaa zake kwake. Si ajabu Mzee Zakaria katika *Rosa Mistika* (1971:20) anasema kuwa "*Atakayeninunulia madebe mawili ya pombe nitampatia binti yangu aoe*"

Rosa alipopata mchumba, Zakaria alifurahi kwani alipenda sana binti zake waolewe upesi iwezekanavyo.

Deogratias alipofika kwa kina Rosa kupeleka Posa, babake anamwambia kama ni swala la mahari walikuwa wamekwishalizungumzia na bibi yake na hangempa jibu na kisha anaanza kusema,

> "*Bila shaka tunahitaji nyumba, utatoa ng'ombe wanne, mbuzi wawili, kinu, viti vitatu na shilingi elfu moja. Nimeongezea debe moja la pombe ya moshi", (uk 39*).

Kando na kumtajia malipo haya anamwambia Deogratias kuwa angemtuma kwa jamaa zake wote na pia kwa jamaa za mke wake na wao pia wataongezea mahitaji yao.

## 2.9 Kunyanyaswa Kimapenzi

Kunyanyasa ni kauli ya kumtendea au kumfanyia mtu vitendo vya dharau, kudhalilisha na kumfanya kuwa si mtu. Riwaya ya *Rosa Mistika* (1971) inadhihirisha maonevu ya kijana wa kike kunyanyaswa kimapenzi kutokana na mtazamo wa ubabedume.

Mzee Deogratias aliye na umri wa makamo anadhihirisha ukandamizaji kwa vijana wa kike katika umri wao mdogo na hata wale walio shuleni. Ili kujishusha na kupata kutangamana na kijana huyu inambidi atumie hila kuwa yeye ni mwanafunzi wa shule ya upili kiasi cha hata Rosa anamwita kijana anaposema katika ukurasa wa 34;

"Ninamfumia kitambaa boy wangu D." Huyu anayeitwa 'boy" inadhihirika wazi anapokuwa jela kuwa ni mzee katika ukurasa wa 40, "Watu walimcheka kiasi cha kushikilia mbavu aliposema kuwa alikuwa bado hajaoa." Wakati huo Deogratias hakuwa na kofia na nywele nyeupe ingawa hazikuwa nyingi zilikuwa zinaonekana. Dai lake la kumnyanyasa Rosa kuwa yeye ni kijana linafichuliwa wakati inapobainika kwa Rosa kuwa si yeye tu msichana wa shule aliyekuwa amehadahiwa bali kuna wengine aliokuwa amewaoa na wengine kuwapa mimba.

*"Huyu ndiye Rosa aliyemfanya Deogratias akafungwa"*

*"Yule Bwana Maendeleo wa Mwanza!"*

*" Ndiyo, huyo huyo".*

*"Mbona yeye mzee wa miaka arobaini?"*

*"Si ameoa, ana wanawake wawili, wote wasichana".*

*"Nasikia alikuwa amekwishawapa mimba watoto wawili wa shule?"*

*"Ndiyo, lakini aliwapa shilingi wasiseme".(uk 40-41) (msisitizo wetu).*

Deogratias anawanyanyasa vijana wa kike kimapenzi ilhali umri wake ulikuwa sawa na wa babake Rosa. Inabainika kuwa licha ya kuwanyanyasa vijana wa kike kimapenzi aliwahonga wasimseme wala kufichua siri ya kimapenzi.

Asasi ya uongozi ni mojawapo ya asasi kandamizi dhidi ya vijana wa kike katika jamii ya Rosa. Mwalimu mkuu wa Chuo cha Ualimu cha Morogoro naye anawadhulumu wanafunzi wake shuleni. Katika *Rosa Mistika*, ukurasa 51, yeye kama kiongozi anayepaswa kuwa kielelezo bora

katika jamii yake anashiriki ngono na mwanafunzi wake na kisha kusababisha hata dhuluma kwa Rosa anapokatwa sikio. Kunyanyasa kwa mwalimu mkuu kunachangia kufukuzwa kwa Rosa kutoka chuoni.

Viongozi wengine kama mkuu wa wiliya wanashiriki pia katika kuwakandamiza na kuwadhulumu vijana wa kike. Watu walio na umri wa makamo na wanaofaa kuchangia katika kuongoza vijana wa kike katika jamii ndio tena walio katika msitari wa mbele kuwadhulumu vijana wa kike kimapenzi. Hata baada ya kukemewa na Mzee Zakaria kwenye uk 58 anaposema;

> "*Rudi na motokaa yako! Unafikiri hapa kuna wasichana wengi wa kuchukuwa kwa gari. Toka hapa!*"

Mkuu wa wilaya alipiga hatua ya kumchukua Rosa na kwenda "Beach" na siku hiyo Rosa hakurudi nyumbani kwao. Charles mchumba wake Rosa, na tegemeo lake la mwisho anadhihirisha dhuluma kandamizi ya kumnyanyasa kijana wa kike. Baada ya kumfanyia tendo la siri na kugundua siri ya ubikira na aliamua kuvunja uchumba wake. Sababu ya tukio hili inachangia hatima ya Rosa kujiua.

Imebainika kuwa watu wazima ambao ni wanaume ndio waliowanyanyasa kimapenzi vijana wa kike katika jamii ya Rosa. Flora na Charles wanapojadiliana katika *Rosa Mistika* uk 83, Charles anatoa kauli kuwa "Zaidi ya hayo ninaona kwamba watu wakubwawakubwa ndio wapatiao wasichana mimba wala siyo wanafunzi". (msisitizo wetu). Katika majadiliano wanasema kuwa mara nyingi wanafunzi husingiziwa kuwapachika mimba vijana wa kike, na lakini hata kama ni wanafunzi wanaweza kuoana baadaye. Inadhihirika kuwa wafanyikazi wakubwa wengi wameoa dhihirisho kwamba wana hila za kuwanyanyasa vijana wa kike tu.

Flora katika *Rosa Mistika* alidhihirisha jinsi kijana mmoja wa kiume alivyomwambukiza ugonjwa wa zinaa. Aliambukizwa ugonjwa wa zinaa kwa sababu ya kufanya uamuzi mbaya kutokana na dhuluma za ubabedume zilizomnyima nafasi ya kutangamana na wavulana. Anapopata nafasi hiyo anazama kwa pupa katika mapenzi bila kuwa na tahadhari. Tukio hili linasababisha maradhi ya zinaa inavyobainika kwenye ukurasa 63. Naye Rosa anafanya maamuzi ya kutaka kujioza kwa mkuu wa chuo kikuu kutokana na kuchukia msimamo wa babake.

Rosa, (uk 90) aliona kuwa ulimwengu mzima ulimkataa hasa baada ya kukataliwa na mchumba wake wa mwisho aliyekuwa tegemeo la mwisho. Alipobaini kuwa mchumba huyu aliongozwa na uchu katika kufumbua siri, aliamua kukata tamaa. Maisha kandamizi aliyoyapitia na mateso yenye misingi na mifumo ya ubabedume ilimtia Rosa katika maamuzi ya kujiua. Haya yanadhihirika pale Rosa anapoona kuwa dunia imefika mwisho. Amekata tamaa mwandishi anaposema;

> *Aliona ulimwengu wote ukimwonea huruma, lakini sasa aliona kama kwamba ulimwengu wote ulikuwa ukimchekelea. Kuishi aliona hawezi. Aliona ni fedheha (uk 90).*

Baada ya kusaga chupa na kutia ungaunga wa vipande vya chupa kwenye glasi na kuongeza maji, aliyanywa yale maji akasikika katika maneno yake ya mwisho kabla ya kuaga yakiwalaumu wanaume. Alisema kuwa wanaume ndio waliochangia kukata tamaa kwake kulikosababisha kufanya uamuzi wa kujiua. Anasema;

> *"Sasa ninakufa, ninakufa sasa. Maisha yangu yalikuwa magumu. Sasa nimeona wazi kwamba malezi yangu ndiyo yalikuwa chanzo cha taabu. Malezi, siyo malezi ya mama, lakini malezi ya baba yangu. Kweli baba alinichunga. Nilichungwa kama msichana wa jela. Nilipopata uhuru nilishindwa kuutumia. Deogratias , Thomas, Charles – wote hao nimewapoteza (uk 91) (msisitizo wetu).*

Kutokana na haya inabainika kuwa, mwanamume ndiye chanzo cha dhuluma kandamizi dhidi ya vijana wa kike katika jamii ya Rosa.

Wasichana wawili katika *Rosa Mistika* (1971:40) waliolewa na Deogratias, mwanamume ambaye hakuwa mwaminifu katika ndoa. Deogratias anawapachika mimba vijana wa kike wawili wa shule aliowashawishi kwa shilingi ili wasitoe siri yake ili hali alikuwai bado anamng'ang'ania Rosa. Wanawake wawili katika safari yao wanabainisha wazi ukosefu wa uaminifu wa Deogratias pale wanapoeleza wazi kuwa;

> *Deogratias alikuwa mmoja kati ya wale wazee wanaojifikiria bado vijana, wazee wanaopendelea kutembea na vitoto vidogo hata vile vinavyoanza kuota maziwa. Watoto wao wa kuzaa. Wazee wanaomezea mate matiti ya mtoto mdogo. Kwa wakati huu alikuwa akihitaji mwanamke wa tatu na bahati alikuwa amekwishaipata.(uk 71)*

Tabia hii ya Deogratias kuwatafuta vijana wa kike inadhihirisha kuwa alikuwa akiwanyanyasa kimapenzi.Tukio hili linabainika anapowapachika mimba na kuwatenga na hata kuwatishia wengine. Tayari alikuwa ameoa vijana wengine wawili ambao hakuwa mwaminifu kwao. Ndoa hii ya mwanamume huyu inaongozwa na uchu ambao unawafanya wakeze kuishi maisha yenye wasiwasi na hofu bila kujua mipango yoyote ya mume wao.

Mwalimu Thomas alikuwa na mpango wa kumuoa Rosa na ndoa hii ilikuwa yenye misingi iliyokuwa na msukumo wa uchu. Inabainika kuwa Thomas hakuwa mwaminifu kwa wake zake watatu waliotangulia. Wakati huu alikuwa na mpango wa kumfukuza mke aliyekuwa naye ili kumchukua Rosa. Lengo hili linaonekana wazi anapoacha kimakusudi barua aliyomwandikia Rosa ili kumfukuza mkewe. Ukosefu wa uaminifu katika ndoa yake Thomas unadhihirika wazi;

> *Mwalimu mkuu Thomas alikuwa mtu ambaye alielewa kwamba ndoa ni maisha ya watu wawili, mume na mke, mpaka siku watakayoafikiana; siyo mpaka kufa! Huyo aliyekwenda alikuwa mke wake wa tatu. Thomas alikuwa amefanya hila ili amfukuze mke wake bila kumwambia ( uk 52).*

Katika *Rosa Mistika* urafiki wa Rosa na afisa anayefanya kazi kwenye benki pamoja na ule wa Deogratias ulichangia Rosa kufanya vibaya kwenye mtihani na hata kufukuzwa shuleni. Hali hii inadhihirika pale Rosa anapofukuzwa na kuagizwa kurejea shuleni kufanya mtihani wake wa *Cambridge*. Kutofanya mitihani yake ya mwisho katika shule ya upili na chuo cha ualimu iliathiriwa pakubwa na vishawishi vya kiume vya kumkandamiza Rosa kimapenzi.

## 2.10 Kukanwa na Jamii

Vijana wengi wa kike wanapokiuka na kutofautiana na matakwa ya wanaume hasa baba zao, jamii yao inawadhulumu na kuwakataa, Jamii ya Rosa inawaona vijana wa kike kama watu wanaostahili kutengwa. Haya ni kutokana na imani na misingi kwamba wanaaibisha jamii na jinsia ya kiume kwa jumla. Wanaume mara nyingi huwakana vijana wa kike na daima wanawatarajia watende kulingana na matakwa yao hata kama ni tukio lenye misingi ya kuwakandamiza na kuwadhulumu. Vijana wa kike wanaokiuka matakwa ya kiume hukataliwa na jamii za wanaume hao.

Katika *Rosa Mistika* (1971:36) baada ya Rosa kufukuzwa shuleni marafiki zake waliposikia sifa zake mbaya inabainika kuwa polepole Rosa alianza kuwapoteza. Inabainika kuwa baadhi ya

marafiki hao walikuwa marafiki kwa muda tu. Marafiki hawa inadhihirika kuwa hawakuwa tayari kuwa na ule urafiki wa kufaana wakati wa shida na faraja.

Rosa mwanafunzi wa chuo cha Ualimu cha Morogoro baada ya kupatikana na makosa, jamii ya chuo cha ualimu ikiongozwa ma mwalimu mkuu Albert ambaye ni mwanaume inaamua kumfukuza Rosa. Albert anapoombwa msamaha na hata kushuhudia jaribio la Rosa kujiua kwa sababu ya kufukuzwa chuoni, hakuwa tayari kumpa msamaha bali anamchukulia hatua ya kumfungia kwenye kijumba mfano wa jela. Baadaye alimsindikiza kwa gari na kuhakikisha kwamba ameabiri gari la kuenda kwao. Hili ni dhihirisho kwamba kijana huyu alikuwa amekataliwa na jamii.

Matamshi ya Zakaria na kandamizi zake dhidi ya Rosa zinamfanya awe na moyo wa kukata tamaa kuhusu uhusiano wake na babake. Hii ni hali ambayo inamfanya kuamua kutorudi nyumbani baada ya kukosana na babake. Inabainika katika majibizano kati ya Zakaria na Rosa, kukataliwa kwa Rosa. Haya yanadhihirika katika majibizano kuwa;

> *"Rosa tangu leo wewe si mtoto wangu"*
>
> *"Tangu leo wewe si baba yangu" Rosa alidakia bila kukawia. Aliingia mara moja ndani ya motokaa na kwenda zake Beach. Siku hiyo Rosa hakurudi nyumbani (uk 58). Na baada ya kurudi nyumbani alifunga virago na kwenda kwa mama yake wa ubatizo.*

Kijana wa kike anapokataliwa na jamii huathirika kimawazo na kufanya uamuzi wa kuhamia kwao na kumkana mzazi wake pia.Kijana Rosa alipokataliwa na mwalimu mkuu aliamua kufanya jaribio la kujiua kwa kutumia kamba na alipoikosa akajaribu kujidunga kisu.

> *Rosa alianza kukisukuma kisu polepole ili kingie tumboni mwake.Ngozi ya juu ilikuwa imekwishakwaruzwa alipostukia mkono wake unashikwa. Rosa alikuwa mikononi mwa Albert.*
>
> *Kijana wa kike hukumbana na mawazo katika fikra zake, tendo linalomtia kwenye hangaiko la kimawazo na hata kudhamiria kujiua.*

## 2.11 Hitimisho

Katika sura hii utafiti wetu umeangazia aina mbalimbali za dhuluma na athari zake kwa kijana wa kike kama inavyodhihirika katika riwaya ya *Rosa Mistika* (1971). Hali hizi za dhuluma na

athari zake ambazo tumeziangazia zinadhihirisha jinsi vijana wa kike wanavyokumbana na maonevu na udhalilishaji. Dhuluma na athari hizi zinadhihirika kutokana na misingi wanayoshikilia wanaume na vijana wa kiume dhidi ya kumkandamiza kijana wa kike katika riwaya ya *Rosa Mistika.*

Kudharauliwa ni mojawapo ya dhuluma zinayowakumba vijana wa kike katika jamii ya Rosa inayoendelezwa na upande wa kuumeni. Kudharauliwa kwa kijana wa kike kunatokana na misingi kuwa yeye ni kiumbe duni kijinsia anapolinganishwa na mwenziwe wa kiume.

Vijana wengi wa kike wanakumbwa na hali ya kupachikwa mimba na wazee wa makamo ambao huishia kuwatisha kama watawahusisha na mimba hizo. Kutokana na hali hii vijana wengi wanakumbana na matatizo mengi ya kiafya na hata kulazamika au kushauriwa kuziavya mimba hizo.

Mara nyingi vijana wa kike wanadhalilishwa kwa kutumika kama bidhaa zinazoweza kuchuuzwa na kuletea wazazi wa kiume faida au mali ili waweze kunufaika kiuchumi. Hisia na matakwa ya vijana hawa wa kike zinapuziliwa mbali na mfumo wa ubabedume. Inadhihirika kwamba vijana hawa ni kama vyombo vya kunadiwa na wanaume na thamani yao hata huweza kulinganishwa na madebe mawili ya pombe (uk 20).

Kijana wa kike anakumbana na vitisho na matusi kwa minajili ya kutiwa woga na hofu. Kusudi la kutiwa woga ni kuwa aweze kuwatii, kuwanyenyekea na kuwatambua wanaume kuwa wao ndio viongozi wenye mamlaka. Inadhihirika kwamba wanaume wana usemi kuhusu maisha ya kijana wa kike yanategemea mwongozo wa wanaume.

Udhalimu mwingine unaowakumba vijana wa kike ni kunyanyaswa kimapenzi. Wazee wa umri wa makamo na hata wengine ambao ni viongozi wanaopaswa kuwapa vijana wa kike mwelekeo ndio wanaowakandamiza kimapenzi. Wanaume hawa wanatumia vyeo vyao na mali waliyonayo katika kuwashawishi vijana kukubali kuwatumia kingono. Wengi wa wanaume hawa huwageuka na kuwakana vijana hao wanapopata mimba. Wanaume wengi huwaona vijana wa kike kama ni vyombo tu vya kuwatumbuiza na vya kushiriki nao kimapenzi.

Inadhihirika na kubainika kuwa licha ya kandamizi na udhalilishaji unaowakumba, vijana wa kike wana uwezo na ari ya kujitetea na kufanya maamuzi ya kutetea uhuru na haki zao. Nadharia ya Ufeministi huru tuliyoitumia inadhihirisha kuwa vijana wa kike hujibidiisha na kupambana

kujikomboa wenyewe kutokana na dhuluma zenye misingi na mifumo ya ubabe dume. Hata hivyo baadhi ya vijana wa kike wana misimamo thabiti ya kupambana na dhuluma kandamizi wanazofanyiwa na wanaume.

Kijana wa kike katika jamii ya *Rosa Mistika* ana ari kubwa katika kujiendeleza kimasomo. Hata hivyo juhudi zake zinakumbana na vizuizi na vikwazo vinavyoendelezwa na udhalimu wa wanaume ambao una misingi ya kumtweza kijana wa kike huku mwenzake wa kiume akitwazwa. Udhalimu huu wa kuwanyima vijana wa kike uhuru katika masomo unapata upinzani mkali kutoka kwa vijana wa kike.Vijana wa kike wanajitolea kupuuza vikwazo wanavyowekewa na wanaume waliobobea katika mifumo yenye itikadi na mila zinazoongozwa na ubabedume. Hali hii ya tetezi ya vijana wa kike katika kupata uhuru katika masomo inaafiki nadharia ya Ufeministi Huru unaodhamiria kumkomboa mwanamke kutokana na minyororo ya dhuluma kandamizi yenye misingi katika mila na tamaduni.

Mwandishi wa *Rosa Mistika* (ukurasa 19-21) anatoa taswira ya jinsi misingi ya yenye mashiko katika itikadi na mila inavyomwongoza Mzee Zakaria katika kupora pesa zilizotengewa karo ya Rosa na kuzitumia kuwanywesha wanaume wenzake pombe. Tukio hili linasababisha Rosa kukosa kujiunga na shule ya upili alipokuwa anatakiwa kujiunga katika kidato cha kwanza. Hali hii inafanya maafisa kung'ang'ania nafasi yake, huku maafisa wengine wakitumia hila kuwa Rosa alikufa maji wakati wa kuogelea ziwani. Kulingana na Nadharia ya Ufeministi Huru, mwanamke anastahili kuwa na mwamko wa kujikomboa kutokana na dhuluma kandamizi. Rosa hakufa moyo baada ya Zakaria kupora pesa zilizotengewa karo yake. Anashirikiana na mamaye na dadake katika kuuza pombe na walifanikiwa kupata pesa za kumwezesha kujiunga na shule baada ya mwezi mmoja.

Wanaume wenye uchu wa mapenzi kama vile mfanyi kazi wa benki, Deogratias, Thomas na mwalimu mkuu wanao uwezo wa kuwaelekeza vijana wa kike walio shuleni, lakini wanashibisha tamaa zao zinazochangia kuwaletea vijana wa kike athari ya kufukuzwa shuleni.

Kutokana na dhuluma na athari zake vijana wa kike wanafanya maamuzi yasiyo ya busara na baadhi yao mengine ni mapotovu yanayoishia katika kuwatia kwenye dhiki. Kutokana na shida wanazokumbana nazo, baadhi ya vijana wa kike wamekata tamaa katika maisha yao baada ya kushindwa kujimudu kimaisha. Wao hutazama matatizo na hali hizo kandamizi kama ni vigumu kujinasua kutokana nazo. Ukataji tamaa wao umechangia katika kutoa maamuzi makali dhidi ya

maisha wanayoyaishi kama vile Rosa alivyoamua kujiua baada ya kukataliwa na mchumba aliyemwona kama tegemeo lake la mwisho katika maisha yake.

Katika sura hii tumeshughulikia dhuluma dhidi ya vijana wa kike na athari zake katika riwaya ya Kezilahabi ya *Rosa Mistika (1971)* . Katika sura ifuatayo tunashughulikia dhuluma dhidi ya vijana wa kike na athari zake katika riwaya ya Momanyi ya *Tumaini (2006).*

# SURA YA TATU

# DHULUMA NA ATHARI ZAKE DHIDI YA VIJANA WA KIKE KATIKA RIWAYA YA TUMAINI

## 3.0 Utangulizi

Katika sura hii tunachanganua dhuluma na athari zinazowakumba wahusika vijana wa kike na mbinu au juhudi wanazozitia katika harakati za kujiepusha na hali hii kandamizi inayodhalilisha jinsia yao.

Wengi wa wahusika vijana wa kike katika fasihi ya Kiswahili hukabiliwa na changamoto ya udhalimu kutokana na taasubi kandamizi ya ubabedume. Kijana wa kike katika mazingira ya Kiafrika ana uwezo wa kuwa na ujasiri wa kujitetea na kuishi bila ya kunyanyaswa, kuwa na ushujaa wa kuwa kiongozi na ana nafasi kubwa katika ujenzi wa jamii anamoishi.

Katika sura hii tumeangazia swala la kuchanganua na kuchunguza athari za dhuluma dhidi ya kijana wa kike. Athari tunazoziangazia zimejitokeza katika riwaya ya *Tumaini* (2006) ya C.Momanyi. Athari hizo ni pamoja na: kuingiwa na woga, kuteseka, kuathiriwa kihisia, kufanya uamuzi mbaya, kukata tamaa, kupachikwa na kuafya mimba, kuathiriwa kimasomo na kuwa katika ndoa zenye machungu.

Dhuluma kandamizi zimejikita katika mitazamo na mifumo kandamizi yenye misingi katika mila na tamaduni ya kuumeni ambayo imezua athari tata katika maisha ya vijana wa kike katika jamii ya Tumaini.

## 3.1 Kudharauliwa

*Tumaini* ambayo ni riwaya ya Clara Momanyi ya mwaka wa 2006, imemwangazia mhusika kijana wa kike Tumaini na vijana wengine wa kike ambao wamedharauliwa katika jamii yao. Hali hii ya kudharauliwa kwa kijana wa kike inajitokeza wakati Idi kijana mdogo wa kiume anaposema;

*"yapi hayo, si utaolewa tu'" Idi alimjibu kwa dharau. (uk 29)*

Tukio la kuwa ataolewa lilimfanya Tumaini kumwangalia Idi ,kakake Tumaini kwa muda. Alielewa kuwa tabia ya Idi kuwadharau vijana wa kike illitokana na kielelezo halisi cha malezi ya babake. Kijana mdogo Idi tayari alijua kuwa vijana wa kike ni vifaa vya utumishi vya

nyumbani mwao. Katika riwaya ya *Tumaini* (2006:29), Idi anadhihirisha dharau kwa vijana wa kike anaposhawishiwa na dadake Tumaini amsaidie kuchochea moto mekoni au kuteka maji. Idi alimjibu kuwa ile ilikuwa kazi ya wanawake. Hii ni dhuluma ya kudharau hali ya dadake kama msichana. Inadhihirika wazi kuwa majukumu yananayotekelezwa na vijana wa kike ni duni, hayawezi kutekelezwa na kijana wa kiume.

Vijana wa kike kama Waridi na Almasi katika *Tumaini* (2006), walikuwa wamekosa matumaini ya kufanya vyema katika masomo ya Hesabu na Sayansi kutokana na mtazamo wa jamii yao kuhusu jinsia yao na masomo haya. Hali ambayo ilichangiwa na kuvunjwa moyo ilitokana na itikadi kuwa masomo hayo ni ya wavulana na wala si ya wasichana. Tukio hili limemfanya Almasi kuchukia hata mwalimu anayefundisha hesabu. Kwa upande mwingine mwalimu wake wa hesabu anamvunja moyo Almasi kwani anapoanguka na kupata sufuri, mwalimu aliichora sufuri na kuitia macho, pua na mdomo. Licha ya Tumaini kuwashauri kuwa;

> *Mkiamini kwa dhati kuwa sayansi na hesabu siyo masomo yaliyotengewa wavulana pekee, bila shaka mtafaulu. "Hivi ndivyo ninavyoamini." (uk 74)*

Licha ya wasichana hao kuwaza na kuyapima maneno ya Tumaini kwa muda kuhusu ushauri wake, wanadhihirisha hali ya kukata tamaa pale wanaposema;

> *Pengine maneno yako yana ukweli fulani, lakini sasa hatuna muda tena wa kurekebisha mambo. Imebaki miezi kadhaa tu kisha tuufanye mtihani huo tuanguke (uk 74) ( msisitizo wetu).*

Hali hii ya wasichana hawa inadhihirisha kuwa tayari wamekata tamaa katika masomo. Kiini hasa cha kukata tama kikiwa ni taasubi ya kiume kuwa masomo ya Sayansi na Hisabati ni ya wavulana. Misingi ya wanaume na ya wavulana ni kuwa wasichana hawatayaweza ila kusubiri kuolewa tu. Mashikilio haya ni ya Masumbuko, kijana Idi na mwalimu Majaaliwa wenye mashiko ya itikadi na mila zenye misingi ya kiubabedume.

## 3.2 Kupigwa

Momanyi (1998), anaelezea kwamba jamii nyingi za Kiafrika zina mifumo ya kuumeni yenye utaratibu na masharti yanayohalalisha asasi za kijamii zenye kuhimili tofauti za kiuana katika

ugawaji wa kazi. Utaratibu huu humpa mwanamume nguvu dhidi ya mwenzake wa kike katika nyanja zote za kimaisha, kisiasa, kiuchumi na hata kijamii katika ugawaji wa majukumu.

Masumbuko, babake Tumaini katika *Tumaini,* (1971:13) alikuwa na mazoea ya kuwadhulumu binti zake kwa kuwapiga hata kwa kosa dogo tu. Baada ya kulewa, haya yanadhihirika wazi pale inapojitokeza kuwa;

> *Baada ya kuchapa maji, mzee huyu alisepetuka huku akibwata maneno yaliyosheheni nishani za ulevi. Hapo ndipo wanawe walipokimbia na kujificha kwani aliwapiga kwa kosa dogo tu.*

Tamaduni nyingi za Kiafrika zinampa uwezo na uhuru mwanamume kumpiga mkewe na watoto wake. Mwanamume ana uhuru wa kuwapiga watoto wake, ilhali mwanamke hana uwezo wa kuingilia kuwauni. Atakapoingilia kuwauni yeye basi hujumuishwa katika kundi linalopigwa. Hali hii ya tamaduni humfanya mwanawake kuwa mtazamaji wa kuona vioja vya kipigo kwa wanawe bila kunena lolote. Ndiposa katika *Tumaini* (2006), Bi Amina hashiriki kuwauni vijana wa kike wake wanapopigwa hadi mpita njia atokee na kumkemea Mzee Masumbuko. Tumaini anaelezea masaibu yanayowakumba bila mama yao kuingilia, anaposema;

> *" Baba ana mazoea ya kutuadhibu kwa kututia ndani ya gunia pamoja na majani ya upupu. Natumaini mnajua jinsi yanavyowasha.Baada ya kulifunga gunia ndi kwa kamba, ndipo anapomchapa anayeaadhibiwa hadi fimbo ivunjike vipande vipande. Isipovunjika, nakwambia ataendelea kuchapwa hadi mpita njia atokee kumkemea. Wakati huo wote, mama husimama mbali, na hathubutu kutamka lolote" "Mwanamume atayetokea na kumkemea anapomwadhibu wanawe hana budi kuwa asiri''.*

Tendo la kupigwa lilizua athari ya kuwaumiza vijana wa kike kimwili na kuwaogofya. Kutokana na hali ya kupigwa vijana wa kike wanaogopa kuishi kwao na kukimbilia mahali penye hifadhi. Hali ya kupigwa pamoja na vitisho ilisababisha Tumaini kugura kwao na kutafuta hifadhi kwa Bi Halima.

## 3.3 Tohara

Tohara ni tendo au tukio linalotumika kama kigezo katika tamaduni fulani ya kuwapeleka vijana jando ili waweze kuvuka kutoka kiwango cha utoto hadi utu uzima.

Katika utamaduni wa riwaya ya *Tumaini* (2006) tohara ni tendo ambalo jamii ya Tumaini inalienzi. Jamii hutumia tendo hilo kama kigezo cha kuwaandaa vijana wa kike katika asasi ya ndoa. Anayekwepa kitendo hiki hukumbana na kejeli na dharau na huitwa 'msungo.' Jina hili 'msungo' linachukiwa hasa na kina baba katika jamii ya Tumaini. Mzazi wa msichana aliyekwepa tendo hili hufedheheka naye huonekana kumdhalilisha bintiye.

Tohara ni tendo linalodhihirisha unyama kwa vijana wa kike. Unyama huu hudhihirishwa katika riwaya ya *Tumaini.* Vijana wa kike wanaathiriwa na kulazimishwa katika tendo hili bila hiari yao. Mbali na kuwa kupashwa tohara huwa ni kigezo cha kulazimishwa katika ndoa, pia huwa ni chanzo cha kuwakatisha vijana wa kike masomo yao. Wasichana wengi katika jamii ya Tumaini wanajikuta katika tendo hili kwa kulazimishwa. Katika uk 14, Tumaini anasema kuwa ;

> *''Wasichana wengi mle kijijini, walipashwa tohara hata ingawa serikali ilikataza kitendo cha ukeketaji wa watoto wa kike. Tumaini alielewa pia kwamba idadi kubwa ya wale waliotahiriwa ililazimishwa kuolewa mara moja.''*

Tumaini anawaonea dada zake huruma wakati anapokumbuka mambo kuhusu tohara ya lazima. Mawazo kuhusu tohara yalimtia hofu kiasi cha kufanya uamuzi wa kukimbilia mahali pa kujistiri. Aliwaza kuhusu dada zake na kujisaili kama wataweza kujitetea wakati watakapokabiliwa na tatizo kama lake. Aliweza kuona hatua aliyoichukua kama itakuwa kichocheo cha babake kughairi kuwapeleka shuleni na kuwapasha tohara kisha kuwaoza kwa waume ambao dada zake hawakuwafahamu.

Utamaduni huu wa kupasha tohara vijana wa kike ulikuwa umemganda Bi Amina hata baada ya Tumaini kukimbilia usalama kwa Bi Halima, inambidi amfuate Tumaini na kumkemea;

> *"umetorokea huku ili usitahiriwe siyo? Unafikiri huwezi kunyanyuliwa*
> *juu hadi nyumbani? Unadhani kuna usalama hapa? Mnh! Hiyo ni starehe ya mbwa kukalia mkia wake. "wewe ukitaka usalama ujilete nyumbani taratibu, ukamilishe ada inayostahili. ( uk 32) m.w*

Imefahamika kuwa pindi tu baada ya tohara, vijana hawa waliozwa kwa lazima na kukatiziwa masomo yao. Masumbuko anamchukulia bintiye, Tumaini kama 'msungo.' Hakutaka kubadilisha mawazo yake kuhusu msimamo wake uliobobea katika tamaduni kuhusu tohara.

Licha ya mwanyumba na shemejiye kumtembelea na kumshauri kuhusu wazo la kumpasha tohara bintiye Tumaini, anadhihirisha msimamo wake thabiti kwa kusema;

> *"Haya! nieleze mlilolijia, lakini kama ni juu ya tohara ya Tumaini hiyo ni lazima. La sivyo nyumba hii aionee paa." (uk 39) (msisitizo wetu).*

Masumbuko alipokosa mafanikio ya kumpasha tohara kijana Tumaini, alingilia binti zake, yaani Mashaka na Rehema. Bi Halima anasikika akisema baada ya Idi nduguye Tumaini kutumwa kuwafahamisha na kuwaalika kufika nyumbani kuhudhuria tohara ya binti hawa mapacha. Bi Halima anasema;

> *"Salaala!" mzeee Masumbuko hajapata funzo baada ya tafrani za Tumani, ataka kuwatahiri mapacha wale kisha awaoze!"*

Vijana hawa wa kike wameonewa na kudhulumiwa na baba yao ambaye anaonekana kuwa na taasubi ya kiume. Hii ni mojawapo ya mifumo ya kudhalilisha na kumkandamiza kijana wa kike katika riwaya ya *Tumaini*. Masumbuko na vijana wa kiume wanamshutumu na kumkemea Tumaini. Wanamshutumu kwa kugomea desturi hii ambayo ilistahili kutekelezwa kwa kila msichana katika jamii hii yao. Bi Halima mtetezi na mkombozi wa vijana wa kike anampongeza Tumaini kwa kugomea desturi hii ya tohara. Msimamo na imani ya Bi Halima umedhirika kuhusu tendo hili la tohara, anapomtembelea Masumbuko na kumshauri akisema;

> *"Siku hizi hakuna mtoto wa kike anayekubali kupashwa tohara, wengine hata wamewachukulia wazazi wao hatua za kisheria kuhusu jambo hili, wewe unayaona haya lakini unaamua kuishi katika dahari za kale."* (uk 40).

Imebainikia kwamba Mzee Masumbuko bado anashikilia taasubi kandamizi za ubabedume zinazoongozwa na tamaduni kuhusu tohara kwa vijana wa kike (tafsiri yetu)

Itikadi, mila na desturi kandamizi anayoshikilia Masumbuko ni tukio linalodhihirisha kuwa ni mmoja wa washika dau la nguzo za ubabedume. Misingi hii ya ubabedume ya kudhulumu kijana na kike imedhihirika wakati Masumbuko anaposema;

> *"Tumaini aliasi mila za kikwetu na kakimbilia kwa mamae mdogo. Kilichobaki ni kumpasha tohara na kumwoza ili nisafishe jina la ukoo wangu……." (uk 63)*

Suala hili la ukeketaji wa vijana wa kike limeshugulikiwa na Naradon L. na Chant S (1989) katika *Women in the Third world* ambapo anaangazia maeneo ya Afrika Kaskazini na Mashariki ya kati. Anadai kwamba ukeketaji wa wanawake hukisiwa kupunguza hisia zao hivyo

kuhakikisha uadilifu katika ndoa na pia kunadaiwa kuwa ni sawa kiafya, kistadi na kimsingi katika tendo la kuhitimu kuingia ukomavu. Akimnukuu Mclean (1985:7) anasema;

> *"Ingawa lengo la kupashwa tohara laweza kuwa ni la kupunguza hamu ya mwanamke, ukweli kutokana na maoni ya matibabu ni kuwa ukeketaji wa kinembe hupunguza uiitikiaji lakini hauondoi haja.*

Tohara yenyewe inadhihirika katika kumdhulumu na kumkandamiza kijana wa kike. Bi Amina naye amefungika katika imani za mila na tamaduni kandamizi kwa kuchangia kumdhulumu kijana wa kike. Masumbuko hana subira kwa bintiye afaaye kukamilisha masomo ya msingi kabla apashwe tohara. Haya yanadhihirika pale Tumaini anapojitetea lakini mamake hampi muda wa kujitetea anaposema;

> "*Kwa kuwa sasa wewe umefika umri wa kuingizwa unyagoni, hatuna budi kuyatenda yale yanayopaswa kutendwa. Hii ni mila yetu tangu azali" Mama alimjibu. ( uk 45) (msisitizo wetu).*

Baada ya kujiuliza hivi, mawazo mengi yalimpitia kwa kasi akilini mwake na kujiuliza kama ni yeye, na alipojitazama kioni alijiona kuwa hakuwa na sura yake aliyoizoea. Alilengwalengwa na machozi na kisha yakaanza kumpukutika. Inabainika kwamba mawazo aliyokuwa nayo Tumaini yalitokana na dhuluma za babake. Mateso yaliyosababisha kuathirika kwake kimawazo na kimwili kwa jumla yalitokana na lengo la kupashwa tohara.

Katika riwaya ya *Tumaini*, ukurasa 30, Tumaini aliyaona maisha kuwa magumu. Alisema kuwa Mungu tu ndiye angeweza kukitegua kitendawili cha maisha yake, hali inayomfanya kuingiwa na mawazo nafsini. Alizama kwenye mawazo kiasi kwamba alizinduliwa na shangaziye kutoka kwenye mawazo aliyoyazamia. Hali hii ilichangiwa na hali kandamizi ya kiume ya babake, kiasi cha kujiona kama kiumbe duni kisicho na maana. Inaelezwa kuwa;

> *"Unyama ambao Majuto alitaka kumtendea ulimfanya kuhisi kama kiumbe asiye na maana kabisa. Nyavu za mawazo zilimzonga akilini* (uk 30).

Hali hii kandamizi ya kiume inayomtia Tumaini katika lindi la kuwaza na kumwaathiri nafsiye imesababishwa na babake, Chifu Andrea na Majuto ambao wote wanaendeleza taasubi kandamizi dhidi ya vijana wa kike.

Katika *Tumaini*, kijana Tumaini anaposhinikizwa na kulazimishwa na Masumbuko kupashwa tohara, kutamatishiwa masomo na kutafutiwa mchumba, alijaribu kujitetea kuhusu tarajio lake. Tukio hili limezua athari ya kufanya uamuzi wa kukata tamaa na kuhama kwao kabisa hata hakutaka kughairi kuangalia nyuma, kwani kungemkumbusha dhuluma alizokuwa amepitia. Anasema;

> *Kifurushi hicho kilikuwa ndicho miliki yake pekee. Hakuwa na jingine wala mwenziwe, ila Mungu wake. Alipiga hatua moja kwa moja bila kugeuka nyuma. Hakutaka kutazama nyuma kwani nyumba yao ilimkumbusha mengi machungu (uk 1) ( msisitizo wetu).*

Tumaini amedhihirisha kukata tamaa anaposema kuwa hakuwa na jingine wala mwenziwe ila Mungu wake. Ikumbukwe kwamba jamii hii yake haimpi kijana yeyote nafasi ya kujielezea kwani ilikuwa ikiendelezwa na mifumo ya ubabedume iliyokuwa na misingi katika mila na itikadi zenye kumkandamiza kijana wa kike.

Nadharia ya Ufeministi Huru iliyotumika katika kazi hii inaafikiana na mawazo ya Tumaini katika *Tumaini* (2006). Tumaini ameamua kukaidi matakwa ya tamaduni zake na kufanya uamuzi wa kuhama kwao chanzo ikiwa ni dhuluma kandamizi ya kumnyimwa uhuru wake. Maamuzi ya kijana huyu yamedhihirisha kwamba vijana wamejitahidi na kupiga hatua kijasiri wanapokataa kandamizi za kiume za kina baba zao. Nadharia ya Ufeministi Huru ina msimamo kuwa mwanamke wa Kiafrika ana uwezo wa kujikomboa na kujiondolea dhuluma kandamizi anazotendewa na mwanaume.

Tumaini anaona jambo la tohara kwa vijana wa kike kuwani tendo lenye imani ya ushirika ambao hauna maana na ni tamaduni iliyopitwa na wakati. Aidha vijana wengine wa kike wamedhihirisha imani ya kukataa tohara, hali inayojitokeza katika ukurasa wa 43 pale Tumaini anasema kuwa alishuhudia baadhi ya wasichana wakikataa tohara hiyo na kuwashtaki wazazi wao kwa serikali. Kwa hivyo alijiona kuwa hakuwa pekee katika migongano na mikinzano ya kuikataa mila hiyo. Hali hii ya Tumaini na baadhi ya msimamo wa vijana wa kike imelingana na Nadharia ya Ufeministi Huru iliyoongoza utafiti huu, inapodhihirika kuwa vijana hao wanapigania uhuru wa kujikomboa kutokana na dhuluma zinazowakumba. Vijana wengine kama Zena, Rehema na Mashaka wanakatiziwa masomo yao pindi tu wanapopashwa tohara na kuozwa. Maisha yao katika masomo yaliathirika licha ya juhudi na ufanisi wao katika kupita

mitihani kama vile Mashaka aliyepita vyema lakini babake aliyeongozwa na taasubi ya ubabedume anamkatizia masomo na kumuoza.

## 3.4 Kuozwa Kwa Lazima

Tukio hili la kuozwa bila hiari kwa wasichana liliwadunisha katika nafsi zao na kuhisi kujionea kama watu duni. Tukio hili linachangia ukosefu wa ndoa zilizokuwa za kudumu. Kuozwa kwa lazima au kufanyiwa uamuzi wa kuchaguliwa mume kwa vijana wa kike ni tendo la kuwadhulumu na kuwadunisha katika maisha yao. Vijana wa kike wanajiona kuwa watu waliokandamizwa, wasio na uhuru wa kujifanyia uamuzi katika kujichagulia mpenzi. Licha ya hayo vigezo vinavyotumika katika kuwateulia wanaume ambao huwakandamiza. Wazazi wa kiume huwaona vijana wa kike kama bidhaa za kuwaletea mali hasa wanapoingiwa na tamaa ya kutajirika.

Tukio la kuwaoza vijana wa kike bila hiari linadhihirika pale Mashaka analazimishwa kuozwa kwa Mzee wa rika ya babake. Anakumbana na athari ya kuathirika Kisaikolojia anapokumbana na mateso yenye msingi ya ubabedume. Ndoa yake ilimsababishia mashaka, madhara makubwa ya kimwili na kiakili ukurasa 122. Imedhihirika kuwa Mzee huyo aliyemuoa alimtesa Mashaka kiasi cha kuwa hawakuwa wanasikilizana kabisa, kwani inasemekana kuwa;

> *"Yale yaliyomfurahisha Mashaka, mumewe aliyaona ni ya kitoto tu. Hakuacha kumsononesha kimawazo hasa pale alipomsuta kwa kosa lolote dogo alilofanya. Kwa sababu ya madhila haya ufyefye ulimvaa Mashaka, vibega vikainuka juu kama vya ndege."* (uk 123).

Udhalimu anaotendewa kijana wa kike katika ndoa yake changa ni ule wa ukosefu wa kufikia lengo la ndoa kwa kuishi kwa pamoja na kuwajibikiwa kikamilifu. Wanaume wanadhihirisha mila na itikadi katika kutawala ndoa hizi bila kuwashirikisha washika dau wenzao ambao ni wanawake. Matatizo mengi yanazuka katika ndoa hizi kwani vijana wa kike waliolewa hawafaidiki kutokana na wanaoishi nao kama waume wao, tukio linaloofanya ndoa zao kukosa ladha.

Mifumo ya kiume huchukulia kuwa mwanamume huwa mwenye mamlaka yote na vile vile huweza kutoa maamuzi atakavyo kama vile kumtaliki mkewe wakati wowote bila kuulizwa sababu. Ndoa zenye misingi ya kulazimishwa zinadhihirika kutodumu kwani zinabainika

kufurahisha upande mmoja ambao ni wa kiume ilhali kumhuzunisha mwanamke. Kwa sababu mwanamke hakuhusishwa kikamilifu katika maamuzi ya ndoa.

Ndoa kati ya Zena na Mzee Chumo ni mojawapo ya ndoa zinazosambaratika kwani Zena alitawishwa, akaingizwa unyagoni na kufunzwa kunga za utu uzima na kisha kuozwa baada ya kuachishwa masomo. Taasubi ya ubabedume inadhihirisha kuwa;

> *Hapo ndipo wangealikwa wazazi, jamaa na marafiki kushuhudia ndoa hiyo isiyo na misingi ya mapenzi kwa wawili wapendanao (uk 50) msisitizo wetu.*

Ndoa kama hii ya Chumo na Zena ni ya kusambaratika kwani haina mizizi ya mapenzi bali ni ya kumsukumizia kijana wa kike, inavyodhihirika kuwa;

> *Hata kama hakufurahia yote yale kutokana na lazima za wazazi kuolewa angelazimika kutia tabasamu bandia ili mradi afurahishe umati (uk 50) msisitizo wetu.*

Nadharia ya Ufeministi huru inaafikiana na hali hii ya kutochangamkia ndoa kandamizi kama hizi. Zena anadhihirisha kutoichangamkia ndoa yake kwani anapigania uhuru wa vijana katika kujikomboa kutoka kwa kandamizi dhalimu.

Katika *Tumaini* (2006), Mashaka ameishi maisha magumu na yaliyosheheni mateso kutoka kwa mumewe Mzee Lusimbo. Inathibitika kuwa Mashaka aliozwa kwa lazima kwa Lusimbo kama mke wa tatu. Lusimbo kutokana na umri mkubwa alimtesa Mashaka na kumsononesha kimawazo na kumsuta kwa kosa dogo alilofanya. Alizaa watoto watatu katika umri mdogo. Mashaka alibughudhiwa na wakewenza naye Lusimbo anaamua kuhama na kumtembelea kwa nadra tu. Mateso haya aliyoyapitia yalimwathiri kimwili. Tukio hili linadhihirisha athari inayowakumba vijana wa kike ya kukosa thamana katika ndoa. Imani ya Mashaka imepotea kwani anajiona kama mtumwa wa kiakili, kiroho na hata kimwili. Hali hii ya mateso katika ndoa inadhihirisha kuwa ndoa isiyo na mapenzi haiwezi kudumu kwani ni muhimu mke na mume kuishi pamoja na bali si mmoja kudhulumiwa huku mwenzake akifurahia. Ndoa yenye athari hasi kwa wanaohusika huwa ni vigumu kudumu.

Tendo la ndoa za mapema na hasa za kulazimishiwa zimekithiri katika jamii ya Tumaini. Jamii hii imeongozwa na taasubi ya ubabeume katika *Tumaini* (2006:15) tendo hili ni bayana na limedhihirika kuwa,

*"Tumaini alielewa pia kwamba idadi kubwa ya wale waliotahiriwa, ililazimishwa kuolewa mara moja. Ndoa za mapema na za lazima katika jamii lilikuwa jambo la kawaida. Wasichana wadogo waliozwa kwa waume wasiowajua na mipango yote ilitekelezwa na wazazi wao wa kiume"*

Tendo la ndoa za lazima na za umri mdogo ni dhihirisho kuwa vijana wa kike wamedhulumiwa na kukandamizwa katika jamii ya Tumaini. Katika jamii hii ya Tumaini, na imethibitika kuwa Masumbuko alikuwa na hangaiko kwa kudai kuvunjiwa heshima kutokana na hali ya Tumaini kukimbilia usalama kwa Bi Halima. Masumbuko anashauriana na rafikiye wa kibiashara Mabrui Suleimani, wote wawili wanapatana na kukubaliana kuwa kijana wa kiume wa Suleimani alete posa ya kuoa Tumaini. Tukio hili lilikuwa la kisiri kwa Bi Amina na Tumaini na hata kwa waposaji ambao hawakuwa wanafahamu kuwa Tumaini alikuwa mwanafunzi wa shule ya msingi. Haya yanadhihirika kwa wageni walioleta posa walipoelezewa na Yusufu, mjombake Tumaini kuwa;

*"Yaani Masumbuko unawaleta wageni kutoka huko- sijui wapi- Mambrui-*
*kumposa mtoto wetu mchanga anayesoma shule? Hii ni aibu gani?*
*(uk 61).*

Tamaduni yenye misingi katika mila na itikadi pamoja na taasubi ya ubabedume imemwongoza na kumtawala Masumbuko. Hakutaka kulegeza uamuzi alioufanya anapowakabili waliokuwa katika kikao chenye njama ya kumwoza Tumaini bila hiari yake na wala hata jamaa yake kufahamu ila tu Mzee Masumbuko. Yote haya yamedhihirika anaposema kuwa;

*"Kilichobaki ni kumwoza ili nisafishe jina la ukoo wangu-"*
*Mimi nimekata shauri kumwoza binti yangu (msisitizo wetu) inadhihirika kuwa*
*ana msimamo usiobadilika kuhusu ndoa ya vijana wa kike".*

Ukweli uliopo ni kwamba tamaduni huelekeza majukumu yake kupitia kwa mila zikihusiana na mtazamo wa ubabedume kuwakandamiza vijana wa kike katika jamii ya Tumaini. Mfano bayana unadhihirika wakati, Zena mwenye rika sawa na Tumaini anapokabiliwa na tendo dhalimu la kuozwa kwa lazima.

*"Tumaini alikumbuka jinsi vijana hao makatili walivyombeba Zena juu*
*juu na kumpeleka Mzee Chumo ili akawe mke wake wa nne.....*
*Lilomshtua na kumshangaza Tumaini ni jinsi wapita njia*
*Walivyokataa kumsaidia Zena... Wengi wao waliona tukio hilo kama jambo la kawaida*
*tu(uk 49).*

Hata ingawa mila zimebadilika bado zingali zinaenziwa, kutokana na vile wale wapita njia hawakuchukua hatua kumwauni Zena. Tukio hili linadhirisha hali ya kutokuwa na haraka ya kubadilisha mawazo kuwapa fursa vijana wa kike kujifanyia uamuzi wa kuwachagua wachumba wa matakwa yao. Lakini zaidi imedhihirisha ishara ya udhalimu wa ubabedume. Vijana wa kike wanadhulumiwa katika umri wao mdogo Imebainika kuwa pindi tu mzazi wa kiume anapokata shauri hufanya uamuzi bila kuangalia umri wa bintiye. Bi Halima anasema;

*"Nionavyo mimi ni kwamba Masumbuko amekwisha kuamua*
*kumtafutia Tumaini mchumba, mwanangu huyu mdogo mwenye umri*
*wa mika kumi na minne tu aolewe? Kwa nini akatizwe masomo ilhali ana*
*ari ya kusoma? Kwa nini amsukume kwenye ndoa ya mapema? (uk 34).*

Maswali haya mengi yalimsumbua Bi Amina anayemwelewa bintiye na hata kuona kuwa asasi ya ndoa inatumika kumkandamiza mwanawe. Hata Tumaini anakubaliana na maswali haya anaposema,

*"Alikwisha kuona wasichana wa hirimu yake wakiozwa kwa nguvu*
*Pale kijijini mwao na kukatizwa masomo yao" (uk 43).*

Mfumo huu wa dhuluma wa kuwaoza vijana wa kike bila hiari umechangamkiwa na jinsia ya kiume kwa jumla yaani vijana wa kiume na hata wazee wa kiume. Masumbuko anasikika akisema

*"-utaolewa upende usipende". (uk 43)*

Naye Idi anamwambia dadake Tumaini kuwa;

*"Aaaa kuolewa sio siri. Tunasubiri kusherehekea...".*

Hili limeonekana ni tendo limechangamkiwa na kufurahiwa na vijana wa kiume. Ndoa ya kike inapofanywa kwa msingi yoyote ile iwe ni kulazimishwa au kuolewa bila hiari. Kuwaoza wasichana kwa wanaume wazee na bila hairi yao ni aina ya udhalimu kwa sababu wasichana hao huishi maisha yaliyodhibitiwa na wanaume ambao wamemithilishwa na miungu yao ya kuabudiwa. Vijana wengi walioolewa jinsi hii wameishi maisha duni yasiyo na utulivu ambayo yameongozwa na mtu mwingine na hana mamlaka juu ya maisha yake mwenyewe. Haya yamedhihirika wakati;

*"Mzee Masumbuko alipokea mahari ya Mashaka, akamwoza kwa*
*Lazima kwa mzee Lusimbo, kama mke wa tatu. Ndoa hiyo ilimsababishia*
*Mashaka madhara makubwa ya kimwili na kiakili. Pia mzee huyo*

*alikuwa na umri mkubwa sawa na babake Mashaka.*

*Yaliyomfurahisha Mashaka, mumewe aliyaona ni ya kitoto tu".*

Hali kama hii kandamizi itafikia kikomo kama vijana wote wa kike katika jamii ya Tumaini wangeamua kuvunja minyoyoro ya ukandamizi ya kulazimishiwa ndoa kwa kufuata mkondo ambao Tumaini aliuchukua, anaposema;

*" Ndoa haishurutishwi wala hairidhishi ikiwa haitaambuliwi na wawili Wapendanao. Ndoa ya kupangiwa na wazazi hairidhishi kwani kigezo cha mapenzi hakifikiriki hapa" (uk 129) (msisitizo wetu).*

## 3.5 Kubakwa na kupachikwa mimba

Dhuluma ya ubakaji wa vijana wa kike iliendelezwa na hata wahuni katika kijiji cha Mkwajumi. Haya yamedhihirika pale Tumaini anaposema kuwa alikwisha sikia mara nyingi kuwa wasichana wamewahi kubakwa katika mtaa huo na wahuni, hasa pale walipodiriki kutembea peke yao. Hali hii ni ya kuwadhulumu vijana wa kike.

Chifu Andrea ni kiongozi anayeongozwa na tamaa ya kibinafsi inayomzinikiza katika kuwatendea vitendo viovu vijana wa kike. Kijana wake wa kiume, Majuto, naye alikithiri na kumpita babake katika vitendo viovu na njama ya ubakaji dhidi ya mabinti za watu.

Chifu Andrea na Majuto, kijana wake, wanajaribu njama ya kumbaka Tumaini mtawaliwa. Kama haingekuwa ujasiri wa Tumaini wangefanikiwa kutekeleza maovu yao ya kushibisha tamaa zao za kumdhulumu na kumkandamiza kijana Tumaini na mabinti wengine.Imeelezewa kuwa Majuto;

*"Alikuwa farisi katika wizi na ubakaji wa mabinti za watu. Aghalabu wazazi wa vijana hao wa kike walipomletea chifu mashtaka kuhusu unyanyasaji wa Majuto, aliwapiga pande. Walipoamua kupeleka mashtaka mahakamani chifu aliyazima kwa kutoa mlungula" (uk 54)*

Kutokana na tendo la chifu kuyakwepa malalamizi na kutoa mlungula kuzima mashtaka ni dhihirisho la kutojali dhuluma dhidi ya vijana wa kike. Njama ya Majuto kutaka kumbaka Tumaini imedhihirika kutokana na usemi kuwa;

*"Kwa ghafla alimshika Tumaini kiuno na kujaribu kumbwaga chini. Tumaini alikuwa sasa yumo hatarini. Alimpiga Majuto kwa kiko cha mkono katika sehemu ya kinena kwa nguvu zake zote. Majuto alipiga kelele kwa maumivu....(uk 71).*

Hali ya kijana wa kike kukosa watetezi na wakombozi ilichangia vitendo dhalimu kwao. Jamii ya Tumaini inamwona kijana wa kike kama chombo cha kutumbuiza vijana wa kiume na wanaume kama vile imejitokeza katika njama za chifu Andrea kuwa;

> *"Lakini kwa ghafla, chifu alimrukia kama kozi na kujaribu kumbusu, huku akihema na kumpapasa mwili mzima. Tumaini alitapatapa kama mfa maji, alijaribu kuimamanua mikono ya chifu iliyomshika kifuani kwa nguvu (uk 91) (msisitizo wetu).*

Vitendo hivi vya chifu Andrea na Majuto vina misingi ya ubabedume ambayo inakuza kijana wa kiume na mwanamume kuwa na uwezo mkuu dhidi ya jinsia ya kike iliyo changa.

*Katika Tumaini* (2006:54), Chifu Andrea amedhalilisha vijana wa kike iwapo wangemtaja kama mhusika wa mimba alizowapachika. Hii ni dhuluma inayoongozwa na taasubi ya ubabedume. Vijana wa kike wamedhulumiwa na kutishwa.Imebainika kuwa;

> *"Baadhi ya wasichana hao aliowapachikwa mimba wengine aliwafadhili*
> *ili kuharibu mimba hizo hali wengine aliwatishia maisha yao iwapo*
> *wangemtaja yeye kama mhusika".*

Rehema katika Tumaini (2006) ni kijana wa kike mdogo aliyezalishwa watoto wawili licha ya umri wake mdogo, baada ya kuozwa na kuachishwa shule.inaelezewa kuwa;

> *"Rehema sasa alikuwa na watoto wawili akiwa bado ana umri mdogo.*
> *Je baada ya miaka kumi, angekuwa na watoto wangapi? (uk 114).*

Hali hii ya kujifungua watoto wegi na katika umri mdogo imesabishwa na kuchangiwa na imani na mila kuwa mwanamke pindi anapoolewa kazi yake ni kumzalia mwanaume watoto. Mume haangalii aghalabu hali yake ya kiuchumi na hupuuza hali ya kiafya ya mwanamke. Tumaini anabainisha hili kwa kusema;

> *"Swali kama hili na mengineyo yalimtia hofu, hasa alipoelewa kuwa*
> *mumewe Rehema hakuwa na uwezo wa kumkimu yeye na wanawe." (uk 114)*

## 3.6 Vitisho

*Katika Tumaini* (2006:27) vitisho vimedhihirika wakati ambapo Idi amefika makazi pa Mzee Shabani na kumkuta Tumaini na kumwelezea yaliyokuwa yakimsubiri. Idi anasema;

> *"Eeehe! Tuma, leo utakiona, baba amekasirika walahi sijamuona*
> *Kukasirika vile! Amesema nikikuona nikuambie............"*

Vitisho vya babake Tumaini vya kutaka kumpasha Tumaini tohara vilisababisha Tumaini kufikiria kukimbilia usalama katika jamii ya Shabani. Lengo la Tumaini lilikuwa aweze

kuendelea na masomo yake. Anapotishwa anaamua kujikomboa kwa kuchukua hatua ya kuhamia kwa Bi Halima. Naye Bi Halima anamhakikisha Tumaini kuwa;

*"Mimi mamako mdogo nakuhakikishia usalama.*

*Kwa hivyo usihofu vitisho vya babako. Hayo ni maji moto, hayachomi nyumba." (uk 30).*

Vitisho hivi vilimnyima Tumaini utulivu katika maisha yake na ndoto yake ya kuyaendeleza masomo yake, Yusufu anamwambia Masumbuko;

*"Vitisho vyako ndivyo vilivyomtoa Tuma hapa" (uk 40).*

Kwa upande mwingine chifu Andrea aliwatishia wasichana aliowapachika mimba. Thibitisho la vile vijana wa kike wanavyodhalilishwa na kudhulumiwa na wanaume katika jamii ya Tumaini. Chifu Andrea aliwatishia maisha yao iwapo wangelimtaja yeye kama mhusika wa mimba alizowapachika. Kando na kutendewa uovu, vijana wa kike hutishwa ili kuwaogofya kuchukua hatua dhidi ya dhuluma wanazokumbana nazo.

Mwalimu Majaaliwa naye anadhihirisha vitisho kwa vijana wa kike kwa kutoa amri ya kutothubutu kuchagua masomo ya Sayansi. Tukio hili linadhirika katika harakati za kujaza fomu za kujiunga na vyuo vikuu. Mwalimu alishikilia msimamo wake kwa vijana wa kike na kuwatishia kutothubutu kujagua masomo na hakutaka kuwapa nafasi kamwe. Katika riwaya ya *Tumaini*, mateso yalizua athari katika nafsia na akili ya Tumaini kiasi cha kwamba anatishika kuona nyumbani kwao kama makao pa mateso. Inadhihirika kuwa;

> *"Mikononi, alikuwa kasitiri kifurushi cha nguo zake pamoja na vitabu vyake vya shule. Kifurushi hicho kilikuwa ndicho miliki yake pekee. Hakuwa na jingine wala mwenziwe , ila Mungu wake. Hakutaka kutazama nyuma kwani nyumba yao ilimkumbusha mengi machungu (uk 1)( msisitizo wetu*)

Vitisho vinavyowakumba vijana wa kike vinazua athari katika maisha yao, hali hii inawafanya kuofya maisha yao nakukosa malezi na miongozo kutokakwa jamii yao hasa wazazii wao.Kutokana na hofu Tumaini anatengwa na malezi ya wazazi wake.

## 3.7 Matusi

Katika riwaya ya *Tumaini* (2006), Tumaini anachukizwa na matusi ya vijana wa kiume waliyombandika anaposema kuwa;

*Hakustahili kufananishwa na twiga, mnyama aliye na shingo ndefu iliyositiri kichwa kidogo. Au kufananishwa na kitumbua ambacho ni chakula kinacholiwa tu na watu* (uk 44-46) (msisitizo wetu).

Maneno ambayo hakustahili kufananishwa nayo yanaonyesha kuwa maneno yaliyotumika ni ya kumvunjia heshima yake. Kejeli na mifananisho hii ilitumiwa na vijana wa kiume, hali hii ya ubabedume imeendelezwa na hata vijana wadogo wa kiume kama vile Idi anayewatusi vijana wa kike. Matusi haya yanadhihirika pale Tumaini anaposema kuwa; "Alielewa kuwa tabia ya Idi ni kielelezo halisi cha malezi ya babake.

*Kijana huyo mdogo wa kiume tayari alijua kuwa wanawake ni vifaa tu vya utumishi nyumbani mwao." (uk 29) (msisitizo wetu).*

Maneno 'vifaa tu vya utumishi' yanapotumika dhidi ya Tumaini licha ya kudhihirisha dharau pia ni matusi kwa vijana wa kike. Maneno haya ni ya kuwatukana vijana wa kike kwani wao si vifaa. Mbona waonwe kama vifaa ilhali wana usawa na wale wa kiume.

Matuzi yanayowakumba vijana wa kike yanazua athari katika maisha yao. Kijana Tumaini anajiona duni na kuchukia jinsia yake ya kike. Jina kama vile 'msungo', bidhaa ya uwekezaji, watumishi wa nyumbani, kitumbua na twiga ni maneno yaliyomdhalilisha kiasi cha kuchukia nafsi yake. Matusi yanazua changamoto katika maisha ya vijana wa kike, wanapokumbwa na matusi wao hujitazama kama viumbe duni visivyo na thamana katika jamii yao.

## 3.8 Kubaguliwa na Kunyimwa Uhuru

Mzee Masumbuko aliendeleza dhuluma ya kuwabagua vijana wake wote wa kike na kuwanyima uhuru wa kuendelea na masomo. Shinikizo lake la kutaka Tumaini kupashwa tohara au kudai kuwa hana pesa za kumsomesha Tumiani lilijangia kutorokea kwake kwa Bi. Halima. Hata mabinti wengine kama Mashaka na Rehema waliozwa tu pindi walipopashwa tohara. Idi ndugu yao wa kiume aliendelea na masomo ilhali dadazake wakikatizwa masomo yao. Masumbuko alidhihirisha misimamo ya kumpendelea kijana wa kiume, Idi huku akiwadhalilisha na kuwabagua wale mwenzake wa kike kama Tumaini, Mashaka na Rehema.

Katika jamii ya Tumaini vilevile ubaguzi wa kumnyima uhuru unadhihirika kupitia maneno ya bi Halima katika ukurasa wa 32 anasema;

*"Mbona mnamlazimisha Tuma kutenda asiyotaka? Huku ni kumnyima uhuru wake wa kibinafsi. (msisitizo wetu)."*

Kauli ya kubaguliwa kwa vijana wa kike inaendelezwa na kijana wa kiume mdogo. Idi aliyekuwa anaongozwa na mifumo yenye misingi katika mila na itikadi za tamaduni. Imedhihirika kuwa vijana wa kike wana jukumu la kuolewa ili wazazi wapate pesa za kumsomesha kijana wa kiume. Anapokanywa na dadake, babake anachangia katika kutilia chumvi mawazo ya ukasumba wa Idi kwa kumkanya vikali Tumaini.

Kutokana na vitimbi vya babake, kijana huyu mdogo aliwaona dada zake kama watumishi tu pale nyumbani. Alithibitisha haya kutokana na kauli kali alizoelekeza kwa dada zake kuwa wao ni bidhaa za uwekezaji tu pale nyumbani. Walisubiri tu kuolewa ili wazazi wapate pesa za kumsomesha. (uk 14) (msisitizo wetu).

Matendo ya chifu Andrea dhidi ya vijana wa kike yalidhihirisha kuwadhulumu na kuwadhalilisha kwa kuwanyima uhuru wao na kuwabagua dhidi ya mwenzao wa kiume. Inadhihirika katika ukurasa wa 53 kuhusu majuto kuwa,

> *"Alikuwa farisi katika wizi na ubakaji wa mabinti za watu. Aghalabu wazazi wa vijana hao wa kike walipomletea chifu mashtaka kuhusu unyanyasaji wa majuto, aliwapiga pande. Baadhi ya wazazi hao walipoamua kupeleka mashtaka yao mahakamani, chifu huyo aliyazima kwa kutoa mlungula kwa wakili na hata mahakimu ili watupilie mbali kesi hizo. Hali hii inambagua kijana wa kike na kumpendelea yule wa kiume.*

Vijana wa kike wamebaguliwa masomoni hata wakati wanapokuwa na juhudi za kutaka kujiendeleza kimasomo. Wamekumbana na vizuizi vya kunyimwa uhuru na kubaguliwa. Tumaini katika ukurasa wa 21 anasema;

> *"Alitamani sana kuendelea na masomo yake ili aweze kutambua vipawa vyake, lakini mzazi wake alitaka kumwekea vizuizi ili kuzififisha juhudi zake kwa upande mwingine. Majuto hakuwa na pingamizi zozote zilizomkabili bali yeye mwenyewe ndiye aliyekuwa kizuizi dhidi ya masomo yake".*

Chifu Andrea na Masumbuko wanashiriki katika njama ya kumnyima Tumaini uhuru wa kusoma. Wamembagua kwa kumwondoa kutoka orodha ya wanafunzi waliokuwa wametolewa katika orodha ya kufadhiliwa na kusalia wavulana tu. Orodha hii inathibitika kwake inaposomwa na chifu, Tumaini akiwa nyuma ya ofisi ya D.O na kubainika wazi katika ukurasa wa 101 anaposema,

> *"Wote waliotajwa ni wale wavulana wanne tu waliofaulu mtihani pamoja naye".*

Mwalimu mkuu wa shule ya upili Bwana Majaaliwa anaendeleza dhuluma kandamizi dhidi ya vijana wa kike katika shule anayoiongoza. Anawanyima wasichana uhuru wa kuchagua masomo wanayopenda katika harakati ya kujaza fomu za maombi ya kujiunga na vyuo vya kitaifa. Katika riwaya ya Tumaini wakati mwalimu anaposema katika ukurasa 115;

> *"Nimesema masomo ya Sayansi yasijazwe na nyie wasichana na ni vigumu sana kufuzu katika masomo haya. Kwanza ni wasichana wangapi ambao umesikia hufuzu udaktari chuo kikuu enh? Wewe unataka kuiletea shule yangu aibu? Mwalimu alitamka kwa hamaki ili kumvunja Tumaini moyo.*

Hata baada ya Tumaini katika ukurasa 115 kumwomba idhini ya kuchagua masomo aliyoyapendelea kwa kusema;

> *"Tafadhali mwalimu ningependa kuchukua masomo ya Sayansi ikiwa nitafaulu kuingia chuo kikuu ningependa kuwa daktari wa matibabu."*

Mwalimu mkuu hakutaka kumsikiliza kamwe. Kwani alishikilia msimamo wake kuwa masomo ya sayansi ni ya vijana wa kiume. Msimamo wa kuwa masomo ya sayansi ni ya kiume ni mojawapo ya misingi ya kumbagua kijana wa kike.

Mitazamo ya desturi na mila ya jamii ya Tumaini iliyoendelezwa na miongozo yenye mashiko katika mila na tamaduni imedhalilisha na kumbagua kijana wa kike katika jamii ya Tumaini. Hata vijana wa kiume tayari walifunzwa na itikadi na mila hizi za kumbagua kijana wa kike kutokana na mawazo kuwa msichana akielimika atakosa mume. Haya yanadhirika katika mawazo kuwa.

> *Tumaini alichukizwa na wazo la Idi aliyedhani kwamba baada ya kumaliza kidato cha nne, dadake alipaswa kuolewa. Alihisi kuwa elimu ya msichana ilitakikana kuhitimishwa baada ya kidato cha nne (uk 127).*

Jamii hii iliwafunza vijana wa kiume mle kijijini kutothamini elimu ya kijana wa kike. Jamii ilimfunza kuwa msichana hangempata mume wa kumwoa baada ya kidato cha nne kwa ajili ya umri mkubwa. Hizi zilikuwa desturi zinazoongozwa na itikadi.

Hali ya kero chungu kukaa kifuani mwa Tumaini ni thibitisho kuwa kero hilo lilikuwa limemsumbua kwa muda kimawazo na kiakili. Hili kero lilizua Tumaini kupukutikwa na machozi na kuhisi kusakamwa kooni na hata kumzuia kuongea.

Wakati mwingine mateso ya kumbagua yaliyomkumba Tumaini alizidi kuyakumbuka hata baada ya kutorokea kwa Bi. Halima. Tumaini anajikuta tu akiwaza kuhusu dhuluma za babake na kuishia kuathirika kihisia. Inadhihirika kuwa;

> *"Humo ndani, aliketi kitandani huku mawazo mengi yakimzonga. Mara alishtukia machozi ya moto yakibubujika na kufanya michirizi mashavuni mwake. Aliyaacha yamwagike bila kuyafuta kwani yangempunguzia maudhiko moyoni mwake* (uk 18).

Kijana wa kike alibaguliwa kiasi kwamba anaathirika kiakili na kuanza kuchukia jinsia yake ya usichana. Mifumo kandamizi inaathiri hali ya Kisaikolojia ya vijana wa kike kwa kiwango kikubwa. Kubaguliwa kwake kunazua hali ya kudharau hali yao ya usichana, badala ya kuenzi hali yao ya usichana. Haya yamebainika katika ukurasa wa 22 pale inaposemekana kuwa;

> *Tumaini alianza kujiuliza kwa nini kazaliwa msichana. Alianza kujichukia hasa alipokumbuka kuwa tohara aliyoitazamia pamoja na mafunzo ya unyagoni vilipaswa kuweko ili kuthibitisha kwamba yeye ni mwanamke." Tumaini alijiuliza huku nyavu za mawazo zikishindana akilini mwake.*

Kijana Tumaini anaathirika kiakili hali hii inazua matatizo ya hisiathirika Kisaikolojia Tumaini alikumbana na changamoto nyingi akilini, ikiwa ni pamoja na kutiririkwa na machozi, kuzungumzazungumza pekee vitendo vinavyomtia simanzi.

Masharti na itikadi zenye misingi katika mila zinamtia Tumaini unyamavu wa mawazo yaliyoathiri hali yake ya Kisaikolojia. Mateso haya yalisababisha kubadilika kwake kimwili. Tumaini anajisemea kimoyomoyo kuwa;

> *"Ole wako Tumaini, unajiumbua kabla hujaumbwa?*" (uk 26)

Masharti na itikadi zenye misingi katika mila zinamtia Tumaini unyamavu na mawazo yaliyoathiri hali yake ya Kififikira . Mateso haya yalisababisha kubadilika kwake kimwili.

## 3.9 Kunyanyaswa Kimapenzi

Katika *Tumaini,* Chifu Andrea kiongozi mwenyewe rika la babake Tumaini anaamua kumtaka ushirika wa kimapenzi Tumaini kwa kumletea vishawishi. Haya yanadhihirika wakati Chifu Andrea anasema;" Subiri kwanza Tumaini, hapa nimekuletea viatu vizuri sana. Hebu njoo uvijaribu kama vitakutosha".

Baada ya hali hii inabainika kuwa chifu alimsogelea na kutaka kumshika bega huku akitoa vicheko vya bandia. Hali hii inadhihirisha ukandamizi wa kuwanyanyasa vijana wa kike kimapenzi. Tumaini mwenyewe anathibitisha katika ukurasa 88 kuwa kamwe hakudhani kuwa Chifu Andrea, mwenyewe rika moja na babake, angemtaka kwa njia hiyo. Bi Halima naye kwa upande mwingine anapomshauri Bi Selina kuhusu tabia ya mumewe katika uk 93 anamwelezea kuwa alishangaa bibi huyo kujitia mtonga huku mumewe akizidi kuwanyemelea mabinti za watu.

Katika ukurasa 122 kuozwa kwa Mashaka kwa Mzee Lusimbo mwenye umri sawa na Masumbuko babake, Mashaka na tena kumwoza kama bibi wa tatu ni dhuluma kandamizi kwa vijana wa kike. Rehema dadake Mashaka naye anakumbana na dhuluma hiyo ya kuozwa kwa Mzee Shauri kama bibi mdogo. Hii ni changamoto inayowakumba na kuwadhulumu vijana wa kike kimapenzi. Kulingana na hali yao ya umri hawa vijana wa kike wanafaa kuwa na wenzao wakiwajibikia masomo. Vijana hawa wamenyimwa haki zao kwa kulazimishwa katika ndoa wakiwa wangali wadogo.

Katika riwaya ya *Tumaini* ukurasa wa 90, kijana Tumaini anateseka katika kufanya kazi ya sulubu na hata katika mazingira magumu. Tumaini amenyanyaswa kimapenzi katika makao ya chifu katika hhali ya kutafuta fedha za masurufu atakapojiunga na shule ya upili. Hali inayodhihirisha mateso kwa Tumaini, kwani babake alikuwa na uwezo wa kugharamia malipo yake yote ya shule ya upili. Masumbuko aliongozwa na uchu ya pombe na kumpuuza elimu ya bintiye.

Tumaini anateseka chini ya ukatili na uongozi wa wanaume wakatili. Masumbuko, Chifu Andrea na Majuto wanamtia mateso Tumaini. Tumaini hana fahamu ya kujinasua kutoka kwayo. Mateso haya yanamtia katika machungu mengi. Haya yanabainika anaposema;

> *"Maskini mimi.., mbona mnanitesa nami sina pa kwenda – baba hanitaki, Majuto anataka kunishika kwa nguvu – babake naye anitaka pia – jamani wuuui! Nisaidieni." (uk 51)*

Mateso ya Tumaini hayana mkombozi na hali ya mateso yalimpa kumbukizi ya machungu mengine aliyokuwa ameyatenga na kuyasahau.

Kulingana na nadharia ya Ufeministi Huru tulioitumia inafikiana na hali ya kujikomboa na kuwa huru kwa baadhi ya vijana wa kike akiwamo Tumaini. Vijana hawa kama vile Tumaini walisimama wima kujitetea na kujikomboa kabla kuathirika na dhulumaya kupachikwa mimba. Haya yanadhihirika wakati Bi. Halima anamwelezea Bi. Selina katika ukurasa wa 92 kwamba ni wasichana wengi wa kazi waliokwisha mtoroka kwa sababu ya vitimbi vya mumewe. Naye Tumaini hakusita kuhama kwa Chifu hata baada ya Bi. Selina kimsihi akae kwa muda mfupi hadi atakapopata msichana mwingine wa kumsaidia.

Idadi kubwa ya wanaume wa Kiafrika wanaongozwa na imani na itikadi zenye misingi ya ubabedume inayoshikilia kwamba mwanamke anapoolewa anafaa kujishughulisha na kazi ya nyumbani na kazi yao kubwa ni kuwazalia watoto waume. Dhuluma inayotendewa vijana wa kike imeasababisha ndoa zao kukosa lengo lake la wawili waliooana ili waishi kwa umoja. Mwanamume anamtenga mke na kutowajibikia mahitaji yake. Vijana walioolewa wanateseka pale wanapopachikwa mimba na hawashughulikiwi na waume zao wanapokumbwa na matatizo yanayohusiana na mimba walizo nazo. Katika *Tumaini* ukurasa wa 114, inadhihirika kuwa Rehema alikuwa na watoto wawili na bado alikuwa na umri mdogo. Naye Mashaka katika ukurasa wa 122 inadhihirika kuwa ana shida ya kiakili na kimwili kutokana na kudhulumiwa na mumewe aliyekuwa anaona kila wazo lake kama la kitoto. Hali ya kuona mawazo ya Mashaka kama ya kitoto ni njia moja ya kumdhulumu kijana wa kike kimapenzi na matokeo yake ni kuathirika kiakili.

## 3.10 Hitimisho

Kijana wa kike amedhulumiwa kwa kupigwa kama ishara ya kuwapa adhabu na hata nyakati nyingine kwa visingizio vya kukosa kufuata maagizo waliopewa. Kwa sababu ya uwezo wanaume walionao kutokana na misingi ya mila na tamaduni katika jamii ya Tumaini. Wanaume wana hisia kuwapigwa vijana wa kike ndio suluhisho la kumwelekeza kufuata maadili na kutii matakwa ya jamii.

Kijana wa kike anatarajiwa kuwa mnyenyekevu na mtiifu mbele ya babake na kakake mbali na umri wake hata akiwa mdogo. Hata kama matakwa ya kuumeni ni potovu sharti kijana wa kike ayafuate. Anapokosa kuyafuata hayo na kufanya hivyo huweza kuadhibiwa kwa kupigwa.

Tohara ni asasi mojawapo inayotumika kumdhulumu kijana wa kike. Vijna wa kike inawabidi kunyenyekea na kukubali kulazimishwa kutahiriwa bighairi ya umri wao mdogo hata kuepushwa

elimu ili waweze kushiriki katika shughuli hii. Wanapokataa na kukosa kushirikishwa katika tohara, hupata kejeli na kudharauliwa kwa kuitwa majina kama 'msungo' na hata kuonwa kama waasi wa maadili na wavunja mila na desturi. Wazazi huwachagulia wasichana waume na wanatarajiwa kuwakubali bila pingamizi wala kuuliza maswali kuhusu wachumba bali hutarajiwa kuwakubali kama waume.

Vijana wa kike wanakumbana na ndoa za kulazimishiwa. Katika ndoa hizi vijana wa kike hawana uamuzi wowote kuhusu uchaguzi wa wachumba wao. Wanakumbana na athari kubwa pale wanajikuta wakiozwa kwa wazee wakongwe wenye umri wa rika za baba zao. Kandamizi zaidi ni kuwa wanaozwa kama mke wa tatu au wa nne. Tukio hili la kuozwa kama mke wa tatu au wa nne linawaletea tatizo la kuteswa na wakewenza. Kwenye ndoa hizi za lazima, wanaume ndio walio na uamuzi kizihusu.

Katika sura hii tumejaribu kubainisha athari zinazoibuka kutokana na dhuluma dhidi ya wahusika vijana wa kike. Dhuluma kandamizi zenye misingi katika uongozi wa ubabedume unaojikita katika mifumo ya mila na itikadi zilizopitwa na wakati zingali zinanyanyasa kijana wa kike. Matokeo ya nguzo hizi zenye misingi ya ubabedume ina athari mbovu kwa kijana wa kike.

Imedhihirika kuwa mwanamume anachangia katika kupoteza matumaini na ari aliyonayo kijana wa kike. Jamii nayo inayafungia macho maonevu hayo ya ubabedume bila kumlaumu mwanamume. Hali hii inawapa wanaume moyo wa kumhadaa kijana wa kike kimapenzi, kumpachika mimba na kisha kumkana. Mifumo hii ni mojawapo ya taasubi kandamizi zinazozua hata vifo kwa vijana wa kike. Jamii pia inawapendelea wanaume na hata vijana wa kiume kimaadili. Mwanamke anapaswa kuwa bikira ilhali mvulana ana uhuru wa kufanya atakalo bila kutolewa lawama. Tukio hili ni tata na la kumvunjia heshima kijana wa kike anapolaumiwa kuwa amekosa maadili.

Udhalimu anaotendewa kijana wa kike humwogofya na kumfanya kuwa mnyamavu anapokabiliwa na unyanyasaji. Hana ujasiri wa kujitetea kwani huogopa adhabu atakayoipata ikiwa atajaribu kutoa pingamizi kwa mifumo ya ubabe dume. Kijana wa kike anakumbana na mateso mengi kutokana na kupigwa na kuumizwa lakini hana sauti ya kujitetea dhidi ya dhuluma hiyo. Mateso wanayokumbana nayo yanachangia katika kuathiri hali yao ya saikolojia na hata afya. Hali hii ya kuathirika kisaikolojia inawafanya waweze kuwaona vijana wa kiume kuwa watu wasiopaswa kutangamana nao.

Katika utafiti huu inabainika kwamba kutokana na dhuluma kandamizi, vijana wengi wa kike wanakumbana na athari za kupachikwa mimba katika umri wao mdogo na hasa wanapokuwa shuleni. Tukio hili linazua athari zaidi pale wanapofukuzwa na kukatiza masomo yao au kufanya vibaya masomoni. Wanapokataliwa wanalazimika kuziavya mimba hizo ambazo pia zinawaathiri kiafya na kimasomo. Vijana wa kike wenye nia masomoni wanajikuta wakitamatishiwa masomo yao kutokana na hila za wanaume kutaka kujinufaisha kutokana na mahari wanapowaoza kwa lazima.

Wengi wa vijana wa kike wanajikuta wakiozwa kwa lazima na ndoa zao zinawaathiri kimaisha wanapolazimika kuozwa kwa wanaume wanaowatesa na kuwadhulumu. Katika *Tumaini* dhuluma hizi zimeafikiana misingi ya Nadharia ya Ufeministi huru tuliyoitumia katika utafiti huu kwamba mwanamke ana uwezo wa kujitegemea na kujitetea katika kujikomboa kuwa huru. Haya yamebainika kutokana na kupambana na dhuluma kandamizi licha ya athari zinazomkumba katika kujikomboa kwake. Tumaini amedhihirishia jinsia ya kiume kuwa kijana wa kike anaweza kufanikiwa kujikomboa akiwa na lengo la kujikomboa kutokana na dhuluma kandamizi.

## SURA YA NNE

# MITAZAMO YA WAANDISHI : EUPHRASE KEZILAHABI, ROSA MISTIKA (1971) NA CLARA MOMANYI, TUMAINI (2006), KUHUSU DHULUMA DHIDI YA VIJANA WA KIKE.

## 4.0 Utangulizi

Katika sura hii ya utafiti, tunaangazia waandishi wawili wakuu. Mwandishi mmoja ni wa kiume ambaye ni Euphrase Kezilahabi na mwingine ni wa kike, Clara Momanyi. Waandishi hawa wawili wameandika riwaya zao katika vipindi tofauti. Euphrase Kezilahabi aliandika riwaya ya *Rosa Mistika* mnamo mwaka wa 1971 ilhali Clara Momanyi akatunga riwaya ya *Tumaini* mwaka wa 2006.

Katika sura hii tumemulika na kuangazia riwaya hizi ambazo zimeandikwa katika vipindi tofauti ambavyo vimeachana kwa takriban miaka arobaini. Vipindi hivi tumeviangazia ili kuchunguza kama kuna mabadiliko katika dhuluma inayomkabili kijana wa kike. Tumelinganisha na kulinganua uandishi wa kiume na wa kike. Pia tumeweza kuchunguza ni kwa kiasi gani kazi zao zimeathiriwa na itikadi, mitazamo yao binafsi pamoja na jinsia zao.

Kimsingi tumechunguza na kuona swala la dhuluma dhidi ya wahusika vijana wa kike linavyoshughulikiwa na waandishi hawa wawili wa jinsia tofauti. Aidha, mikondo wanayoichukua katika maelezo yao kutoka mwanzo hadi mwisho wa utunzi wao inaangazia. Mitazamo yao imechunguzwa ili kuipa jamii taswira na changamoto zinazomkumba mhusika kijana wa kike katika jamii.

## 4.1 Mwandishi wa Kiume

Euphrase Kezilahabi aliyeandika *Rosa Mistika* (1971) ndiye mwandishi wa kiume tuliyemteua katika utafiti huu unaoshughulikia swala la dhuluma dhidi ya wahusika vijana wa kike. Kezilahabi (1971) akiwatumia wahusika Rosa pamoja na Flora kama wahusika vijana wa kike anaonyesha jinsi vijana wa kike wanavyodhulumiwa na wanaume katika jamii yao. Rosa anakumbana na maisha ya dhiki na masaibu katika nyumba yao, shuleni na kutoka kwa mpenzi wake Charles. Babake Rosa anamtesa kwa kumpiga, kumtusi na hata kumfukuza kutoka kwao.

Kutokana na machungu aliyokumbana nayo, Rosa alianza kusaili kweli kama Zakaria alikuwa baba yake na mwishowe, akamwambia baba yake waziwazi kuwa yeye si babake .(Uk 57-58).

Zakaria hawaheshimu binti zake kutokana na kasumba ya ubabedume pamoja na kuzama kwake katika ulevi wake. Anawapiga na hata kufikia kiwango cha kuwavua mavazi na kusalia uchi. Mateso yaya haya anayaendeleza kwa binti zake wengine kwa kuwaamsha usingizini wakati ambapo wanafaa kulala ili waweze kumtumbuiza na kuendeleza mchezo aliouzoea (uk 5).

Mali aliyokuwa nayo Zakaria aliyaponda na kuyaharibu katika ulevi bila kujali masomo ya vijana wake wa kike. Mama yake , Rosa anapojitahidi kutafuta mali ili kuwaelimisha wasichana wake, Mzee Zakaria, anazichukua pesa hizo bila kumfahamisha bibiye na kuzitumia kujifaidi katika ulevi pamoja na walevi wenzake. Tukio hili linamfanya Rosa kutohudhuria shule mwezi mzima alipotakiwa kujiunga na shule ya upili.

Mwandishi Kezilahabi anadhihirisha na kuonyesha jinsi vijana wa kike wamedhulumiwa kwa kunyimwa uhuru wa kutangamana na wenzao vijana wa kiume. Zakaria anawachunga wasichana wake mithili ya ng'ombe na hata kuwapiga, nia yake ikiwa ni kuwatenga kabisa na jamii ya kiume. Mwandishi anakusudia kutuonyesha kuwa msichana katika jamii amenyimwa uhuru wa kuwa na haki ya kujumuika na kufurahi pamoja na wenzake wa kiume. Pindi vijana wa kike walipopata uhuru wa kutoka katika mazingira ya kuchungwa, vijana wa kiume nao hawakuwapa vijana wa kike usalama bali walikumbana na uchokozi (uk 14).

Mwandishi Euphrase Kezilahabi anadhihirisha na kuonyesha vile kijana wa kike Rosa na vijana wa kike wengine wanavyodhulumiwa na viongozi katika asasi za Serikali. Watu kama vile ni Deogratias wenye vyeo na wanayetumia vyeo vyao kuwanyanyasa vijana wa kike kimapenzi, kuwapachika mimba, kuwasaidia kuavya mimba na kuwatishia iwapo watafichua njama yake. Mkuu wa wilaya naye akiwa anayepaswa kuwa kielelezo kwa vijana anawakandamiza vijana wa kike na hata kuwasababisha kufukuzwa na kina baba zao. Mwalimu mkuu wa chuo cha ualimu, Bwana Thomas, naye anaonyeshwa na mwandishi kumdhulumu Rosa kimapenzi na kisha kumsababishia shida ya kukatwa sikio, kufedheheka na hata kufukuzwa chuoni.

Mwandishi huyu ana maoni kuwa wanawake pia wanatumiwa kwa kiwango kikubwa, kuwadhulumu vijana wa kike. Wanawake kama vile mke wa Thomas anampiga Rosa na hata kumkata sikio. Nao wanawake wa mtaa wa Uhuru wanamchukia Rosa, kumtusi na hata kumfanyia njama ya kumuua kwa kutumia sumu kali.

Mwandishi Kezilahabi, kwa kutumia wahusika Rosa na Flora, anaonyesha kwamba jamii pamoja na asasi ya elimu hazifai kumkandamiza kijana wa kike kwa kushikilia tamaduni zilizopitwa na nyakati za kuwanyima vijana wa kike uhuru. Jamii lazima izinduke na kufahamu kuwa kijana wa kike anafahamu ni yepi ya kuchagua na kuyatekeleza na ni yepi hayafai. Rosa, kijana wa kike, anaelewa kwamba msichana hapaswi kunyimwa uhuru wa kutangamana na vijana wa kiume kwa kuwa wataishi pamoja baadaye, pia babake kumpiga alikuwa akiingilia utawala usio wake (uk 9)

Kazi ya mwandishi Kezilahabi, Katika *Rosa Mistika* (1971), inaonyesha jinsi vijana wa kike wanavyodhulumiwa. Akitumia mhusika wake Rosa anaonyesha vile jamii inayoongozwa kwa misingi ya ubabedume inavyotarajia msichana kuwa mwanamwali. Tukio hili halizingatiwi kwa kijana wa kiume. Mwandishi anaonyesha na kudhihirisha jinsi Charles anavyomdhulumu Rosa kwa kisingizio cha kutaka kufahamu ubikra wa Rosa. Inapodhihirika kuwa si mwanamali kwa Charles licha ya kushiriki katika tendo hili, anamtenga. Rosa analiona tukio hili kama la kumvunjia heshima na kusema kwenye barua aliyoandika kabla ya kufa kuwa "ukimwonja mchumba wako kabla ya ndoa si bikira tena hata kama alikuwa" (uk 93).

Baada ya kuchunguza kindani jinsi Kezilahabi katika *Rosa Mistika* alivyomsawiri mhusika wa kike, hebu sasa tumwangalie Momanyi katika *Tumaini* ili kuweza kuwalinganisha na kuwalinganua waandishi hawa wawili.

## 4.2 Mwandishi wa Kike

Clara Momanyi aliyeandika *Tumaini* (2006) ndiye mwandishi wa kike. Tulimteua katika utafiti huu ili kuangazia swala la dhuluma dhidi ya wahusika vijana wa kike. Momanyi (2006) anaonyesha kijana wa kike katika hali yake hasa ya jamii na namna ambavyo utamaduni na mila zimevyomdhalilisha na kumweka katika nafasi ya pili akilinganishwa na kijana wa kiume. Kijana anayeangaziwa, hata hivyo, anafahamu kwamba amekandamizwa na kudhulumiwa na angetaka kujikomboa kutoka kwa minyororo kandamizi. Ogundipe-Leslie (1984) akinukuliwa na Katola (2006), anasema kuwa ni mwanamke mwenyewe ambaye anafaa atambue kuwa yeye tu ndiye anayeweza kuufasiri uhuru wake na kujua kile hasa anachohitaji. Haya yamelingana na vile mwandishi huyu anajaribu kuonyesha jitihada za mhusika mkuu kijana wa kike za kujiepusha na dhuluma dhidi yake. Tendo hili linadhihirisha kwamba kijana wa kike wa Kiafrika

anadhalilishwa na kunyanyaswa na jinsia ya kiume ilhali kijana huyu wa kike anaweza kujikomboa kutokana na udhalimu unaomkabili.

Mwandishi Momanyi anajaribu kuonyesha mazingira anamolelewa kijana wa kike ni ya mashambani, mahali malezi ya kijana wa kike yanaongozwa na desturi na mila za jamii husika. Katika mazingira haya mifumo ya ubabedume ikiambatana na itikadi vimetawala katika mahusiano ya kijinsia. Mifumo ya kiubabe dume inakandamiza jinsia ya kike. Mwandishi anabainisha haya kwa kuonyesha mahusiano baina ya kijana wa kike na jinsia ya kiume katika jamaa na jamii.

Mwandishi Momanyi ameteua mhusika Tumaini na kumtumia kudhihirisha jinsi kijana wa kike anavyoweza kuwa na ujasiri na ushujaa wa kupigania uhuru wake. Tumaini ametumika kudhihirisha harakati ya kujikomboa kutokana na dhuluma kandamizi inayoongozwa na mifumo kandamizi ya ubabedume. Haya yamedhihirika wakati Tumaini anapokuwa darasa la saba na Mzee Masumbuko ana njama ya kumpasha tohara na kumwoza kwa mwanamume asiyemfahamu. Hali hii imemfanya Tumaini kuamua kutorokea kwa mamake mdogo Bi. Halima. Kutokana na kutoroka kwake, mwandishi amedhihirisha kwamba Tumaini ana msimamo wa kujikomboa kutokana na kandamizi za kiubabedume za babake. Kwa upande mwingine, vitisho vya babake, Mzee Masumbuko, vimedhihirisha dhuluma dhidi ya kijana wa kike vilivyo na misingi ya ubabedume.

Mwandishi wa Tumaini amebainisha kwamba jamii ya Tumaini ina makundi mawili. Kundi moja ni la kumwangazia kijana wa kike na lingine limemtetea kijana wa kike kutokana na dhuluma kandamizi. Bi. Halima na mumewe Shabani na mjomba Yusufu wamemtetea Tumaini na hata kumkabili Mzee Masumbuko anapowaalika wageni kwa siri kuleta posa ya Tumaini. Aidha Bi. Halima na Shabani wamempa Tumaini hifadhi na kumfadhili katika masomo yake na hata kumpa ujasiri katika kujitetea.

Katika jamii ya *Tumaini* asasi ya uongozi imeonyeshwa na mwandishi kuwa imegawika katika mtazamo wa kumdhulumu kijana wa kike. Kuna viongozi wa kiume wanaomdhulumu kijana wa kike kama vile Chifu Andrea anayehusika katika njama ya kuondoa jina la Tumaini kutoka kwenye orodha ya ufadhili na pia kuwanyanyasa vijana wa kike kimapenzi. Mwalimu Majaliwa pia amewakandamiza vijana wa kike kwa kuwanyima haki ya kujichagulia masomo wayapendayo. Mwandishi anatumia viongozi kama mwalimu Mwadime katika kutetea

unyanyasaji dhidi ya kijana wa kike. Bwana D.O alikuwa na msimamo thabiti katika kumkemea Chifu alipogundua kuwa alikuwa na njama ya kumdhulumu Tumaini kwa kumnyima nafasi yake katika orodha ya ufadhili.

Katika *Tumaini* (2006), Idi, kijana mdogo wa kiume, ametambua kuwa kijana wa kike ni mali ya jamii, bidhaa za uwekezaji, mtumishi wa nyumbani na anayesubiri kuolewa wazazi wapate pesa za kumsomesha. Tumaini alipomwambia babake amkanye Idi , alikomeshwa kwa kuonywa kuwa asijaribu kumwingilia Idi kwa kuwa yeye alikuwa kijana wa kiume na wala si wa kike (uk 29). Mwandishi amedhihirisha kwamba jamii hii imembagua kijana wa kike na kumtukuza wa kiume.Hii ni ishara kwamba kijana wa kiume ana mamlaka ya kuwakemea vijana wa kike waliokomaa kiumri. Mtunzi wa riwaya ya *Tumaini* amedhihirisha kwamba jamii hii imemtweza kijana wa kike huku ikimtukuza yule wa kiume kwa misingi ya ubabedume. Haya yamethibitika kutokana na mapendeleo kwa kijana wa kiume ilhali wa kike akidunishwa.

Mwandishi wa *Tumaini* (2006), amedhihirisha kwamba jamii ya Tumaini imesadiki kwamba dhuluma dhidi ya kijana wa kike haina mkombozi wala mtetezi. Kutokana na tukio la Zena, mtoto wa Mzee Bakari, alivyonyanyuliwa juujuu na genge la vijana, alipoomba usaidizi wakati juhudi zake za kujiopoa zilipoambulia patupu, wanaume waliambaa ilhali wanawake wakipita na hamsini zao. Unyama huu unatendeka mchana peupe wakati ambapo angepata msaada lakini kutokana na itikadi na mila kandamizi hakupata msaada wowote. Mwandishi amedhamiria kuonyesha jinsi hali halisi ya unyanyasaji kwa vijana wa kike ilivyo.

Mwandishi wa *Tumaini* (2006) ameonyesha kwamba kuzaliwa kwa kijana wa kike hayakuwa mapenzi ya Mungu ateseke bali ni sheria za mila na itikadi za kitamaduni. Hali hii inaibuka kutokana na ugawaji wa majukumu yaliyo na misingi ya uana. Hivyo, hali hii inaweza kubadilishwa na wanawake wenye muungano kama vile chama cha *Jitihada Womens' Group*. Hiki ni chama ambacho mwandishi wa *Tumaini* amekitumia katika utunzi wake kudhihirisha jinsi wanawake wanavyoungana kutetea masilahi ya kijana wa kike. Hata hivyo, chama hicho hakijasajiliwa kwani kimekwamiza na jitihada za chifu pamoja na wazee kadhaa mle kijijini na ambao ni wenye mifumo iliyozama katika mila na tamaduni zenye misingi ya ubabedume.

Mashaka na Rehema ni vijana wa kike wenye umri mdogo ambao wanaozwa kwa wazee wa makamo. Wanakumbana na mateso mengi kama vile kuteswa na wakewenza, kudharauliwa na waume zao na kuzalishwa watoto wengi wakiwa na umri mdogo. Wakati wa kujifungua

wanakumbana na matatizo ya uzazi yanayotokana na umri wao mdogo. Mashaka anateseka kiasi cha kukaribia kufa kama haingekuwa bahati ya Tumaini kuzuru nyumbani kwake.

Mtunzi wa riwaya ya *Tumaini* amedhihirisha kwamba baadhi ya wanawake wamechangia katika kumnyanyasa kijana wa kike. Mamake, Tumaini ameshirikiana kwa siri na babake katika njama ya kumdhulumu. Bi. Selina ameshiriki katika kuficha udhalimu wa mumewe dhidi ya vijana wa kike. Bi. Maimuna alishiriki katika njama ya kumkejeli Tumaini kwa kumwita 'msungo' na kutaka aolewe mapema.

Mwandishi wa kike, Momanyi (2006), ameshughulikia swala la dhuluma dhidi ya wahusika vijana wa kike. Imedhihirika kwamba ni kijana Tumaini pekee ambaye amejitahidi kupinga ule utumwa unaowakabili na kuonyesha kielelezo cha jinsi vijana wa kike wanavyopaswa kuwa na ujasiri wa kujikomboa ili kuwa huru kutoka kwa kandamizi za kiume.

## 4.3 Ulinganishi na Ulinganuaji wa Dhuluma katika Riwaya za Tumaini na Rosa Mistika.

Katika sehemu hii tumeangazia maswala ya ulinganishi na ulinganuzi wa waandishi wa kiume na kike mtawaliwa katika riwaya teule na ambazo ni Kezilahabi na Momanyi. Maelezo yetu yanaelezea kwa muhtasari swala la dhuluma dhidi ya vijana wa kike kama vile limeshughulukiwa na waandishi hawa wawili na walio wa jinsia tofauti.

Katika riwaya zote mbili za *Rosa Mistika* na *Tumaini* inabainika kwamba kuna matatizo tisamakuu yanayowakumba vijana wa kike katika jamii hizi mbili za waandishi. Matatizo haya ni kudharauliwa, kupigwa, kubakwa, vitisho, matusi, kubaguliwa na kunyimwa haki, kuchuuzwa, kupachikwa mimba, kunyanyaswa kimapenzi pamoja na kukanwa na jamii. Matatizo haya yanayodhihirisha jinsi vijana wa kike wanavyokumbana nayo katika jamii zao yameshughulikiwa na waandishi hawa wa riwaya mbili teule katika utafiti huu.

Kuna maswala ya kulinganua katika dhuluma kama vile ukeketaji, ndoa za lazima na mateso katika ndoa. Inadhihirika kwamba matatizo haya yanawakumba vijana wa kike katika jamii ya riwaya ya *Tumaini* ya mwandishi wa kike C. Momanyi. Tatizo la kudhulumiwa na matokeo kuwa kifo yalimkumba kijana wa kike katika riwaya ya *Rosa Mistika*. Masuala ya uke wenza, kuzalishwa watoto katika umri mchanga yanaathiri tu vijana wa kike katika jamii ya *Tumaini*.

Katika riwaya zote mbili, waandishi wote wawili wa riwaya hizi wameshughulikia swala la tamaduni zilizopitwa na wakati. Inadhihirika namna ambavyo wazazi wa kiume wenye mashiko katika tamaduni hizi wanavyowadhulumu vijana wao wa kike. Mzee Masumbuko katika *Tumaini* na Mzee Zakaria katika *Rosa Mistika* wana misingi katika itikadi zilizopitwa na wakati katika kuwadhulumu binti zao.

Swala la wahusika vijana wa kike linaloonyesha misimamo thabiti katika kujikomboa kutokana na dhuluma zinazowakumba linaangaziwa na waandishi wote wawili. Vijana hawa wanadhihirisha ujasiri katika kujikomboa ili kupata uhuru katika maswala ya kutafuta elimu na kutoroka nyumbani ili kuepukana na dhuluma zaidi. Mifano hii inadhihirisha jinsi kila jamii, licha ya kuwa na matatizo yanayolingana vilevile kila mmoja huwa na matatizo yake binafsi yanayotofautiana na ya mwingine.

Katika riwaya zote mbili za *Rosa Mistika* na *Tumaini*, waandishi hawa wanadhihirisha mioyo migumu ya wazazi wa kiume kwa wanawao wa kike pale wanapowakataa na kuwaambia wazionee nyumba zao kwa paa. Waandishi hawa wanadhihirisha mioyo hii migumu ya kuwakataa vijana wao wa kike hadi tamati ya tungo zao. Katika riwaya hizi, kina mama hawawajibiki kuwakomboa binti zao kwa sababu ya woga waliotiwa na waume zao.

Tatizo la kukandamizwa na kudhulumiwa kwa vijana wa kike na vijana wenzao wa kiume linadhihirika katika uandishi wa kike na vilevile ule wa kiume. Vijana wa kiume katika riwaya hizi mbili wanaendeleza udhalimu kwa vijana wenzao wa kike wanapokuwa shuleni na hata katika mazingira ya nje ya shule. Waandishi wote wanabainisha kuwa jamii haishughuliki katika kuwauni vijana wa kike kutokana na dhuluma wazokumbana nazo kutoka kwa wenzao wa kiume. Mwandishi wa kike, ambaye ni Momanyi katika riwaya ya *Tumaini* anabainisha kuwa katika harakati za wanaume kuwadhulumu vijana wa kike kuna baadhi ya wanaume ambao wanashiriki katika kumtetea na kumkomboa kijana wa kike. Wanaume hao wamejitokeza katika kupinga njama za wanaume wenzao katika harakati za kuwanyanyasa vijana wa kike. Wazee kama Shabani, Yusufu, Mwalimu Mwadime na Bwana D.O wanashiriki katika kumtetea kijana wa kike na kumuauni kutokana na dhuluma kandamizi ilhali katika jamii ya Rosa kijana wa kike hana mtetezi wa kiume.

Wandishi E.Keziilahabi na C.Momanyi wa kiume na yule wa kike wanaafikiana na kulingana katika tungo zao kuwa wanawake pia wameshiriki katika kuchangia katika dhuluma

zinazokumba jamii ya Rosa na Tumaini. Inabainika katika tungo za waandishi hawa kwamba vijana wa kike nyakati zingine wamejikuta wakidhulumiwa na wanawake kiasi kwamba masaibu hayo yanawatia uchungu katika maisha yao.

### 4.2.1 Taswira Hasi

Katika riwaya za Rosa Mistika na Tumaini ambazo tumeshughulikia vijana wa kike wamepewa picha mbaya zinazofanana. Vijana hawa wa kike wamechorwa kama viumbe dhaifu, waasi wa mila na tamaduni, vyombo vya kutumbuiza wanaume kimahaba na 'malaya'. Sifa hizi walizopewa vijana wa kike zinahitilafiana na kulingana katika riwaya mbili tunazotafitia. Swala la kijana wa kike kuonekana kama malaya linaangaziwa kwenye riwaya ya *Rosa Mistika* (1971) ilhali hali hii haijitokezi katika riwaya ya *Tumaini* (2006). Picha hii ambayo kijana Rosa amepewa inawafanya vijana wa kike waonekane waovu na wabaya katika jamii. Sifa hii ya uovu imehuzishwa kwa kijana wa kike kulingana na mtazamo wa jamii ya Rosa inavyowaangazia.

Vijana wa kike wamesawirika kama vyombo vya kutumbuiza kimahaba vijana wa kiume na wazee wa kiume katika riwaya za *Rosa Mistika* na *Tumaini.* Usawiri huu unawavunjia heshima na kudhalilisha hadhi zao katika jamii. Vijana wa kike hujikuta wakiwa wanyonge wasio na usemi katika maswala yanayowahusu kutokana na sifa na picha hii wanayopewa katika jamii zao.

Picha mbaya ya vijana wa kike inayojitokeza katika riwaya mbili za *Rosa Mistika* na *Tumaini* ni ile ya kuwachora vijana wa kike kama viumbe dhaifu na waasi wa mila na tamaduni katika jamii zao. Hali hizi zimejengwa katika riwaya hizi mbili kiasi kwamba zinawadunisha na kuwafanya kujiona kuwa wamesalitiwa na jamii zao. Picha hizi zinawafanya waweze kuibua mbinu za kupigania haki zao na kuwa na msimamo wa kutaka kujitetea, tukio linalowafanya wajikute kwenye masaibu mengi katika jamii wanamoishi.

Katika *Rosa Mistika* mtunzi Kezilahabi amempa taswira hasi Rosa na ambayo ni ya kuwa dhaifu anaposhindwa na jaribio la kuachwa na mpenzi wake Charles Lusato. Rosa anashindwa kumudu hali ya upweke na anaamua kujiua. Kifo kinachowakilishwa na hali hii kinaleta picha hasi na kutuonyesha kuwa vijana wa kike ni dhaifu. Katika *Tumaini,* mtunzi anampa Tumaini picha hasi ya kuwa muasi pale anapokataa kufuata mila na tamaduni za jamii yake ya kupashwa tohara. Mwandishi anaendeleza hali ya uasi wake zaidi anapomsawiri kwa kumpa jina la msungo.

Tumaini anapokaidi matakwa ya babake ya kuolewa na kuendelea na masomo, jamii nzima ya Tumaini inamwangazia kama muasi wa tamaduni zake.

### 4.3.2 Taswira Chanya

Waandishi Kezilahabi na Momanyi wa riwaya za *Rosa Mistika* na *Tumaini* mtawalia wamewaumba wahusika vijana wa kike na kuwachora vizuri kwa kutoa mifano kadhaa inayodhihirisha kuwa vijana hao wamepewa sifa nzuri ya kuwa wavumilivu, wenye ujasiri, wenye msimamo thabiti, wanye bidii, wanaowajibika, washiriki katika ukombozi wao na ni weledi.

Riwaya zote mbili *Rosa Mistika* na *Tumaini* zimewapa vijana wa kike sifa ya kuwa wavumilivu katika mateso wanayokumbana nayo katika jamii zao hadi kuibuka washindi. Wamevumilia mateso ya kudharauliwa, kupigwa, kunyimwa haki, kutusiwa na kubaguliwa. Katika maisha yao yote ya ukuaji, wanaume, hasa wazazi wao wa kiume, na vijana wenzao wa kiume wanawadhalilisha lakini wao wamevumilia. Tumaini amevumilia dhuluma nyingi katika jamii hadi akafaulu kujiunga na chuo kikuu huku naye Rosa akivumilia majaribu kiasi cha kufikia ufanisi wa kuwa mwalimu wa shule ya msingi. Vijana wa kike wamesawirika kuwa wavumilivu wakati wa majonzi na hata kutoa machozi lakini wakawa na ari ya kuafikia malengo yao.

Rosa, Flora na Tumaini wamesawirika katika tungo tulizotafitia kuwa vijana wenye ujasiri katika kutetea hali zao. Wanakiuka matarajio ya itikadi na mila kandamizi mradi, kwa mtazamo wao, waliyoyadhamiria waweze kuyafikia na hii ni busara. Tumaini ameumbwa na kupewa sifa ya ujasiri anapokaidi matakwa ya babake ya kukeketwa na kuozwa kwa lazima. Tumaini alikabili kikao cha Bwana D.O alipofahamu kuwa jina lake limetolewa kwenye orodha ya wanaofadhiliwa. Mwalimu Majaaliwa anapomwamuru asichague masomo ya Sayansi, anakuwa na ujasiri kwa kukaidi amri yake. Rosa na Flora katika *Rosa Mistika* wanakuwa na ujasiri wa kukabiliana na baba yao kwa ujasiri anapowanyima uhuru na kutaka kuwachunga kama ng'ombe. Hali hii imewapa taswira chanya ya kuwa na msimamo thabiti.

Kwenye masomo, vijana wa kike wamepewa taswira chanya katika riwaya ya *Rosa Mistika* na ile ya *Tumaini*. Vijana wa kike wanadhihirisha kuwa na bidii kiasi cha kuwashinda vijana wa kiume. Mwandishi Clara Momanyi katika *Tumaini* amedhihirisha kuwa kijana Tumaini aliwashinda vijana wa kiume katika masomo yake. Tumaini ametia bidii na kufanya vyema katika masomo ya Sayansi yaliyofahamika kuwa ya wavulana. Kufuzu kwa Tumaini katika

kidato cha nne na kujinyakulia nafasi katika chuo kikuu kusomea udaktari ni sifa kuu katika kuwapa vijana wa kike taswira chanya. Riziki na Rosa nao wamefaulu katika masomo na kupata kazi ya ualimu picha inayowapa sifa nzuri vijana wa kike.

Taswira chanya ya vijana wa kike ni ile ya kuwajibika ambayo imeshughulikiwa katika tungo za *Rosa Mistika* na *Tumaini.* Riwaya ya *Tumaini* imemchora Tumaini kuwa kijana wa kike anayewajibika wa kutoa ushauri mwema kwa vijana wenzake wa kike kuhusu umuhimu wa masomo na kupuuza dhana kuwa masomo ya Sayansi na Hesabu ni ya vijana wa kiume. Tumaini anazidisha uwajibikaji kwa kuwapa ushauri vijana wa kiume kuhusu mtazamo wao hasi kwa vijana wa kike. Rosa na Tumaini wanawajibikia elimu yao pale wanaposhiriki katika kutafuta karo ya masomo yao.Tumaini anatafuta kazi ya sulubu kwa chifu Andrea akiwa na nia ya kupata karo naye Rosa na Flora wanamsaidia mama yao kuuza pombe ili kutafuta karo ya Rosa. Flora katika *Rosa Mistika* anapewa taswira chanya ya kuwajibikia ndugu zake baada ya wazazi na dadake kuaga. Flora aliwaombea ndugu zake ruhusa ya kukaa na masista miaka miwili na baadaye anamua kuwatunza kwa kuishi na ndugu zake katika makao ya mpenzi wake, John, alipowakubali.

Sifa ya vijana wa kike kuwa na bidii na kushiriki katika ukombozi imeangaziwa katika riwaya za *Rosa Mistika* na *Tumaini.* Waandishi wa riwaya hizi wamewaumba vijana wa kike kuwa mashujaa stadi katika kupigania ukombozi wao dhidi ya dhuluma zinazowakabili. Mwandishi wa *Tumaini* amempa kijana Tumaini taswira chanya katika kupigania haki dhidi ya dhuluma kandamizi dhidi ya vijana wa kike. Tumaini anakiuka na kupuuza vitisho anavyokabiliwa navyo kutokana na jinsia ya kiume na kuwa na ujasiri katika kukabiliana na dhuluma zinazomkumba. Anatoroka kwao anapogundua njama ya babake pamoja na mipango yake ya kumpasha tohara na kumuoza. Ujasiri wake unamsaidia katika kukabiliana na njama ya babake na chifu kwa D.O. Anakataa na kupuuza vitisho vya majuto kwa kusimama na kisu kujitetea, anakabilina na chifu katika harakati za kutaka kubakwa na mwisho anakuwa na msimamo imara kuhusu kuchagua masomo ya sayansi aliyoyapenda. Katika *Rosa Mistika*, mwandishi amewapa Rosa na Flora sifa ya kuwa watetezi wa haki zao na wanaotaka kujikomboa kutokana na itikadi na imani katika mila zilizopitwa na wakati. Rosa anakabiliana na babake kiasi cha kutomtambua kama babake anaponyimwa uhuru wake. Baada ya kufuzu chuo, Rosa anaamua kuishi peke yake na kuwa na msimamo wa kutotaka mwanamume katika nyumba yake baada ya kugundua hila za kiume. Flora katika *Rosa Mistika* ameamua kujichagulia mchumba wake, John, na kuamua kuishi naye

na kupuuza hali ya kuchungwa kama ng'ombe. Hali hii ya kujikomboa kwa Flora ndiyo iliyowauni ndugu zake wadogo baada ya kufiwa na wazazi wake.

## 4.6 Hitimisho

Katika sura hii tumechanganua mitazamo na mielekeo ya wandishi wa kiume na wa kike katika kazi walizoandika katika vipindi toauti na hata nchi tofauti za Afrika Mashariki kuhusiana na mhusika wa kike. Tumelinganisha na kulinganua uandishi wa jinsia ya kike na wa kiume kuhusu dhuluma dhidi ya wahusika vijana wa kike. Waandishi hawa wamewapa taswira hasi na chanya vijana wa kike katika tungo zao.

Imebainika kwamba waandishi hawa wanalingana kwa kiasi na kutofautiana pia. Mikabala yao katika maelezo yao kuwahusu wahusika vijana wa kike katika harakati za kujinasua kutokana na itikadi na mila kandamizi ya kiume. Licha ya wanaume kudhihirisha ukandamizaji kwa vijana wa kike, waandishi wamewashirikisha wanaume hao katika juhudi za ukombozi wa vijana wa kike baada ya vijana hao wenyewe kuwa na ari ya kujikomboa

Kutokana na uchunguzi katika utafiti huu imedhihirika kuwa mitazamo hii ya waandishi katika kazi zao imechangiwa na mabadiliko ya kiwakati ambayo yametokea katika muda wa uandishi wao. Aidha mitazamo yao ya uandishi imechochewa na hali ya kijinsia ya waandishi wenyewe. Momanyi (2006), amemuumba kijana wa kike kuwa na ujasiri na ukakamavu mwingi kitaka kuonyesha ushindi dhidi ya mwanamume. Hii ni kinyume na Kezilahabi (1971) ambaye amedhihirisha unyonge katika kujikomboa kwa kijana wa kike labda kwa kuongozwa na kasumba na taasubi ya ubabedume kuwa ukombozi wa kijana wa kike unaegemea kushiriki kwa mwanamume kwenye vita vyake vya ukombozi.

Inathibitika kwamba waandishi wa jinsia zote wanakubaliana na utambuzi wa nadharia Ufemisti huru inayoongoza utafiti huu kuwa kijana wa kike wa Kiafrika amekabiliwa na dhuluma kutoka kwa mwanamume anayeongozwa na tamaduni na mila katika kumkandamiza. Ili kupata ukombozi na uhuru wake itamlazimu kijana wa kike kufahamu haki zake, kuwa na msimamo thabiti na kushirikiana na watu wengine katika kujiondoa kutokana na nafasi kandamizi aliyowekewa na jamii. Ni wazi kwamba kijana wa kike ni shujaa na anaweza kujikomboa na kuishi bila kudhulumiwa licha ya kukabiliwa na mifumo mikali na kandamizi ya kiume. Haya yamebainika kupitia kwa wahusika hao vijana wa kike katika riwaya za tulizoshughulikia za Kezilahabi na Momanyi.

Katika sura ifuatayo tunatoa muhtasari wa mahitimisho kwa kujiegemeza kwenye malengo ya utafiti na Nadharia tete  na kisha kutoa mapendekezo kuhusiana na yafaayo kutafitiwa zaidi kuhusiana na mada yetu ya utafiti.

# SURA YA TANO

## MUHTHASARI NA MAPENDEKEZO.

### 5.0 Utangulizi

Sura hii inazungumzia swala la matokeo ya utafiti huu kulingana na madhumuni tuliyoyateua pamoja na yale yaliyoibuka kuhusiana na mada katika vitabu tulivyovishughulikia. Katika sura hii pia tumeangazia mapendekezo yanayotarajiwa yafanywe kwenye tafiti za baadaye katika kazi ya fasihi.

### 5.1 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Swala la dhuluma dhidi ya vijana wa kike linabainika katika riwaya mbili *Rosa Mistika* (1971) na *Tumaini* (2006), tulizoshughulikia kwenye utafiti huu. Swala la dhuluma limejitokeza kwa hali mbalimbali na kudhihirisha kuwa kijana wa kike amekandamizwa na kunyimwa haki. Hali hii imebainika kutokana na sababu ya kumuona kama kiumbe duni na jinsia ya kiume yenye misingi na kaida zenye mashiko katika mila na tamaduni zinazompendelea kijana wa kiume. Katika jamii,mila na tamaduni hizi zinajidhihirisha kwenye matamshi na matendo yanayoelekezwa kwa kijana wa kike kutoka kwa wanaume na vijana wa kiume. Katika utafiti huu, vijana wa kike wanakumbana na dhuluma ya kupigwa kama mbinu ya kuwaadhibu. Kutokana na kupigwa, vijana wa kike hutiwa woga na kuwafanya wawe wanyamavu na kuwanyenyekea wanaume. Vijana wa kike wanapopigwa, huathirika kimwili kutokana na uchungu wa kupigwa na pia huumizwa kutokana na woga wanaotiwa. Vijana hawa wa kike hujikuta wakiwanyenyekea wanaume na kusababisha kuwa watiifu hata katika maswala yanayowadhalilisha. Hivyo basi mfumo huu wa ubabedume humpa mamlaka ya kumtawala kijana wa kike katika nyanja zote za maisha.

Inadhihirika bayana kwamba vijana wa kike wanadharauliwa hivyo basi kuwadunisha na kuwatweza. Mara nyingi kijana huyu wa kike hukabiliana na matusi kwa kuitwa mshenzi, mjinga, malaya na hata maneno ya utani yenye matusi ndani yake kama vile " msungo", "Lab" na "Zoo". Maneno haya huwadhalilisha na kuwafanya kujiona kuwa viumbe duni katika jamii zao.

Katika muktadha huu, neno kama 'malaya' lina mshiriki na mshirika. Ajabu ni kwamba kijana wa kike huitwa malaya ilhali mwenzake wa kiume ambaye ni mshirika katika tendo hili la kuitwa malaya haitwi Malaya. Hapa panadhihirika uonevu kwa vijana wa kike unaochochewa na taasubi ya ubabe dume.

Dhuluma ya tohara ya lazima kwa kijana wa kike yenye makusudio ya kuwaandaa kwa ndoa ya lazima ni dhuluma iliyodhihirika kwenye utafiti huu. Vijana wa kike hana uamuzi wowote kuhusu tendo hili ambalo linamnyima haki zake za usichana. Inabainika kwamba pindi tu anapopashwa tohara kijana hayu hukatiziwa masomo yake na kuozwa kwa lazima ilhali kijana mwenzake wa kiume akiendelea na masomo. Hali hii inabainisha wazi kuwa kijana wa kike hathaminiwi katika jamii ya Kiafrika. Kuachishwa kwake masomo kwa minajili ya kupashwa tohara wakati mwenzake wa kiume anapoendelea na masomo ni hali ya kumpa kijana huyu nafasi ya pili huku mwenzake wa kiume akipewa nafasi ya kwanza katika jamii hii ya Kiafrika.

Ndoa ni asasi moja kandamizi kwa vijana wa kike. Imedhihirika kuwa vijana wa kike wanatazamwa na jamii kama vitega uchumi, vipeto vya kuchuuzwa na kuozwa kwa wanaume waliochaguliwa na wazazi wao wa kiume. Mahari yanayotolewa katika ndoa hizi ni miliki ya wanaume. Katola (2006:125), anasema kuwa hapo awali mahari yalitolewa kama ishara ya shukrani kwa wazazi wa msichana aliyeolewa.Kwa sababu ya ubinafsi na mifumo ya ubabedume, utoaji wa mahari umechukua mwelekeo tofauti, kinyume na hapo awali wakati mahari yalitolewa kama zawadi. Inabainika katika utafiti huu kuwa mahari ni njia ambayo wanaume wanaitumia kujipatia mali. Katika tendo hili la ndoa, inadhihirika kwamba vijana wa kike wanaozwa wakiwa na umri mdogo na hili ni changio la masaibu ya kiuzazi yanayowakumba wakati wanapojifungua watoto.

Imejitokeza kwamba vijana wa kike wanakumbana na dhuluma ya kubakwa na pia kupachikwa mimba katika harakati zao za kusoma. Juhudi zao za kujitetea zinazimwa pale wanapojitetea kwa kukumbana na vitisho kutoka kwa wanaume na hata watetezi kama vile kuhongwa na kuzima juhudi zao za kujitetea. Hali hii ya kuzima juhudi ni dhuluma inayowadhalilisha baada ya kufanyiwa maonevu ya kuwadhulumu. Kijana wa kike anakandamizwa na taasubi ya kiume. Dhuluma hii ya kubakwa inaendelezwa na wanaume wa sampuli yote yaani vijana wa kiume, wazee na hata viongozi serikalini. Tendo hili la kukumbana na unyanyasaji kutoka kwa jinsia ya kiume inadhihirisha ukandamizi unaomkumba kijana wa kike.

Imebainika kwamba vijana wengi wa kike wanapodhulumiwa hutishwa pia. Kutishwa kwao kunawafanya wawe wanyamavu na kuyavumilia mateso moyoni. Kutokana na vitisho hivi, vijana wa kike huathirika kisaikolojia. Aidha vijana hawa huwa wanyamavu, hutoa machozi, huzungumzia nafsi na hata kuwa na mawazo mengi akilini. Dhuluma ya vitisho imebainika kuwafanya wasiwe na ari ya kutekeleza majukumu yao vyema na hata kuwavunja moyo wa kutetea uhuru wao.

Vijana wa kike wamebaguliwa na kunyimwa uhuru wao. Vijana wa kike wanatawishwa na kutarajiwa kuwa makao yao ni nyumbani. Hawatakiwi kutoka nje ya makao yao ili kutangamana na vijana wenzao wa kiume. Wanapokuwa shuleni wananyimwa haki ya kujumuika na kutangamana na vijana wa kiume. Hali hii inawadunisha na kuwafanya wajione kama viumbe duni na dhaifu kimwili na kiakili. Mtindo huu wa kuwatawisha unawafanya kukosa kuwa na mtazamo mpevu kuhusu maisha yao ya kike na ushirikiano wao na wavulana. Kutokana na dhuluma hii, vijana wa kike wanabidiika kuwaona wavulana kama watu ambao hawafai kushirikiana nao katika maisha yao. Ili kuwe na mafanikio katika jamii yoyote ile ni lazima mwanamke ashirikiane na mwanamume. Hali hii inadhihirisha kuwa jamii ya Rosa na ile ya Tumaini haziwezi kufikia lengo la mafanikio haya ikiwa vijana wa kike watabaguliwa na kunyimwa uhuru wao.

Wanaume wa umri wa makamo wanadhihirika kuwa ndio wanaochangia zaidi katika kuwadhulumu vijana wa kike. Viongozi ambao wamepewa majukumu ya kuwa walinzi wa vijana wa kike nao wako katika mstari wa mbele katika kuwanyanyasa kimapenzi vijana wa kike. Wanaume wanaopaswa kuwa vielelezo bora katika kuwaelekeza na kuwatetea vijana wa kike wanadhihirisha ukandamizi wao wanapowadhulumu vijana wa kike. Kutokana na taasubi zao za ubabedume zinazongozwa na uchu katika kuwatumia vijana wa kike kimapenzi. Wanawapachika vijana wa kike mimba kisha kuwatishia wasifichue maovu waliyotendewa na hata kushauriwa kuavya mimba hizo. Wanaume hawa ndio wanaowakana vijana wa kike katika jamii pindi vijana wa kike wanapokuwa na msimamo thabiti katika kutetea haki na uhuru wao wa kutaka kujikomboa kutoka kwa mila na tamaduni zenye misingi ya ubabe dume.

Katika nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, tapo la Ufeministi huru inadhihirika kuwa kijana wa kike anakabiliwa na dhuluma inayotawaliwa na misingi ya ubabe dume kama vile tohara na ndoa lazima. Inabainika kuwa nafasi ya kijana wa kike katika jamii ni ile ya pili baada ya kijana mwenzake wa kiume. Ni kwa misingi hii ambapo kijana wa kike anainuka na kuwa na moyo wa

kujikomboa kutokana na dhuluma kandamizi zinazomkumba. Nadharia tuliyoiteua na kuitumia ya Ufeministi huru katika utafiti huu inakubaliana na kazi tuliyoichunguza.

Katika utafiti huu athari za dhuluma dhidi ya kijana wa kike zimebainika. Imedhihirika wazi kuwa baada ya kijana wa kike kulemewa na dhuluma kandamizi zenye mifumo ya kiubabedume anaamua kutoroka kutoka kwao nyumbani. Lengo la kutoroka kwao likiwa ni kutafuta hifadhi ambapo atapata ukombozi wa haki zake na uhuru wao wa kuwajibikia mahitaji yake bila kukatizwa. Vijana wengi wanafanya uamuzi kutorudi kwao mpaka watakapofikia nyota ya ndoto yao katika masomo. Haya ni baada ya kutambua kuwa wazazi wao wa kiume hawako tayari kubadilisha nia yao kuhusu misimamo yao ya kuwakatishia masomo na kuwaoza.

Baadhi ya vijana wa kike wanashindwa kuendelea kufuata mifumo na itikadi kandamizi ya kuwatisha na kuwafanya kuishi kwa woga. Vijana wa kike wanakumbana na hali ya kuishi kwa hofu na wasiwasi. Vitisho hivi vinadhamiria kumkandamiza kijana wa kike na kumnyamazisha ili asiwe na ari ya kupigania ukombozi wa uhuru wake. Hizi taasubi za kiume zinadhamiria kumkandamiza kijana wa kike ili asipate kupingwa na jinsia ya kike, ndiposa aendelea kujinufaisha na kutawala. Mojawapo ya madhumuni kwenye utafiti huu ni kubainisha athari zinazojitokeza kutokana na dhuluma dhidi ya wahusika wa kike. Katika jamii athari mojawapo tuliyoangazia inalenga kuafikiana na madhumuni ya utafiti kwamba vijana wa kike wanaokandamizwa na dhuluma wanajaribu kupambana na udhalimu kandamizi wenye itikadi na imani zenye misingi ya kiubabe dume. Hivyo basi wameamua kupuuza misingi na mifumo dhalimu kwa kuamua kupigania haki na ukombozi wao. Hali hii inaafikiana na nadharia tunayoitumia yenye malengo ya kumkomboa kijana wa kike na kupuuza udhalimu.

Ukandamizi wa dhuluma zenye misingi ya kiume inayopinga elimu ya vijana wa kike inaafiki hali ya vijana wa kike kupoteza imani katika tamaduni na mila zenye mifumo inayoongozwa na jinsia ya kiume. Viongozi katika jamii wamechangia katika kumtweza kijana wa kike katika asasi ya elimu na kumtwaza kijana wa kiume. Dhuluma hii ya kiume dhidi ya kijana wa kike katika elimu imezua matatizo katika ushirika wa vijana katika kupata elimu. Harakati ya kujikomboa katika asasi hii ya elimu inawafanya vijana wa kike kuonekana kama waasi wa maadili.

Imebainika katika utafiti huu kuwa licha ya vijana wa kike kupigania kujikomboa kutokana na dhuluma zinazowakandamiza. Kuna vijana wa kike na baadhi ya wanawake wanaoendeleza

udhalimu dhidi yao. Wanawake hawa ni wale waliokata tamaa na kukubali kwamba vijana wa kike hawawezi kupigania haki zao na kujikomboa bila kumhusisha mwanamume. Kwenye utafiti huu imebainika kuwa kuna vijana wa kike waliojitahidi na kujitolea kukabiliana na wanaume katika kupigania ukombozi wa haki zao. Vijana hawa wanajitahidi kujikomboa na kuwakomboa wenzao wanaodhulumiwa ili kuweka jamii ya vijana wa kike huru kutokana na kwa dhuluma zenye misingi ya ubabedume zinazowakumba katika jamii ya Rosa na Tumaini.

Inajitokeza katika utafiti huu kwamba kuna ulinganifu na kutofautiana katika uandishi wa kiume na wa kike. Katika riwaya mbili teule za Kiswahili *Rosa Mistika* (1971) na *Tumaini* (2006), kuna mlingano kati ya waandishi wote katika kushughulikia hali mbalimbali za dhuluma zinazowakumba vijana wa kike. Waandishi wote wawili wamedhihirisha na kubainisha asasi zinazomkandamiza kijana wa kike kama vile utamaduni, mila, ndoa, elimu na uongozi katika jamii.

Ulinganifu uliobainika katika waandishi hawa wa kike na kiume ni kuwa wazazi wa kiume wa vijana wa kike ndio wanaochangia katika dhuluma nyingi zinazowakumba vijana wa kike. Waandishi hawa wote wamebainisha kuwa wazazi wa kiume wana misingi yenye mashiko katika mila na tamaduni zisizobadilika kamwe katika kuwadhulumu vijana wao wa kike. Wazazi wa kiume hawakubali mabadiliko ya kutaka vijana wa kike wapate ukombozi wao na kuwa huru katika maswala yanayowahusu kama vijana wa kike.

Waandishi hawa wote wameonyesha ulinganifu pale wanapoonyesha juhudi za vijana wa kike kuwa na ujasiri katika harakati za kutetea haki zao. Vijana hao wa kike wamebainishwa na waandishi kuwa na msimamo thabiti katika kupuuza itikadi na mila zenye imani iliyojikita kwenye misingi ya ubabedume.

Tofauti kati ya waandishi wa kike na wa kiume inabainika katika maelezo kuhusu athari zinazomkumba kijana wa kike kutokana na dhuluma kandamizi. Mwandishi wa kike anabainisha kuwa kijana wa kike hana ushupavu kamilifu wa kukabiliana na ukombozi dhidi yake. Mwandishi huyu wa kiume amehitimisha tungo yake kuwa kijana wa kike anashindwa kujikomboa na anaamua kujiua. Mwandishi wa kiume anadhihirisha kuwa kijana wa kike ni kiumbe dhaifu asiyeweza kuvumilia dhuluma na kujitegemea katika kujikomboa. Mwandishi wa kike kwa upande mwingine anadhihirisha ujasiri wa mhusika kijana wa kike katika kukabiliana

na athari za ubabedume na kuchukua hatua madhubuti na mwishowe kufaulu katika kujikomboa kutokana na dhuluma dhidi yake.

Mwandishi wa kiume amedhihirisha tofauti katika kuangazia dhuluma dhidi ya vijana wa kike kwamba vijana wa kike hukata tamaa anapokandamizwa na kudhulumiwa. Anaonyesha kwamba kijana wa kike si mvumilivu katika matatizo yanayomkumba ilhali mwandishi wa kike ameumba kijana wa kike kama mstahimilivu, mwenye moyo mgumu usiokata tamaa kamwe na anayepambana na kukabiliana na dhuluma kwa ujasiri.Moyo huu wa ujasiri na mgumu umeibuka kushinda katika kuleta ukombozi kwa kijana wa kike. Hivyo basi kufanikiwa kulingana nadharia tuliyoiteua ya kukomboa na kuweka huru vijana wa kike.

Utafiti wetu umeafiki dhumuni letu la mwisho kwenye utafiti huu kwa kuangazia ulinganishi na tofauti kati ya wandishi wa kike wa na kiume katika kushughulikia swala la dhuluma dhidi ya wahusika vijana wa kike.

Inabainika kuwa waandishi hawa wawili wanalingana na kutofautiana kwani wamempa kijana wa kike taswira chanya na hasi katika jamii. Taswira ya kijana wa kike kuwa hasi au chanya ni ya kawaida katika binadamu. Hali ya kijana wa kike kupewa taswira hasi au chanya imetokana na jinsi kijana mwenyewe anavyojichukua na wakati mwingine hutokana na mtazamo wa jamii yake. Taswira hasi anazopewa kijana wa kike hazifai kumvunja moyo bali anastahili kukabiliana na hali yenyewe ili aweze kupata sifa nzuri.

Inadhihirika kwenye matokeo ya utafiti kuwa huu kijana wa kike anakumbana na dhuluma tofauti tofauti kutoka kwa jinsia ya kiume. Vijana wa kike wamedunishwa, kuonewa, kuvunjiwa heshima, kudharauliwa na kunyimwa haki kwa sababu ya mtazamo wa kiume kuwa wao ni viumbe duni na dhaifu. Hali hii ya kudhulumu kijana wa kike imechangiwa na asasi za jamii ya Kiafrika kama vile mila na tamaduni zinazoendelezwa na mifumo ya jinsia ya kiume katika kuwadhalilisha na kuwadhulumu wale wa kike.

## 5.2 Mapendekezo ya Utafiti

Katika utafiti huu imebainika kwamba kijana wa kike anakumbana na dhuluma mbalimbali zilizojikita kwenye misingi ya ubabedume. Imedhihirika kwamba wazazi wa kiume ndio wanaochangia katika dhuluma nyingi zinazowakumba vijana wa kike. Katika kujikomboa kutokana na dhuluma hizi, utafiti huu unapendekeza kuwa wazazi wa kike wawe na ujasiri katika

kushirikiana na vijana wao wa kike katika kutetea ukombozi wa vijana wa kike. Aidha vijana wa kike waweze kuwa na ujasiri katika kupigania ukombozi wao ili kuepukana na dhuluma zinazowakumba.

Wandishi walioshughulikiwa waliangazia dhuluma za kijana wa kike na athari zinazotokana na kudhulumiwa kwao kutokana na jinsia ya kiume. Watafiti wa baadaye wanatarajiwa kuangalia swala la wanawake katika kuwadhulumu vijana wa kike.

Imebainika kwamba kijana wa kike anakumbana na dhuluma kutoka kwa jinsia ya kiume na ya kike kiasi kwamba inakuwa vigumu katika harakati zake za kujikomboa. Ili kuwe na mafanikio katika kujikomboa, kazi hii inapendekeza kwamba wanawake kwa wanaume wachukue hatua katika kushirikiana na kijana wa kike katika ukombozi wake.

Silaha kubwa ambayo imejidhihirisha kuwa inafaa kutumiwa na kijana wa kike katika kujikomboa ni kupata elimu. Mbinu hii ikifuatwa na kutumika vizuri, mbinu zingine za kujikomboa zitafuata bila kuwepo na matatizo. Kijana wa kike akipata elimu anaweza kujitetea binafsi na pia kuwatetea vijana wa kike wenzake na kuweza kujikomboa kutokana na dhuluma kandamizi zinazowadhalilisha.

Ukombozi wa kuwaweka vijana wa kike huru haupaswi kutengewa vijana wa kike tu bali ni tukio linalohitaji kushirikisha vyombo vya habari kama runinga, redio, majarida, magazeti, tovuti na kushirikisha mashirika ya kiserikali na ya kibinafsi katika kuleta mabadiliko kwenye jamii ambapo kijana wa kike yu huru.

Mwisho, tunapendekeza kuwa viongozi wanaoshiriki katika njama ya kuwadhulumu vijana wa kike wanapaswa kuchukuliwa hatua kali ili iwe funzo katika jamii katika harakati za kumweka kijana wa kike huru.

Aidha serikali na dini zichukue jukumu la kuelimisha vijana wa kike kupitia kwenye makongamano kuhusu hali ya dhuluma mbalimbali na athari zinazoibua kutokana na harakati za kumkandamiza huyu kijana wa kike. Vijana wa kike pia waweze kufundishwa haki zao na kuhizwa kuwa na ujasiri na misimamo thabiti katika kutetea ukombozi wao.

## 5.3 Tafiti za Baadaye

Katika utafiti huu tumeshughulikia swala la dhuluma dhidi ya vijana wa kike katika riwaya mbili za Euphrase Kezilahabi, *Rosa Mistika* (1971) na Clara Momanyi, *Tumaini* (2006). Tunapendekeza kuwa utafiti wa baadaye uchunguze jinsi vijana wa kiume wanavyodhulumiwa na wanawake katika jamii na kuweza kubainisha mikakati yao katika kujinasua kutokana na dhuluma hizo.

Utafiti wa baadaye unaweza pia kuchunguza jinsi vijana wa kike wanavyodhulumiwa na viongozi katika taasisi za kiserikali. Tukio hili linabainisha masaibu ambayo kijana wa kike anakumbana nayo kutokana na asasi ya uongozi katika tanzu zingine za fasihi ya kiswahili.

## MAREJELEO


Allen, J. W (1971) *Tendi*. Nairobi: Heineman Education Books

Banks, O ( 1990) *Faces of Feminnism*. Cambridge: Basil Blackwell.

Barbara Smith (1983) *Home Girls A Black Feministis Authology*. New York Women of Color

Baroness na Dr. John (2006) *This Immoral Trade*: Slavery in the 21St Century. England: Monarch Books.

Biblia, (2004) *Agano la Kale na Agano Jipya*. The Gideons International.

De Beauvoir's (1949) *The Second Sex. London:Pan Books Publishers.*

Eagleton( 1992) *Marxism and Literary Critism*. London: Routledge.

Eagleton, M (1986) *Feminist Literary Criticism*. New York: Longman

Freedman, E. B (2002) *No Turning Back. The History of Feminism And The Future of Women.* New York: The Ballantine Publishing Group.

George Alan (1982) *Shaping Your Child, Sexual Identity*. Michigan: Baker Book House.

Greer, G (1981) *The Female Eunuch*. London: Grafton Books.

Kabira, W and Nzioki, E (1993) *Celebrating Women Resistance*. Nairobi: African

Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2004) Nairobi:Oxford University Press.

*Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004). Nairobi: Oxford University Press.

Katola, E. (2006) *Udhalimu dhidi ya Wahusika Wanawake Katika Tamthilia Nne za Kiswahili*."

Kezilahabi, E. (1971) *Rosa Mistika*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Khaishani S.A na Njiro E. I (1993) *The Women's Movement In Kenya*, Nairobi. Association of African Women for Research and Development.

Kiango, S (1997) "*Taswira ya Mwanamke Katika Tamthilia za Kiswahili za Kenya*." Tasnifu ya MA Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Kiarie, K (1995) "*Uhakikiwa Taswira ya Mwanamke Katika Riwaya za S. A Mohamed*" Tasnifu ya

Kruger (1998) *Female characters in countemporay Kenya womens writers*: Figures of Subdued London: Longhorn Publishers.

Lugano, R. S (1989) "*Mwanamke katika Riwaya za Kezilahabi.*" Tasnifu ya MA, Chuo Kikuu MA Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Maina, V. (2005) *Nafasi ya Mwanamke Katika Tenzi mbili za Shabaan Robert*: Utenzi wa Hati na Utenzi wa Adila.Tasnifu ya M.A ch uo Kikuu cha Nairobi: (Hajachapishwa)

Maitrayee M and Franz W (2007) *Revisiting Gender Training. The Making and Remaking of Gender Knowledge.* Amsterdam: Kit and Oxfarm Publishers

Marie Kruger (1998) Her Essay "*Negotiating Gender Identity and Authority in the Plays of Penina*

Masibo, B (2009) *Gendered Perspective in the Novel of Ngugi Wa Thiong'o and Alice Walker.* Tasnifu ya Uzamifu Chuo kiuu Cha Nairobi.(Haijachpishwa)

Mbatiah, M. (2001) *Kamusi ya Fasihi.* Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing.

Mdee, J .N na Wengine. (2011) *Kamusi ya Karne ya 21.* Nairobi: Longhorn Publishers.

............................... (2009) *Kamusi ya Kamili ya Kiswahili.* Nairobi: Longhorn Publishers.

Millet, K (1970) *Sexual Politics*. New York.Double day and Company.

Mirikau, S. A (2011) *Taswira ya Mwanamke katikaTamthilia za K.W. Wamitila.* Tasnifu ya MA (Haijachapishwa).

Mlacha, S. A na Madumulla J. (1991) *Riwaya ya Kiswahili.* Dar-es Salaam:University Press.

Mohamed, S.A (1976). *Nyota ya Rehema*. Nairobi: English Press Ltd

.................. (1980) *Utengano.* Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.

.................. (1990) *Tata za Asumini*. Nairobi: Longhorn Publishers.

..................(2000)*Kitumbua Kimeingia Mchanga. Nairobi: Oxford University Press.*

Momanyi, C. (2006). *Tumaini*. Nairobi: Vide-Muwa.

............... (1998) "*Usawiri wa Mwanamke Muislamu Katika Jamii ya Waswahili Kama Inavyobainika Katika Ushani was Kiswahili*". Tasnifu ya PhD, Chuo Kikuu Cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Msokile, M (1990) *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi* . Nairobi: E.A.E.P

*Muhando, Ari Katini Mwachofia.*

Mukobwa, M. J (1985) *Maendeleo Katika ya Kimaudhui Katika Tamthilia Tano za Kiswahili.*

Mule, P. K (1991) *"Swala la Mwanamke Katika Tamthilia ya Kiswahili. Waandishi wa kike Katika Njia panda"* Tasnifu ya MA Chuo Kikuu cha Kenyatta. ( Haijachapishwa)

Mungai, P. K (2005) *Uhakiki Linganishi wa Tenzi za Mikidadi na Mayasa na Swifa ya Nguvumali.*

Mutua, J.M (2007) "*Mitazamo ya Vijana na Wazee Kuhusu Ukombozi wa mwanamke Katika*

Mwachofi, A. K (1987) *Mama ee*. Nairobi : East Africa Educational Publishers.

Ndungo, C.M (1985) "*Wanawake na Mabadiliko ya Kihistoria*." Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Njogu, K. naChimera, R (1999) *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu za Ufundishaji.* Nairobi :Jomo Kenyatta Foundation.

Nyaberi, H ( 1997) *Mwamko wa Wanawake Katika Tamthilia za Penina Muhando*" Tasnifu yz (MA) (Haijachapishwa).

Ogundipe Leslie (1984) *African Women, Culture and Another Development*. The Journal of African Marxists.

Ruth, S (1980) *Issues in Feminism*: An Introductory to Women's Studies. Londan: Mayfield Publishing Company.

Steady, F.C (1981) *The Black Women Cross-Culturally*. Cambridge: Schenkam Publishing Co.

*tamthilia tatu za Kiswahili*." Tasnifu ya MA Chuo Kikuu cha Nairobi

Tasifu ya Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

TUKI (1981*) Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford Univetsity Press.

Utenzi wa Adili Tasnifu ya Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachpishwa).

voices.

Wamitila K. W na Mbuthia, E. M (2003) *Mwongozo wa Kitumbua Kimeingia Mchanga*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Wamitila K. W (1999) *Nguvu ya Sala*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

………………… (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.*

……………… (2003) *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.

…………………..(2008) Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi Nairobi:Vide-Muwa

Wanjiku M. K. na Nzioki A. E. (1993) *Celebrating Women's Resistance*. Nairobi: New Earth

Warner, A (1934) *Utendi wa Mwanakupona- The Advice of Mwanakupona Upon the Wifely Duty*.

Wollstonecraft M (1792) *A Vindication of The Rights of Women. Harmondworth; Penguin*: Blackwell Publishers.